

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TATU**

**Kikao cha Pili – Tarehe 7 Novemba, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG.PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,  
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:**

1.      Toleo Na. 36 la tarehe 7 Septemba, 2018;
2.      Toleo Na. 37 la tarehe 14 Septemba, 2018;
3.      Toleo Na. 38 la tarehe 21 Septemba, 2018;
4.      Toleo Na. 39 la tarehe 28 Septemba, 2018;
5.      Toleo Na. 40 la tarehe 5 Oktoba, 2018;
6.      Toleo Na. 41 la tarehe 12 Oktoba, 2018;
7.      Toleo Na. 42 la tarehe 19 Oktoba, 2018; na
8.      Toleo Na. 43 la tarehe 26 Oktoba, 2018.

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG.PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 14

**Ukosefu wa Wauguzi na Vifaa Tiba – Kalenga**

**MHE. GODFREY W. MGIMWA** aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Kalenga katika kata na vijiji mbalimbali wamejitolea kujenga miundombinu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa zahanati na vituo vya afya lakini hakuna wauguzi na baadhi ya vifaa tiba.

Je, Serikali inaisaidiaje Halmashauri kuhusu tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Mgimwa, Mbunge wa Kalenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti,ili kutatua changamoto ya watumishi wa umma katika sekta ya afya, Serikali imeendelea kuajiri watumishi wa kada za afya kadri wanavyohitimu katika vyuo vya afya pamoja na hali ya bajeti inavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Julai 2018/2019 Serikali imeajiri watumishi 8,447 wa kada mbalimbali za afya. Kati ya hao Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ilipangija watumishi 68 ambapo vituo vya kutolea huduma za afya vilivyo katika Jimbo la Kalenga vilipata watumishi 40. Serikali inaendelea kutoa kipaumbele cha ajira kwa watumishi wa kada za afya ili kukabiliana na upungufu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la vifaatiba, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa inapokea fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya ambapo sehemu ya fedha hizo zinatumika kununulia vifaa tiba. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ilitumia shilingi 21,554,700 kwa ajili ya kununulia vifaa tiba ambavyo vilipelekwa katika vituo vya kutolea huduma za afya vilivyoko katika Jimbo la Kalenga. Vilevile Halmashauri inakusanya fedha za Mfuko wa Afya wa Jamii (*CHF*) ambazo kipaumbele cha matumizi kinapaswa kuwa ununuvi wa dawa na vifaa tiba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante; nitakuwa nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto kubwa kwenye vituo vyetu vya afya na zahanati na changamoto kubwa ni upatikanaji wa magari ambayo yanawasafirisha wagonjwa (*ambulance*). Ningependa kufahamu katika vituo hivi ambavyo tunavyo katika Jimbo la Kalenga vituo kama vinne, tuna gari mbili tu lakini moja linatumika kupeleka wagonjwa katika Jimbo zima. Ningependa kufahamu, je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba tunaongezewa gari hasa katika Kituo cha Afya cha Mgama? (*Makofii*)

Tuna changamoto kubwa ya madawa kwenye vituo vyetu vya afya na zahanati mbalimbali hasa katika Jimbo langu la Kalenga. Ningependa kufahamu kwa sababu vituo hivi vya afya vinatumika kwa wananchi wengi. Ningependa kufahamu katika Kituo cha Ng'enza, Kituo cha Itwaga na Kituo cha Muwimbi ni lini sasa madawa yataanza kupelekwa kwa sababu kuna vituo vimeshafunguliwa kuititia mwenge lakini mpaka sasa hivi havina madawa na havijaanza kufanya kazi, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maswali yake mawili ya nyongeza la kwanza anaulizia juu ya suala zima la upatikanaji wa gari (*ambulance*). Naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mgimwa, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba gari zinapatikana kwa kadri hali inavyoruhusu na hivi karibuni tunatarajia kupata gari 70 na katika gari hizo 70 ambazo tunatarajia kuzipata ni matarajio ya Serikali kwamba tutalenga katika maeneo ambayo yana upungufu mkubwa sana. Nina amini eneo la kwake kama ni mionganoni mwa maeneo ambayo yana upungufu mkubwa litakuwa *considered*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili anaulizia juu ya vituo vya afya vitatu ambavyo amevitaja kwamba vituo vya afya hivyo dawa hazipatikani. Naomba nikiri kwa fursa niliyopata ya kuzunguka katika maeneo yote ya Tanzania kwa mara ya kwanza ndiyo nasikia kwamba kuna vituo vya afya ambavyo havipati dawa. Ni vizuri tuwasiliane na Mheshimiwa Mbunge ili tujue tatizo ni nini kwa sababu ni azma ya Serikali kuhakikisha vituo vyote vinapokamilika na dawa ziweze kupatikana ili huduma iliyokusudiwa na Serikali iweze kupatikana kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja.Kwa kuwa ujenzi wa Kituo cha Afya Mboli ambapo hata Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI Jafo anakifahamu maana ndiyo barabara yake ya kwenda Chamkoroma kule. Na kwa kuwa kituo hiki hakijakamilika wamejenga wananchi, nilikwishawaomba shilingi milioni 500 TAMISEMI ili wakamilishe kituo kile.

Je, Serikali inasemaje kuhusu kutoa shilingi milioni 500 ili tuweze kukamilisha kituo kile ili wananchi wa Kata ya Matomondo, Kata ya Mlembule, Kata ya Chamkoroma na Kata ya Tubugwe waweze kupata huduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo. Waziri, Mheshimiwa Jafo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikiri wazi kwamba nishukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri kwa maeneo yale ya Mheshimiwa Mgimwa ambayo ndiyo Serikali imejipanga katika utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la Mheshimiwa Lubeleje ambaye mimi namwita greda la zamani makali yale yale, si muda mrefu nilikuwa naye kule Wilayani Mpwapwa takribani wiki tatu zilizopita tulikuwa Mpwapwa. Hata hivyo kutokana na mchango mkubwa wa Mzee Lubeleje sasa hivi tunakamilisha Kituo cha Afya cha Mima na ndiyo maana siku ile alitoa hoja ya Kituo cha Afya cha Mboli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jukumu la Serikali kuhakikisha wananchi wa maeneo mbalimbali watapata huduma. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lubeleje uwe na amani kwamba ni mpango wa Serikali kuboresha vituo vya afya na mionganini mwa vituo vya afya tutakavyoviimarisha ni Kituo cha Afya cha Mboli. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Jafo, tunaendelea na Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 15

#### **Ujenzi wa Mabweni**

**MHE. CATHERINE N. RUGE** aliuliza:-

Bado kuna kata ambazo hazina shule za sekondari hivyo kufanya baadhi ya wanafunzi kusafiri umbali mrefu kwenda na kurudi shulenii, kutokana na hali hiyo baadhi ya wazazi wameamua kuwapangishia vyumba watoto wao mitaani kwenye mazingira ambayo si salama.

Je, kwa nini Serikali isije na mpango mahususi wa ujenzi wa mabweni kama inavyofanya kwenye madawati ili kuwapunguzia wanafunzi hasa wa kike adha ya kutembea umbali mrefu kwenda na kurudi nyumbani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE.JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI napenda kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inamiliki na kuendesha shule za sekondari 3,634 Tanzania Bara. Kati ya hizo shule 3,519 ni za kutwa na shule 155 ni za bweni. Idadi hiyo ukillinganisha na kata 4,420 inabainisha kuwepo na kata ambazo hazina shule za sekondari hivyo zipo changamoto za baadhi ya wanafunzi kutembea umbali mrefu kufuata shule kwenye kata za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pendelezo la Mheshimiwa Mbunge la kujenga mabweni katika shule zote sekondari kuwa zuri, Serikali imeweka kipaumbele kujenga mabweni kwanza kwenye shule za kidato cha tano na sita pamoja na zinazoandaliwa kupandishwa hadhi kuwa za kidato cha tano na sita ambazo husajili wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi. Tangu mwaka 2014 Serikali imetumia shilingi bilioni 29.4 kujenga mabweni 298 kwenye shule za sekondari na mabweni 25 kwenye shule za msingi.

Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 15.7 kujenga mabweni 206 katika shule za sekondari na mabweni manne katika shule za msingi. Halmashauri zinahimizwa kuendelea kushirikiana na wananchi na wadau wengine kujenga shule za sekondari kwenye kata ambazo hazina shule na kujenga dahania (*hostel*) kwenye shule za sekondari zenye wanafunzi wanaotembea umbali mrefu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine swalii la nyongeza.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nachelea kusema *level ya seriousness* kwenye hili jambo bado ipo chini sana. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2019 Serikali ilitenga shilingi milioni 750 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika shule za sekondari kwenye kata zenyе mazingira magumu, lakini kwenye taarifa hii ya utekelezaji ukurasa wa 132 mpango huu umetekelvezwa kwa asilimia sita tu. Ningependa kufahamu, ukiwa umebaki mwaka mmoja kukamilika kwa mpango huu ni lini sasa Serikali itakamilisha ujenzi wa wabweni haya kwenye shule kumi ili kupunguza adha kwa wanafunzi wa kike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Serengeti yenye Kata 30 ina shule za sekondari kwenye Kata 21 tu na Kata 9 hazina shule za Kata. Kata hizo ni Lung'avule, Getasamo, Kiambai, Morotonga, Sedeko na kadhalika. Ningependa kufahamu ni lini sasa Serikali itakamilisha ujenzi wa shule za sekondari kwenye hizi kata tisa? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali haya ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ruge amenukuu Mpango wa Taifa wa miaka mitano na mimi kwa niaba ya Serikali napenda nimuhakikishie kwamba mpango ule tunaendelea kuutekeleza mwaka hadi mwaka na itakavyofika mwisho mwaka wa utekelezaji wa mpango wa miaka mitano, malengo mengi yaliyomo yatakuwa yametekelvezwa. Mheshimiwa Mbunge naomba asiwe na wasiwasi na awaarifu wananchi ambao anawawakilisha kwamba

tutatekeleza mpango ule na utakapofika mwisho wa mwaka utekelezaji wake tutakuwa tumefikia malengo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza kwenye Wilaya ya Serengeti kwamba ina kata 30; kata 21 zina shule za sekondari na kata tisa hazina shule za sekondari na akauliza lini tutajenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali lake la msingi ni wazi kwamba kata hizo ambazo hazina shule sekondari wanafunzi wake ni mionganii mwa wanafunzi ambaao wanatembea umbali mrefu kufuata shule kwenye kata za jirani. Nimehimiza kwenye jibu la msingi kwamba Halmashauri iendelee kushirikiana na wadau wengine pamoja na wananchi kuhakikisha kwamba Kata hizo zinaanza ujenzi wa shule na Serikali itaingia kusaidia mara watakapoanza ujenzi huo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joyce Sokombi.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Mkoa wa Mara ilionekana kwamba mtoto wa kike hana thamani kwa upande wa elimu. Sasa Serikali imeona kabisa kwamba kuna shida ya mabweni ya watoto wa kike. Mtoto wa kike anapotoka shule kwenda nyumbani anakwenda kufanya kazi za nyumbani na anapotoka tena nyumbani kwenda shulenii ni umbali mrefu anafika amechoka sana.

Kwa nini Serikali isichukue hatua ya haraka kuhakikisha inajenga mabweni katika shule za Mkoa wa Mara? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema ni kweli katika baadhi ya mazingira tunaweka kipaumbele kujenga mabweni kwa

mfano katika maeneo ya wafugaji na baadhi ya maeneo katika baadhi ya mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya kujenga mabweni kwenye kila shule ya sekondari nchini ni kubwa sana, lakini vilevile katika mazingira ambayo shule imesajiliwa kama shule ya kutwa kwa mazingira yake siyo vizuri sana kuweka mabweni wakati mtoto anaweza akatembea umbali wa kilomita mbili, moja ama mita 500 akafika shuleni. Kwa hiyo, ni jambo ambalo tunaliangalia *case by case* kwa mazingira na tunahimiza kwamba wazazi, wananchi na Halmashauri zjenge dahania (*hostel*) ambazo zitasaidia hasa watoto wa kike wasitembee umbali mrefu kwenda nyumbani na shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hicho ndicho kitu tunachohimiza na Serikali itawaunga mkono katika kuendesha yale mabweni. Shule ikipandisha hadhi tu ikapata hadhi ya kuchukua wanafunzi kutoka mikoa mingine, Serikali inaingiza mkono moja kwa moja hapo kusaidia, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasna Mwilima.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri ametuhamasisha Waheshimiwa Wabunge tuwahamasishe wananchi ili wawze kujenga shule za sekondari kwenye Kata ambazo hazina sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Kigoma Kusini tunazo shule mbili za sekondari; tunayo Shule ya Basanza na Shule ya Mwakizega, lakini kinachosikitisha ni kwamba tangu hizi shule wananchi wamejenga wameweka madarasa kumi, ofisi za walimu na sasa hivi wanakimbizana na maabara. *REO* Mkoa wa Kigoma na Ukaguzi hawataki kabisa kuzisajili hizi shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini TAMISEMI na Wizara ya Elimu hawakai pamoja na kuona ni jinsi gani shule ambazo mnatuhamasisha tuwaambie wananchi wajenge muwe pia mnazipa kipaumbele katika usajili? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA**

**NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimhakikishie dada yangu, Mheshimiwa Hasna kwamba TAMISEMI na Wizara ya Elimu tunafanya kazi kwa vizuri zaidi, ndiyo maana mimi na pacha wangu, Mheshimiwa Profesa Ndalichako tunakwenda vizuri, lakini hata hivyo naomba niwahakikishie kwamba tumefanya hamasa kubwa sana watu wajenge hizi shule kwa ajili ya kupunguza umbali wa watoto kusafiri na hasa kesi ya mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na inawezekana kuna maeneo mengine kuna *case by case*, naomba niichukulie kesi hii ya Mkoa wa Kigoma, Uvinza kuona kuna nini kinachoendelea. Lakini hata hivyo, naomba nitumie fursa hii kumuagiza Mkurugenzi wangu wa Elimu pale Ofisi ya Rais, TAMISEMI kufuatilia jambo hilo haraka iwezekanavyo ili mradi kwamba kama vigezo vyote vimekamilika kuweka mchakato wa haraka kuhakikisha shule hizo zinasaidiwa haraka iwezekanavyo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka. Aah, Mheshimiwa Waziri wa Elimu karibu sana.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa na nimesimama hapa kuwahakikisha Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yangu ndiyo inayohusika na usajili wa shule na hakuna urasimu wowote

katika kusajili shule. Kinachotakiwa ni kwamba wanapoomba usajili vigezo na masharti viwe vimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shule ambazo Mheshimiwa Mbunge, dada yangu, amezisema, bahati nzuri hizo shule nazifahamu na ukaguzi ulishafanyika. Kuna mapungufu ambayo yameonekana na hatua iliyopo sasa hivi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza ameshaji-*commit* kwamba ndani ya miezi mitatu, ifikapo Disemba, 2018 atakuwa amekamilisha mapugufu yaliyopo na timu yangu itarudi kukagua na kama viko vizuri usajili utatolewa kwa sababu tuko hapa kwa ajili ya kuweshesha juhudzi za wananchi watoto wakasome.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu. Tunaendelea na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 16

**Tathmini ya Utendaji wa Maafisa Kilimo na  
Mifugo Vijiji**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza:-

Hali ya sekta ya kilimo na mifugo katika Jimbo la Same Mashariki ni mbaya licha ya kuwepo wafanyakazi wa Serikali wanaosimamia sekta hizo kwenye Wilaya, Kata na hata Vijiji. Wengi wa wafanyakazi hao wanatumia muda mwingu kufanya kazi zao binafsi badala ya kuwasaidia wakulima na wafugaji kuleta mabadiliko katika sekta hizo.

(a) Je, Serikali inatumia kigezo gani kutathmini utendaji kazi wa waajiriwa hao kupima ufanisi wao?

(b) Je, Serikali ipo tayari kupunguza idadi ya waajiriwa hao waliopo vijiji ili fedha itakayookolewa kutoka katika mishahara yao isaidie kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji na malambo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwasimamia maofisa ugani kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara za Kisekta hutoa miongozo inayoainisha viwango vya kitaalam na ikama. Mamlaka za Serikali za Mitaa husimamia masuala ya kiutawala na utendaji kazi wa siku kwa siku ikiwemo kupima ufanisi na tija kwa kutumia Mfumo wa Wazi wa Upimaji wa Watumishi wa Umma (*Open Performance and Review Appraisal System – OPRAS*) ambapo kila mtumishi hukubaliana na mwajiri kuhusu malengo yatakayotekelawa kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bado kuna upungufu mkubwa wa maafisa ugani wa kilimo na mifugo nchini, badala ya kupunguza idadi yao, mpango uliopo kuititia llani ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 22(b) ni kuongeza idadi ya Maafisa Ugani kutoka 9,558 waliokuwepo mwaka 2014 hadi 15,082 ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwakumbusha maafisa ugani wote na wasimamizi wao kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yaliyowataka Maafisa Ugani kutokaa ofisini na badala yake kwenda vijijini kuwasaidia wakulima na wafugaji. Nazikumbusha mamlaka za nidhamu kuchukua hatua kali dhidi ya Maafisa Ugani wazembe wasiowajibika kwa umma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaboyoka swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme tu kwamba kwa kuwa Serikali imeonekana inapeleka pesa kidogo sana ya maendeleo kwenye sekta hii ya kilimo hasa katika jimbo langu na kwa hiyo Maafisa Ugani wanakuwa wanakosa kazi za kufanya. Je, Serikali haioni ni kupoteza hela za Serikali kama watazidi kuongeza waajiriwa wakati hawana kazi za kufanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; ni wazi kwamba Maafisa Ugani hawa wanaopelekwa kwenye vijiji hawajawahi kufanyiwa semina, wengine wana miaka kumi, wala *orientation* ya kwamba kazi ambazo wanatakiwa wazifanye kwa kipindi hiki ni nini na kwa kuwa ukijua kwamba kozi wanazochukua haziko *specific* kwenye mazao yale, mtu ametoka kulima korosho leo anapelekwa kwenye ndizi, hajui hata kutengeneza migomba.

Je, Serikali haioni kwamba haijawatendea haki maafisa ugani hawa wanaopelekwa vijiji bila kufanyiwa semina na *orientation* za kuwafanya waelewe kile wanachotakiwa kufanya katika vijiji au kata zile pamoja na kwamba pia hawana vitendea kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza amesema kwamba Serikali inapeleka bajeti ndogo, nimwambie tu kwamba bajeti inayopelekwa na Serikali Kuu katika Halmashauri ni sehemu ndogo tu ya bajeti ya jumla ambayo Halmashauri inatakiwa ifanyie kazi. Maana yake kule kuna bajeti ya ndani inaitwa *own source budget*. Kwa hiyo hakuna sababu yoyote inayokubalika inayomfanya Afisa Ugani ye yeyote aseme kwamba ameshindwa kwenda kijijini eti kwa sababu ya bajeti ndogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili amesema kwamba kuna Maafisa Ugani wamepelekwa kule lakini hawana ujuzi na mazao husika. Sisi Serikali tunachokifanya tunapeleka Afisa Ugani ambaye amesomea Sekta ya Kilimo, Sekta ya Mifugo kwenda kufanya kazi za

ugani katika Halmashauri fulani, sasa akikuta kule kuna zao fulani mahususi ni kazi yake kujiridhisha kupitia tena, kudurusu documents mbalimbali zinazohusu zao hilo mahususi ili awe vizuri kitaaluma na kiuendeshajji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakubaliana naye kwamba mtu ambaye amesoma *general agriculture* akienda kwenye zao la tumbaku *specific* atalazimika kukosa baadhi ya utaalalm katika zao lile, ni kweli, lakini tunawahimiza kwamba lazima wahakikishe kwamba wanalifahamu hilo zao vizuri na waweze kuwashauri wakulima vizuri kwa sababu wao ni wataalam wa kilimo. Kama mimi ni mchumi lakini nilisoma shule ya kilimo nakumbuka masomo ya kilimo wakati ule, je mtu ambaye amesoma cheti au *diploma* au *ana degree* ya kilimo, lazima atakuwa anajua vizuri zaidi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze pia na mimi kujibu swalii la mama yangu, Mheshimiwa Kaboyoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba na mimi niongezee hapo kidogo kwamba sisi kama Wizara ya Kilimo kupitia vyuo vyetu vyote vya mafunzo nchini, swalii ambalo na mimi niliweza kulijibu jana, ni kwamba tumefanya mpango mkakati hata wale Maafisa Ugani ambao pia bado hawatoshelezi na tumesema wasikae ofisini, lakini tuna mpango mkakati kama Wizara ya Kilimo kuhakikisha kwamba tunawajengea uwezo hata wale ambao Maafisa Ugani wako maofisini ili waweze kutoa mafunzo kwa wakulima kuendana na mazao ambayo yapo katika hayo maeneo. Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa. Uliza swali Mheshimiwa Mariam Kisangi atafuatiwa na Mheshimiwa Selasini.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matatizo ya ukosefu wa Maafisa Ugani inawakumba wananchi wa Jimbo la Ukonga katika Wilaya ya Ilala katika kata za Kitunda, Vigewe, Majowe na Mzinga. Wananchi wa eneo hilo ni wakulima wa mbogamboga na matunda lakini kuna Afisa Ugani mmoja anahudumia kata tatu, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Maafisa Ugani katika Jimbo la Ukonga na Wilaya ya Ilala kwa ujumla?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna upungufu wa Maafisa Ugani nchini, na kama nilivyojibu kwenye swali la msingi ni kwamba kwa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi tunahitaji kuongeza Maafisa Ugani ambapo tukiwafikia hawa ambao tumeponga kuwaongeza kuititia maelekezo ya Ilani tunaamini tutakuwa na Maafisa Ugani wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali ina kibali cha kuajiri watumishi takribani 52,000 na mpaka sasa hivi hatujafikia hata 20,000 katika kuajiri, kibali ambacho kitatoka hivi karibuni labda mwezi wa pili au wa tatu, tutaajiri Maafisa Ugani wa kutosha kupunguza tatizo lililopo. Naamini tutakapoajiri hao kabla ya mwezi wa sita na kata hizo ambazo umezitaja tutazipatia Maafisa Ugani. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi tukizungumza Maafisa Ugani tunazungumza zaidi habari ya maafisa hawa wa kilimo, lakini kuna wanaohusika na uvuvi, kuna wanaohusika na ufugaji na ni dhahiri kwamba upungufu ni mkubwa.

Sasa swalii langu ni hili, kuna maeneo kama Jimbo langu la Rombo vijana ambao wamesoma kwenye vyuo vya kilimo, vyuo vya uvuvi na vyuo vya ufugaji wanajitolea kusaidia wakulima au wastaifu wanajitolea kuwasaidia wakulima na wanatumika vizuri sana. Je, Serikali iko tayari kuwatambua hawa na kuwasaidia ili waendelee kuwasaidia wakulima wakati utaratibu wa kuongeza watumishi wengine ukiendelea kufanyika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swalii hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya kujitolea au *volunteering* kwa Tanzania na vijana wetu na wengine wastaifu, kwa wastaifu kidogo naona inatia matumaini lakini kwa vijana ambao wamemaliza vyuo bado haijaingia vizuri katika fikra zao.

Mimi nadhani katika nchi kama India huwezi kupata ajira kabla kwanza hujapata uzoefu kuititia hata kujitolea, kwa hiyo tunahamasisha sana pale ambapo wapo wataalam wetu ambao wanaweza wakajitolea kwenye kijiji, Halmashauri ifikirie namna ya kuwaratibu na kuwapatia posho kidogo ili waweze kufanya kazi zao vizuri sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunamalizia swalii la mwisho kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo aulize swalii lake.

Na. 17

## **Bagamoyo Kupanda Hadhi ya Halmashauri ya Mji**

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA** aliuliza:-

Mji Mdogo wa Bagamoyo ulianzishwa tarehe 15/6/2005. Mwaka 2013/2014 Mamlaka hiyo iliomba Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupewa hadhi ya Halmashauri ya Mji baada ya kujiridhisha kuwa na sifa stahili.

Je, ni lini Serikali itaipa Bagamoyo hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria za Serikali za Mitaa Sura 287 (Mamlaka za Wilaya) na Sura 288 (Mamlaka za Miji), pamoja na mwongozo wa Serikali kuhusu uanzishwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2014, mapendeleko ya kupandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo kuwa Halmashauri ya Mji yanapaswa kujadiliwa kwanza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya (*DCC*) na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*) kabla ya kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maombi hayo yalijadiliwa katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo tarehe 28, Septemba, 2018 (mwaka huu), na Kamati ya Ushauri ya Wilaya (*DCC*) tarehe 06, Oktoba, 2018 na kwa kuwa hayajadiliwa kwenye Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*) ambao wamepanga kikao hivi karibuni, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inamuomba Mheshimiwa Mbunge awaarifu

wadau wa Mji wa Bagamoyo wawe na subira hadi taratibu hizo zitakapokamilika na uamuza kufikiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na nitahamasisha wadau kuvuta subira. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, wakati tunaendelea na mchakato wa kupata Halmashauri ya Mji wa Bagamoyo, je, ni lini Serikali itawaagiza Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kuwalipa Wenyeviti wa Vitongoji malimbikizo yao ya posho ambayo hayajalipwa kwa mda mrefu sasa?

Mheshimiwa Mwenyeekiti, swali la pilli; kwa vile Bagamoyo siyo Halmashauri ya Mji kwa hiyo hatuna fursa ya mafungu makubwa ya ujenzi wa miundombinu ya barabara. Sasa naomba kujua ni nini kauli ya Waziri kuhusu kutusaidia Bagamoyo mafungu ambayo yatatuwezesha kujenga miundombinu ya barabara na mifereji ambayo iko katika hali mbaya sana katika Mji wa Bagamoyo na Vijiji vya Bagamoyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyeekiti, kwanza nimpongeze na kumshukuru kwa kukubaliana na majibu kwenye swali la msingi na hili la kuwaomba wananchi wawe na subira wakati mchakato unaendelea, namshukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, katika swali lake la kwanza amesema kwamba Wenyeviti wa Vitongoji hawajalipwa kwa muda mrefu na mimi napenda kumhimiza Mkurugenzi wa Halmashauri wa Wilaya ya Bagamoyo kutekeleza maagizo ya Serikali ambayo yanamtaka arejeshe asilimia 20

ya mapato yanayokusanywa kutoka kwenye kata husika ili yatumike, pamoja na kazi zingine, kulipa posho za Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji kwenye maeneo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili amesema Mji wa Bagamoyo kweli una mahitaji ya miundombinu kama barabara na mifereji na amesema kwa usahihi kabisa kwamba itakapokuwa ni Halmashauri ya Mji ambayo inatakiwa iwe na sifa fulani kwa upande wa miundombinu sasa tuanze kupeleka mafungu kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu hiyo. Mimi namuomba sana Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane hata baada ya Kikao hiki cha Bunge ili tuone ni namna gani mwakani tunaingiza kwenye bajeti ya *TARURA* huu ujenzi wa miundombinu ambao anaipendekeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa Bagamoyo, Mji Mdogo wa Mbalizi ulianza mchakato wa kuomba iwe ni Halmashauri ya Mji kwa muda mrefu sana. Je, ni lini Serikali itaipa Mbalizi kuwa na hadhi ya Halmashauri ya Mji? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Jafo majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wanavyofahamu Wabunge wengi sana humu, kuna mapendekezo mbalimbali ya maeneo mbalimbali kuanzisha mamlaka mpya lakini najua kwamba Mbalizi ni miongoni mwa maeneo ambayo yalikuwa katika mchakato wa kupandishwa hadhi, lakini nimuombe Mheshimiwa Mbunge kwamba tuvute subira kwa sababu mpango wa Serikali wa sasa hivi wa maelekezo ni kutoanzisha mamlaka mpya lakini kwa vile jambo hili liko katika subira tuvute subira pale halii

itakapokuwa sasa imekaa vizuri Mji wa Mbalizi ni miongoni mwa miji ambayo itapewa kipaumbele cha kwanza katika upandishaji wa hadhi. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Selemani Jafo. Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa swali linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua, Mbunge wa Masasi sasa aulize swali lake.

Na. 18

### **Ukosefu wa Bima ya Afya kwa Wanajeshi**

**MHE. RASHID M. CHUACHUA** aliuliza:-

Kumekuwepo na malalamiko kwa upande wa huduma za afya kwa wanajeshi wetu kwamba hawana bima ya afya kwa sababu Jeshi lina zahanati na hospitali zake.

Je, Serikali haioni haja ya kuwapatia wanajeshi wetu bima ya afya?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGWA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuanzishwa kwake hadi sasa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limekuwa likitumia utaratibu wa wanajeshi kupata huduma za matibabu kupitia hospitali na vituo vya afya vya Jeshi kwa gharama za Serikali kama ambavyo imeainishwa kwenye Sheria ya Ulinzi wa Taifa, Kanuni ya 26 na 27 ya Kanuni za Majeshi ya Ulinzi Juzuu ya Kwanza (Utawala) ambazo zinabainisha kuwa huduma za matibabu kwa maafisa, askari na wategemezi wao zitaghamiwa na Serikali na zitakoma pale utumishi unapokoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa yapo malalamiko kuhusu huduma za tiba. Malalamiko hayo yanatokana na huduma kutokidhi mahitaji halisi kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha kugharamia dawa na vifaa tiba katika hospitali za Jeshi. Hivyo, kutokana na mapungufu na changamoto zilizopo umeonekana umuhimu wa kuwa na Mfuko wa Bima ya Afya wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutimiza azma hiyo taratibu zinakamilishwa ambazo zitapelekwa katika Mamlaka mbalimbali za Serikali ili kupata ridhaa ya kuwa na Mfuko wa Bima ya Afya kwa ajili ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chuachua swali la nyongeza.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza kwa kuwa watumishi wa umma nchi nzima karibuni wote wanatibiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*) na wanajeshi pia ni watumishi wa umma. Je, Serikali haioni kwamba kuanzisha mfuko mwingine kunaleta urasimu na ucheleweshaji usio wa lazima badala yake watumie mfuko wa *NHIF*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili lini mfuko huo sasa unaokusudiwa kuanzishwa utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzisha mfuko mwingine hakutaleta urasimu bali kutaleta fedha ambazo kwa kweli zitatusaidia katika kutimiza mahitaji halisi ya jeshi. Kama mnavyoifahamu taasisi hii ni kubwa na ina watu wengi na

kwa maana hiyo ikiwa na mfuko wake sisi tunahisi kwamba hilo litakuwa ni jambo zuri zaidi litaweza kutimiza azma yetu ya kujenga hospitali za jeshi maeneo kadhaa na kuweza kutoa huduma zilizo kuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pili ni kwamba lini tutaanza kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba tuko katika taratibu za kisheria sasahivi kukamilisha mchakato na kuupeleka katika mamlaka mbalimbali zinazohusika na pindi itakapokuwa tayari basi suala hili litatolewa taarifa rasmi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mfumo wa matibabu wa wanajeshi ni kutibiwa katika hospitali ambazo ziko kwenye makambi ya majeshi ambazo ni chache sana. Tatizo linakuja pale kwa wategemezi wa wanajeshi hao hususani wake, wanafunzi ambao wanasoma shule za bweni ambao hawako katika hayo makambi. Hili limepelekea mzigo mkubwa wa hao wanajeshi kuwashudumia watu ambao hawaishi nao katika makambi.

Je, Serikali haioni sasa umefika wakati kuwapunguzia wanajeshi hao kuwashudumia hawa watu na kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambao utawahudumia hizi familia zao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,kama nilivyosema ufumbuzi wa tatizo hilo analolizungumzia Mheshimiwa Mlinga ambalo ambapo anazungumzia kwamba wategemezi ambao hawako karibu na maeneo ya makambi wanakosa huduma za tiba na ndiyo maana tunataka kuanzisha mfuko huu bima kwa ajili ya jeshi. Tutakapokuwa na mfuko huu basi

wataweza kupata huduma popote wakipewa kadi zile ambazo zitakuwa zinatumika jeshini.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa hiyo mimi nadhani ufumbuzi uko katika uanzishwaji wa mfuko huu na tutafanya kila linalowezekana ili uanze mapema ili kuondoa tatizo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf swali fupi la nyongeza halafu mwisho Mheshimiwa Munira.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ni ukweli ulio wazi kwamba wanajeshi wetu wanafanya kazi ngumu katika mazingira magumu na wakati mwingine wanapata ulemavu wa maisha.Je, mbali na hii Bima ya Afya sasa ambayo imekuja kwa sasa kuna wale ambao hata walipigana vita na kupata ulemavu kwa kuikomboa nchi yetu katika vita vya Kagera, Wizara yako inawaangaliaje wale wanajeshi ambao wanapata ulemavu wa kudumu ili waweze kupata tiba mpaka mwisho wa maisha yao? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upo utaratibu ndani ya jeshi wa kuwashudumia wale ambao wamepata matatizo ya kiafya wakiwa kazini na huwa zinafanyika Bodi za Kitaalum za Utibabu na wanapata fidia kwa ulemavu, lakini vilevile wanatibiwa katika vituo hivi vya jeshi vinavyotoa huduma za afya.

Sasa ni kweli kwamba huduma hizo hazikidhi haja kwa sababu baadhi yao hawapo karibu makambi ya jeshi na ndiyo maana tunasema kwamba tukianzisha huu Mfuko wa Bima kwa ajili ya Jeshi la Ulinzi tutaweza kuwashudumiwa hawa vizuri zaidi kwa sababu kwanza tutakuwa tuna fedha zaidi na pili tutafanya *accreditation* ya hospitali kadhaa ambazo wao watakuwa karibu nazo ili kuweza kupata huduma hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munira swali fupi la nyongeza.

**MHE. MUNIRA MUSTAFA KHATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanajeshi wanapokuwa jeshini wanakuwa wanafanya kazi ngumu kweli, lakini wanapo staafu tu mara nyingi wanapata maradhi tofauti tofauti.

Je, Serikali hamuoni sasa ni wakati mwafaka wastaafu wa jeshi kupatiwa Bima ya Afya? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati najibu swali la msingi ni kwamba kanuni za sasahivi, zinasema matibabu yatakoma pale utumishi unapokoma. Lakini katika suala hili la kuanzisha bima la afya tumelifikiria hilo, tunatambua kwamba wanaohitaji matibabu wale walio staafu wanahitaji zaidi kuliko waliopo kazini.

Kwa hiyo kwa sababu mfuko huu utakuwa una fedha za kutosha tutaweza kutoa huduma hiyo ya tiba kwa wale ambao wako kazini pamoja na waliostaafu. Kwa hiyo, mimi nadhani Waheshimiwa Wabunge karibu matatizo yote haya ambao yanakabili eneo hilli kwa sasa ni kwa sababu ya ukosefu wa fedha ambao ufumbuzi wake upo katika uwanzishwaji wa huu Mfuko wa Bima.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Kujenga Taifa Mheshimiwa Hussein Mwinyi, tunaendelea na Wizara ya mambo ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na.19

### **Ajali Zitokanazo na Bajaji na Bodaboda**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Usafiri wa bodaboda na bajaji umeshamiri katika maeneo ya mijini na vijiji, pamoja na usafiri huo kusaidia ajira kwa vijana kwa kiasi kikubwa umekuwa ukisababisha ajali nyingi.

(a) Je, ni ajali ngapi zimesababishwa na vyombo hivyo tangu kuanza kwa huduma hiyo?

(b) Je, ni vijana wangapi wamepoteza maisha yao na wangapi wamepoteza viungo vyao?

(c) Je, Serikali inawaambia nini Watanzania kuhusu hali hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu vyombo vya miguu miwili bodaboda na miguu mitatu bajaji kuanza kutumika kama vyombo vya usafiri mwaka 2008 hadi kufikia Septemba 2018 vimesababisha jumla ya ajali 38,237.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, watu ambao walipoteza maisha kutohana na ajali za bodaboda kuanzia mwaka 2008 hadi kufikia Septemba 2018 ni 8,237 na waliopoteza viungo vyao katika kipindi hicho ni 37,521.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haitakubali kuona watu wengi kiasi hiki wakiendelea kupoteza maisha katika vyombo hivyo. Hivyo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Polisi kikosi cha Usalam barabarani kwa kushirikiana *SUMATRA* na wadau wengine wengi ambao wanashirikiana na vyombo hivyo itaendelea kusimamia kwa kanuni za usafirishaji kwa njia ya bodaboda ili kuhakikisha ajali hazitokei na wananchi wanakuwa salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fakharia Shomar swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru kwa maelezo mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, ambayo hivisasa imekuwa kama mwiba kwa waendesha bodaboda wote hapa nchini; na maswala mawili ya nyongeza.

(a) Je, kwa kuwa watu mbalimbali ambao wanaoendesha vifaa vyaa aina mbalimbali ikiwa magari kwa bodaboda ikiwa ndege na kadhalika huwa wanapata ajali, je Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuanzisha mfuko ambao mfano *Compensation Fund* kwa wale wote wanaopata ajali ambayo inakuwa ni ajali ya kupata ulemavu wa kudumu na inakuwa hawezi tena kujitegemea na familia yake inamtegemea ili kumuondokea makali ya yale yallyomfika? (*Makofi*)

(b) Je Serikali kwanini haileti sheria ya kuwadhibiti bodaboda ambao wanaoendesha vipando hivo bila ya kufuata sheria ambayo tayari wanausemi wanaosema kwamba fuata sheria, bila kushurutishwa sasa bodaboda nao wakawa wanaweza kuikubali kauli hiyo kwamba kufuata sheria bila kushurutishwa? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo ya nyongeza Mheshimiwa Naibu wa Mambo ya Ndani.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kwanza

kuhusu utaratibu kwa ujumla wake wa matibabu nadhani Waheshimiwa Wabunge ninyi mashahidi juu ya mafanikio makubwa kuititia eneo hili kuititia Wizara ya Afya katika kuhakikisha kwamba wananchi wa nchi hii wanapata huduma bora zaidi za matibabu ya afya ikiwemo kuhakikisha kwamba mkakati wa kuhakikisha wananchi wanapata bima za afya na kuititia utarabu huu. Ni imani yangu kwamba hata hao ambao wanapata ajali za bodaboda wakijiunga katika mifuko hii ya huduma za afya na kutumia fursa mbalimbali za uimarishaji wa sekta ya afya ikiwemo kuimarisha hospitali zetu na matibabu na madawa itaweza kusaidia kupunguza changamoto ya majeruhi ambao wnapata ajali za bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusiana na sheria nimuhakikishie kwamba tuko katika mchakato ambao tumefikia katika hatua mzuri sana za mabadiliko ya Sheria ya Usalama Barabarani kwa ujumla wake ambayo itagusa maeneo mengi. Naamini kabisa sheria hiyo itakapokuwa imekamilika na kuja hapa Bungeni kuitisha itsaidia sana kupunguza kwa kiwango kikubwa ajali za barabarani nchini.

**MWENYEKITI:** Haya ngoja nianze huku Mheshimiwa Balozi Adadi.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swala la ajali ambazo zinatokana na bodaboda ni suala la msingi sana na ambalo linaongoza sasa hivi nchini. Kuna mapendekezo mbalimbali ya kurekebisha sheria ya usalama barabarani, na mapendekezo hayo yamekuwa kwenye Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa muda mrefu na mara ya mwisho Waziri wa Mambo ya Ndani alilihakikisha Bunge hili kwamba mapendekezo hayo yatakuja hapa Bungeni. Nataka Serikali/Waziri wa Mambo ya Ndani atuambie ni lini mabadiliko hayo ya sheria usalama barabarani yatakuja hapa Bungeni?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali Mheshimiwa Naibu Waziri Sheria ya Mabadiliko ya mwaka 1973.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza siyo sahihi kwamba mchakato ule umekwama Wizara ya Mambo ya Ndani. Lakini kama mnavyofahamu kwamba mchakato wa mabadiliko ya sheria unapitia katika hatua mbalimbali. Kwa hiyo, kitu ambacho nimekizungumza katika swali langu la msingi na ambalo naendelea kulisisitiza hapa ni kwamba dhamira ya Serikali ni njema na hatua ambayo tuliyofikia ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa hiyo tutarajie kwamba si muda mrefu itakuja. Ni muombe Mheshimiwa Adadi na Waheshimiwa Wabunge wavute subira na waiamini Serikali kwamba sisi tunaona uhitaji wa sheria hii ni mkubwa zaidi kwa sababu changamoto ya ajali barabarani imekuwa bado inaendelea kutatiza wananchi wetu na kupoteza maisha na kusababisha ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa hiyo Serikali inachukulia kwa uzito. Lakini lazima hatua hizi za kitaratibu ziweze kupitiwa ili tuweze kuleta kitu ambacho kimekuwa kimekaa vizuri zaidi kwa Wabunge, baada ya kuharakisha jambo ambalo linaweza halijakaa vizuri sana. Kwa hiyo Mheshimiwa Adadi na Waheshimiwa Wabunge ni wahakikishie kwamba muda siyo mrefu pengine nadhani labla mwanzoni mwa mwaka ujao tunaweza sheria hii tukaleta Bungeni ili iweze kupitishwa na Wabunge na ianze kutumika rasmi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi uliyonipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudzi za Serikali kuweza kupunguza ajali hapa nchini kwa sasahivi zinazoongoza ni za magari ya Serikali na ajali hizi zinasababishwa na mwendo kasi wa madereva wa Serikali, lakini wakielekezwa na mabosi wao wanaowaendesha kwamba waende mwendo kasi huku wakiwashaa *full light* barabarani na hawasimamishi popote, lakini matokeo yake

wanasababisha ajali. Je, Sheria za Usalama Barabarani haziyahusu magari ya Serikali? Ahsante.

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwa kuguswa na ajali ambazo kwa siku za karibuni tumeona zikihusishwa pia magari ya Serikali, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwamba katika kufuata sheria za barabarani kila mtu anapaswa afuate sheria hizo. Hakuna utofauti kati ya dereva wa gari la Serikali kuvunja sheria na dereva mwingine yeote na ndiyo maana hivi karibuni tumetoa mwongozo kwa ajili ya madereva wa magari ya Serikali kwamba watii sheria za nchi hili na tumeshatoa maelekezo kwa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kwamba kuhakikisha kwamba wanawakamata madereva wa Serikali wanaovunja sheria, wanawapeleka mahabusu waweke ndani na baadae baada ya mahakama kuamua na sisi tutahakikisha kwamba tunawanyang'anya leseni ama kupunguza madaraja yao ili wakose sifa za kuendesha magari ya barabarani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti,kama hiyo haitoshi tutaendelea kuhakikisha kwamba tunasimamia kama Serikali utaratibu wa kuweza kutoa elimu kwa madereva hawa waweze kupata mafunzo ya ziada ili waweze kujua sheria za usalama barabarani na kuendesha hususani mafunzo ya kuendesha viongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa upande wa viongozi nao wenywewe ikiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge tuliokuwemo humu ndani tuhakikishe kwamba hatuwi sehemu ya kushajihisha ama kuhamasisha madereva wetu waendeshe gari kwa kasi. Pale tunapoona kwamba dereva anavunja sheria sisi tuwe wa kwanza katika kumrekebisha ili tuweze kuokoa maisha yake, maisha yetu na maisha ya watu wengine ambao wanatumia barabara. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kutokana na muda tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Edwin Amandus Ngonyani, Mbunge wa Namtumbo sasa aulize swalı lake.

Na. 20

**Makubaliano ya Uanzishwaji WMA ya Mbarang'andu**

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI** aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali imeshirikiana na Taasisi ya *PAMS Foundation* ya Ujerumani kuunguza zao la mpunga kwa dawa ya kutokomeza magugu lilitolimwa na kuotesha mwaka 2018 na wanakijiji wa Kata ya Mchomoro kinyume na makubaliano ya kuanzisha *WMA* ya Mbarang'andu?

(b) Je, ni lini Serikali italipa fidia wakulima wa Kijiji cha Mchomoro walioathirika na kuvunjika kwa makubaliano ya uanzishwaji wa *WMA* ya Mbarang'andu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swalı hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Edward Amandus Ngonyani, Mbunge wa Namtumbo lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PAMS Foundation* ni Shirika Lisilokuwa la Kiserikali ambalo lina Ofisi zake Arusha, Dar es Salaam, Manyara na Tunduru, Mkoani Ruvuma. Shirika hili linatoa misaada mbalimbali kwa Jumuiya za Hifadhi za Maliasili kwa Jamii yaani *WMAs* nchini, ikiwemo Jumuiya ya Mbarang'andu ya Wilaya ya Namtumbo. *PAMS Foundation* inasaidia jumuiya hiyo katika kuwajengea uwezo viongozi wa jumuiya viongozi wa Serikali za vijiji na kata katika

kusimamia maliasili, kutoa mafunzo ya askari wa wanyamapor wa vijiji yaani *VGS* na kutoa vitendea kazi zikiwemo sare, *GPS*, darubini na kamera ili kutekeleza majukumu yao ya kulinda maliasili kwa kufanya doria kwa ufanisi zaidi. Aidha, Taasisi ya *PAMS Foundation* ilishirikiana na *WMA* ya Mbarang'andu kuteketeza mimea vamizi iliyokuwemo ndani ya maeneo ya hifadhi ya Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makubaliano ya uanzishaji wa *WMA* ya Mbarang'andu yalifanyika kati ya wananchi wa vijiji saba vinavyounda Jumuiya hiyo ikiwemo Kijiji cha Mchomoro kwa lengo la kusimamia eneo lao pamoja lilitengwa kwa ajili ya hifadhi kwa mujibu wa Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapor na makubaliano hayo bado hayajavunjika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji saba vinavyounda Jumuiya ya Mbarang'andu inayosimamia eneo la *WMA* kwa niaba ya wananchi husika ni Mchomoro, Kitanda, Nambecha, Lukuyusekamaganga, Songambele, Kilimasera na Mtewawamwahi. Aidha Serikali haina mpango wa kulipa fidia kwa wakulima wa kijiji cha Mchomoro kwa kuwa Jumuiya hiyo ilianzishwa na wananchi wenye kwa makubaliano ya kuendeleza uhifadhi na kulinda ushoroba wa Pori la Akiba la Selous Tanzania ambalo linaelekea kule ni Niassa nchini Msambiji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amandus Ngonyani swalil ya nyongeza.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa na kabla sijauliza maswali yangu mawili ya nyongeza nilitaka kumpungeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kufika Namtumbo na kuziona changamoto halisi za Wanamtumbo.

Lakini vilevile niipongeze Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kumpokea Mkuu wangu mpya wa Wilaya ya Namtumbo na kumpa taarifa sahihi kuhusu masuala ya Mbarang'andu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasema nini kwa maafisa wake walioko katika Wilaya ya Namtumbo wanaowapotoshaviongozi na Wananchi wa Wilaya ya Namtumbo kuwa Jumuiya za *WMA* za Mbarang'andu, Kimbanda na Kisungule ni maeneo ama hifadhi ya Serikali kuu na hivyo wananchi waliounda Jumuiya hizo hawana uwezo wakupunguza ama kupanua maeneo hayo kwa nia ya kuweka mipaka ya shughuli za hifadhi na za kilimo?

(b) Taasisi za *PAM Foundations* na *WWF* zinafanyakazi nzuri za kuwajengea *WMAs* za Mbarang'andu, Kimbanda na Kisungule. Je, Wizara iko tayari kuzishawishi taasisi hizo zikubali kuwawezesha hao wana Jumuiya ya *WMA* kuititia upya mipaka ya maeneo yao na hivyo kuondoa mgongano wa maeneo ya uhifadhi kilimo na ufugaji badala ya kufadhili *operations* za kuwatweza wakulima na...

**MHE. JOHN W. HECHE:** Anasoma swalii.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** ...peke yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru sana kwa pongezi alizozitoa kwenye Wizara tunashukuru sana na tunazipokea na tunamuahidi kwamba tutaendelea kushirikiana nae katika kuhakikisha majukumu yake yanakamilika ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maeneo ya *WMAs*, *WMAs* zote zinamiliikiwa na vijiji vinavyohusika na ni maamuzi ya vijiji vinavyohusika katika kuhakikisha kwamba hayo maeneo yanahifadhiwa na Wizara inasaidia kuhakikisha kwamba michakato yote ya kisheria inafuatwa ili kusudi Waziri

wa Maliasili na Utalii atangaze maeneo hayo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba kama wakitaka kubadilisha kwa mujibu wa Sheria na kwa mujibu wa Kanuni mpya za tarehe 3 Agosti, 2018, kifungu cha 38(6) na kifungu 68 vinatoa maelekezo kwa vijiji vinavyohusika na hizo jumuiya kama mojawapo ya kijiji kinataka kujitua katika hilo. Sasa kama wanataka kupunguza lazima warudi kwenye mikutano ya vijiji vinavyohusika waamue kwa pamoja kwamba hilo eneo labda lipunguzwe au lifanyeje. Hayo yako miongoni mwa majukumu walijonayo wao wenye, sisi tutakachokifanya ni ku-*facilitate* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwamba Wizara iko tayari kushirikiana na *PAMS Foundation*, tuko tayari kushirikiana lakini cha msingi lazima tukubaliane kwamba maeneo yaliyohifadhiwa kama tumekubaliana yamehidadiwa kwamba maeneo hayo yatumike kwa ajili ya hifadhi za wanyamaporu yataendelea kutumika kama hifadhi za wanyamaporu. Hakuna shughuli zozote za kibinadamu, ama ufugaji, ama kilimo kinachoruhusiwa katika hayo maeneo mpaka hapo maeneo hayo yatakapobadilishwa kwa mujibu wa Sheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga sasa aulize swali lake.

Na. 21

### **Kufuta Hati za Mashamba Yaliyotelekezwa**

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA** aliuliza:-

Serikali iliahidi kuyafutia hati mashamba yaliyotelekezwa.

Je, ni lini Serikali itafuta hati za mashamba yaliyotelekezwa yaliyoko Wilayani Mkinga na kuwagawia wananchi ardhi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO  
YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kijibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kubatilisha miliki za ardhi za mashamba yaliyotelekezwa katika maeneo mbalimbali nchini. Katika kipindi cha Disemba, 2015 mpaka Oktoba, 2018 mashamba yenye ukubwa wa hekari 84,240.8 yamebatilishwa. Mashamba haya yapo katika Halmashauri za Ngorongoro, Arumeru, Moshi Wilaya, Kinondoni Manispaa, Kigamboni Manispaa, Kilombero, Kilosa, Mvomero, Iringa Wilaya, Bukoba Wilaya, Tarime, Kibaha Wilaya, Serengeti, Busega, Muheza, Lushoto na Mkinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Mkinga shamba namba 278 Mkomazi miliki yake ilibatilishwa tarehe 20 Juni, 2018. Shamba hili lenye ukubwa wa hekari 15,442 lilituwa likimilikiwa na Kampuni ya *Mkomazi Plantation Limited* na hati namba 4268, 9780 na 9781. Baada ya kubatilishwa kwa miliki za shamba hili, Serikali ya Mkoa wa Tanga kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga zipange sasa matumizi upya ya shamba hili kwa kuzingatia mahitaji ya ardhi katika eneo husika na kipaumbele kikiwa ni mahitaji ya Wananchi na ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuzihimiza Halmashauri zote Nchini kubaini mashamba yaliyotelekezwa, kutuma ilani kwa wamiliki wa mashamba hayo kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, Sura Namba 113 na kuwasilisha mapendekezo katika Wizara yangu ili hatua ya kubatilisha miliki za mashamba hayo ziweze kufanyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kitandula swalii la nyongeza.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipeende kutumia fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Mkinga kuishukuru sana Serikali kwa kufuta hati tatu za mashamba liliolokuwa likimilikiwa na *Mkomazi Plantation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maswali, ili nia hii njema iweze kufanyiwa kazi ipasavyo, busara inatutuma kwamba shamba hili lifanyiwe matumizi bora ya ardhi. Je, Serikali kwa nia hiyo njema iko tayari kuiwezesha Halmashauri ya Mkinga kifedha ili tuweze kufanya matumizi bora ya ardhi na hatimaye tuweze kuigawa ardhi hii kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, Wilaya ya Mkinga ni Wilaya ambayo inakabiliwa na tatizo kubwa la radhi yake kuhodhiwa na watu wachache lakini ardhi hiyo wameitelekeza. Sasa miongoni mwa mashamba ambayo tulitoa ilani ya kufuta hati zake ni shamba la Kwamtili lenye ukubwa wa takribani hekta 1,150. Nini kauli ya Serikali kuhusu ufutaji wa hati ya shamba hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza nipokee shukrani alizozitoa kwa niaba ya Waziri lakini swalii lake la kwanza ameuliza kwamba kwa kuwa tayari mashamba haya yamefutwa na yanahitaji pengine kufanyiwa mpango wa matumizi ya ardhi na moja ya mashamba hayo ni hilo la *Mkomazi Plantation*. Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Kitandula kwamba Wizara ina nia njema kabisa kuhakikisha kwamba yale mashamba yanayofutwa yanawekewa mpango mzuri wa matumizi na moja ya mamlaka za upangaji ni Halmashauri zenyewe lakini kwa

sababu changamoto kubwa katika Halmashauri nyingi ni rasilimali fedha kwa ajili ya upangaji, sisi kama Wizara tayari tulikwishanunua vifaa vya kupimia ambavyo viko tayari kwa ajili ya kuzisaidia Halmashauri zote zitakazotaka msaada huo lakini pia tunaangalia namna bora ya kuweza ku-mobilise resources ili kuweza kuzisaidia Halmashauri ambazo tayari zimeweka mipango mizuri na tayari tulikwishaanza na wezetu wa Kibaha. Kwa hiyo tuko tayari pia kuwasaidia wenzetu wa Mkinga kuhakikisha kwamba eneo linalofutwa linapangwa vizuri.

Swali la pili ameulizia shamba la Kwamtili ambalo nalo walileta kwa ajili ya ufutwaji. Shamba la Kwamtili ni moja kati ya yale mashamba yaliyoko kwenye ile *Mkomazi Plantation*, kwa hiyo kwa hali hiyo maana yake na lenyewe liko katika ule mkumbo wa yale mashamba matatu ambayo yenye hati tatu ndani ya lile shamba. Kwa hiyo lile lolote ambalo linakuwa limekamilisha katika kufuata taratibu linafutwa kwa sababu lilishaletwa na kwa utaratibu lilishakamilisha vile vigezo vyote ambavyo vilikuwa vinatakiwa. Kwa hiyo naomba uondoe hofu na lenyewe liko katika mchakato ule ule.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsantekwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongenza.

Matatizo yaliyoko huko Mkinga yanafanana kabisa na yaliyopo katika Jimbo la Manyoni Magharibi. Shamba la Kitaraka *Cattle Holding Ground* ambalo lina hekari 45,000 limetelekezwa kwa muda mrefu na mmiliki wake ambaye Shirika liliokufa la *Tanganyika Packers* na Serikali kuititia Msajili wa hazina lakini katika Bunge hili tukufu kumekuwa na majibu mara nyingi kwamba itasaidia shamba hili kulifuta na kulirudisha katika Halmashauri ya Itigi ili kuondoa mgogoro ambaao unawachoinganisha wananchi na Serikali yao hii nzuri ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Tano.

Je, ni lini sasa Serikali itafuta shamba hili na kulirejesha kwa Halmashauri ya Itigi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli shamba hilo la *Kitaraka Cattle Holding Grounds* ambalo limetelekezwa kwa muda mrefu liko chini ya umiliki wa Msajili wa Hazina na mashamba yote ambayo yanakuwa na umiliki uliokuwa ndani ya Serikali hayawezi kufutwa sambamba na yale mengine ambayo yametelekezwa, yana utaratibu wake wa kuangalia namna bora ya kufuta ukizingatia sasa hivi tunaelekea kwenye Tanzania ya viwanda, hatuwezi kuyabatilisha mashamba yote ya Serikali na tukayarudisha kwa wananchi. Yanarudishwa kwa wananchi pale tu ambapo kweli Serikali inakuwa haina mpango nalo katika shamba hilo, kwa hiyo lile shamba asubiri mpaka pale Msajili wa Hazina atakapokuwa amelipotea maelekezo mengine na tutatekeleza kile ambacho kitakuwa kimeamuliwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mbunge mpya wa Korogwe.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mashamba yaliyotelekezwa Mkinga linafanana sana na tatizo tulilokuanalo kule Korogwe Vijijini na muda mrefu Serikali imekuwa ikiombwa kusaidia kufuta mashamba haya lakini bado haijafanikiwa na tayari Halmashauri ya Wilaya ilishatoa mapendekezo ya kufuta mashamba 28, lakini mpaka leo hatujapata majibu yoyote wala hatujui kinachoendelea.

Swali langu, ni nini kauli ya serikali juu ya mashamba yaliyotelekezwa katika Jimbo la Korogwe Vijijini likiwemo shamba la Hale yanayowanyima wananchi nafasi ya kuweza kufanya shughuli za kilimo? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa swali lake zuri na swali lake la kwanza akiwemo Bungeni, hongera sana, lakini naomba nimhakikishie kwamba juhudzi za Serikali zinaendelea kuhakikisha kwamba mashamba yote yaliyotelekezwa yanafutwa na kama siku zote tunavyosema wanaoanza mchakato ni Halmashauri husika kwahiyio wakiyaleta mashamba hayo sisi tutafuata utaratibu huo lakini mpaka sasa tuna msahamba 15 ambayo yako tayari yameombewa kwenye kufutwa na katiba ya hayo sita yanatoka kwenye Jimbo lake.

Kwa hiyo, na hilo analolizungumza basi tutalifuatilia tuweze kujuia kama kweli watakuwa wametimiza vigezo wao ndiyo watakaotuthibitishia na Wizara itakuwa tayari kulifanyiakazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi sasa aulize swali lake.

Na. 22

#### **Usalama wa Usafiri wa Majini**

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS** aliuliza:-

Historia ya nchi yetu katika usafiri wa majini imekumbwa na ajali kubwa na mbaya ambazo zimegharimu maisha ya watu. Mfano wa ajali hizo ni MV Bukoba, MV Skagit na MV Spice Iceland.

Je, Serikali bado inakumbuka ajali hizo na ina mikakati gani endelevu kuhakikisha usafiri wa majini ni salama kwa maisha ya Watanzania?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA  
MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto zilizopo katika usafiri wa majini nchini. Katika kuhakikisha changamoto hizo zinatatuliwa, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha na kuimarisha usalama wa usafiri huo kwa kutunga sheria na kanuni zinazosimamia usalama wa usafiri majini. Aidha, katika kuimarisha usalama wa usafiri wa majini, Serikali pia imekuwa ikiendesha mafunzo ya vyeti vya umahiri kwa mabaharia. Mafunzo hayo yanatolewa katika viwango vya kimataifa na yanatambuliwa na Shirika la Bahari Duniani yaani *International Maritime Organisation* kuititia Mkataba wa Utoaji wa Vyeti vya Mabaharia yaani *The International Convention on Standards of Training, Certification and Watchkeeping for Seafarers of 1978*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kuimarisha usafiri na udhibiti wa usafiri wa majini nchini, Serikali ilitunga Sheria namba 14 ya mwaka 2017 na kuititia sheria hii Serikali ilianzisha Shirika Maalum la Udhibiti wa Usalama wa Vyombo vya Majini ambalo pia litashughulikia na uwakala wa meli za mizigo ya Serikali yaani *The Tanzania Shipping Agency Corporation (TASAC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na jitihada hizo, Serikali pia imeweka utaratibu wa ukaguzi na utoaji wa vyeti kwa vyombo vya majini zikiwemo meli. Ukaguzi huu hufanyika angalau mara mbili kwa mwaka lengo likiwa ni kijiridhisha na usalama wa vyombo hivyo katika kutoa huduma ya usafiri wa majini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf swalii la nyongeza.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Hivi juzi tu tarehe 22 Septemba, Kivuko cha MV Nyerere kikiwa karibu na bandari yaani masafa mafupi kufika bandarini kilizama. Ukosefu wa vyombo vyaa kisasa vyaa uokozi imepelekeza kupoteza maisha ya watu wengi sana.

Je, Serikali ina mkakati gani kuwa na vyombo vyaa uokozi vyaa kisasa ambavyo vinaweza kufanyakazi saa zote 24? Tumeshuhudia kwamba uokozi wetu tulikuwa tunafanya mchana, usiku tunapumzika wakati watu wanapoteza maisha kwa hiyo nataka kujuu, je, Serikali ina mkakati gani kuwa na vyombo vyaa kisasa vyaa kuweza kufanyakazi saa 24?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, amesema hapa Mheshimiwa Waziri katika majibu yake kwamba kuna sheria mpya zimetungwa na Kanuni kuzimamia usalama wa vyombo vyaa maji vyaa usafiri wa maji lakini siyo tatizo sheria mpya wala kanuni mpya. Sheria zilizopo hazisimamiwi na ndiyo zinazosababisha uzembe wa kupoteza watu maisha. Nataka kumpa mfano Mheshimiwa Waziri; mwaka 1996 ilizama MV Bukoba; mwaka 2011 imezama MV Spice Iceland...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali lako.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga hoja, hili suala siyo mchezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 imezama MV Skagit. Tume zote zilizoundwa zimehakikisha kwamba vyombo hivi vilikuwa chakavu halafu vimepakia kupita uwezo wake watu na abiria. Je, leo Serikali inatoa tamko gani juu ya uzembe unaofanywa na mamlaka hizi ambazo zinasimamia vyombo vyaa baharini? Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikanza na suala la mkakati wa kudhibiti vyombo vya usafiri wa maji; kwanza tumezia matumizi ya Meli aina ya landcraft ambayo yalikuwa yanasaababisha ajali yasisafiri mwendo mrefu. Kwa kufanya hivyo tunaamini kabisa tutaokoa ajali nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kama nilivyozungumza kwenye jibu langu la msingi tunafanya ukaguzi wa meli zetu mara mbili kwa mwaka na kutoa *certificate* maalum ambazo zinasimamiwa na *TASAC* kuhakikisha kwamba meli zote zimefanyiwa ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunashirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, tunashirikiana na KMKM, lakini tunashirikiana na *Fire Brigade*, tunashirikiana na ZMA vilevile tunashirikiana na ZBC kuhakikisha kwamba uokozi unafanyika mara tu inapotokea. Vilevile nimhakikishie Mheshimiwa Mheshimiwa Mbunge kwamba kuititia *TASAC* sasa hivi kuna mtambo maalum ambao tunautumia uko pale kabla hujavuka kwenda Kigamboni unaoitwa *Maritime Rescue and Coordination Centre*. Hiyo inagundua ajali imetokea sehemu gani na tunawasiliana na vyombo vyote vinavyohusika kwa ajili ya kufanya uokozi wa haraka na tumekuwa tukifanya hivyo kuhakikisha kwamba tunaokoa raia wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kutosimamiwa sheria, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sheria zinasimamiwa isipokuwa kuna changamoto mbalimbali ambazo zinatokea kuhusu *monitoring* ya mizigo na abiria, utaratibu uliopo kuititia *TASAC* tumewaelekeza Mamlaka ya Bandari Tanzania pamoja na Mamlaka ya Bandari ya Zanzibar kuangalia zile taratibu zote za idadi ya abiria wanatakiwa kuingia kwenye meli pamoja na mizigo yao kwa maana ya ile orodha ya *man first*, kabla hawaajaingia na wanapokwenda kushuka inatakiwa ilingane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tumekuwa tukipata changamoto na zile bandari za pembezoni ambazo hatuna stafu wa kutosha na hilo tunalizingatia kwa kupeleka wafanyakazi wa kutosha maeneo yale ili abiria na mizigo iende sambamba na uwezo wa meli ambazo zimesajiliwa rasmi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Tunaendelea na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo.

Na. 23

### **Maeneo Yasiyo na Mawasiliano Ya Simu- Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Wilaya ya Urambo ilishawasillishwa Serikalini orodha ya maeneo yasiyokuwa na mawasiliano ya simu.

Je, ni lini maeneo hayo yatapata mawasiliano ya simu?

### **NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba nijibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge aliwasilisha Serikalini jumla ya kata tisa zenye takribani vijiji 27 kama ifuatavyo: Kata ya Uyumbu vijiji vinne, Kata ya Ugalla vijiji viwili, Kata ya Usisya vijiji viwili, Kata ya Kiloleni vijiji viwili, Kata ya Vumilia vijiji viwili, Kata ya Uyogo vijiji vitano, Kata ya Ukondamoyo vijiji viwili, Kata ya Kasisi vijiji vitat na Kata ya Nsenda vijiji vinne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) ilivainisha vijiji vilivyopo

Jimbo la Urambo katika Kta ya Uyumbu, Imalamakoye na Songambele na kuviiingiza katika miradi ambayo utelezaji utakamilika mwaka 2019 ambapo jumla ya vijiji 11 tayari vitafikishiwa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, maeneo ya Kata tisa yaliyoombewa mawasiliano na Mheshimiwa yataainishwa ili kufahamu mahitaji halisi ya kufikisha huduma ya mawasiliano na hatimaye yatainggaingizwa kwenye orodha ya miradi itakayotekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta swalii la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana lakini kabla sijaauliza maswali mawili ya nyongeza naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama hapa Bungeni siku ya leo kwa sababu ndio siku ya tarehe 7 Novemba ambayo Mwenyezi Mungu alimuita Mume wangu Marehemu Samuel Sitta huko aliko mbinguni, namuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo; nilipata nafasi ya kuingia katika mtandao wa ujenzi na mawasiliano nikaona orodha ya Wilaya na Kata nydingi nichini ambazo zitapata huduma ya mawasiliano katika mwaka huu wa fedha, lakini kwa bahati mbaya Wilaya ya Urambo haimo, je, Serikali inawahakikishajie wananchi wa Urambo kwamba nao watapata huduma ya mawasiliano katika mwaka huu wa fedha? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili kuna Kata ambazo hazina mawasiliano lakini wakati huo minara imejengwa, lakini haifanyi kazi kwa mfano Kata ya Ukondamoyo na kwagineko, je, Serikali inawaambiaje wananchi wa Urambo kuhusu kupata huduma ya mawasiliano ahsante sana? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyezekiti, ni kweli mwezi wa nane tulitoa orodha ya vijiji na kata mbalimbali ambazo zitafikishiwa huduma ya mawasiliano lakini tulitoa kwa baadhi ya kata na baadhi ya mikoa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba inapofika mwishoni mwa mwezi huu wa Novemba kuna kata nyingine ambazo zitapelekewa mawasiliano baada ya maombi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, swali lake la pili minara iliyojengwa na hakuna mawasiliano, ni kweli kuna baadhi ya minara ambayo tayari imeshawekwa maeneo mbalimbali lakini haijawashwa na kuna sababu mbalimbali za kutowasha minara hiyo mojawapo ikiwa ni masuala ya mazingira, lakini tumekwishafanya kazi vizuri sana na Ofisi ya Makamu wa Rais kuhakikisha kwamba tunapata vibali kuhakikisha kwamba hiyo minara inawashwa. Vilevile kuna uzembe tu ambao tumeendelea kuufuatilia kutoka kwenye makampuni yanayohusika ambayo mara nyingi ni Halotel na wengine kuhakikisha kwamba wanawasha hiyo mitambo ili wananchi waweze kupata mawasiliano. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa muda umemalizika, tunaendelea na Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali Mbunge wa Manonga.

Na. 24

#### **Ukarabati wa Barabara ya Simbo – Nkinga – Choma**

**MHE. SEIF K. GULAMALI** aliuliza:-

Wakati wa kipindi cha mvua barabara nyingi nchini zimekuwa zikiharibika ikiwemo barabara ya Simbo – Nkinga – Choma.

Je, ni lini Serikali kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) itaanza kuikarabati barabara hiyo ili kuondoa adha zilizopo njiani?

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Simbo – Nkinga – Choma ni sehemu ya barabara ya Mkoa za Puge – Ziba kilometra 83 na Ziba - Choma kilometra 26.6 zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mahitaji ya matengenezo kwa barabara hii katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya shilingi bilioni 1,129.105 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Puge – Ziba – Choma ikiwa ni pamoja na sehemu ya Simo – Nkinga – Choma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kiasi hicho cha shilingi bilioni 1.129 sehemu ya Puge – ziba imetengewa shilingi milioni 809.305 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida na ya muda maalum na shilingi milioni 90 kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha changarawe sehemu ya barabara ya Ziba – Choma imetengewa shilingi milioni 229.8 kwa ajili ya mmatengenezo ya kawaida na ya muda maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) imeshatangaza zabuni kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii na mkandarasi ameshapatikana na hivyokazi ya matengenezo zimepangwa kuanza hivi karibuni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwan Gulamali swalii la nyongeza.

**MHE. SEIF K. GULAMAMLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii moja ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kipindi cha kampeni na hata baada ya kampeni alikuja kushukuru pale akiwa Ziba kwamba barabara hii itawekewa kiwango cha lami. Lakini pili barabara hii inaunganisha Mkoa wa Tabora na Shinyanga kupitia Ziba – Choma mpaka Shinyanga yenyewe, lakini tatu barabara hii ina uhitaji wa maeneo hasa maeneo hasa hasa Mikoa ya Katavi, Kigoma, Shinyanga hasa ikizingatiwa barabara hii ina hospitali kubwa ya rufaa ya Nkinga; je, Serikali haioni sasa ifikie muda sasa barabara hii iwekewe lami ili kuondoa adha za watumiaji wa barabra hiyo? Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii na ndio maana katika jibu langu la msingi tumesema tumetenga fedha za kutosha ili kuhakikisha barabara hii inapitika na wananchi wanaendelea kupata huduma bora. Kuhusu kufanya ujenzi wa lami na kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais niseme tu kwamba ahadi zipo nyingi na ahadi hizi maeneo mengi zipo na zinatofautiana ukubwa kati ya maeneo na maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo utekelezaji wake upo 100% yako maeneo ambayo tuko 50% kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais na yako maeneo ambayo tunaendelea kutekeleza. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Manonga kwamba barabarai tutaaingiza kwenye utaratibu wa kawaida kwa maana ya kwamba tunao mpango mkakati kwa hiyo barabara hii tumeichukua kwa ajili ya kuitazama siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango mkubwa ulikuwa sasa hivi ni kuuunganisha mikoa kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema Mkoa wa Tabora ulikuwa bado haujaunganika vizuri na mikoa mingine ndio maana iko miradi mikubwa inayoendelea sasa hivi kuunganisha Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Katavi, kuunganisha Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Mbeya, kuunganisha Mkoa wa Tabora na Mkao wa Dodoma na maeneo mengine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge uvute subira eneo hili tumelichukua kwenye mpango mkakati siku za usoni tutaweza kuiunganisha kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo nakushukuru sana kwa kufuatilia na sisi tuko makini kuhakikisha kwamba huduma bora zinapatikana maeneo yote ya nchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano muda unamalizika tunamalizia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto, Mheshimiwa Venance Methusalah Mwamoto, Mbunge wa Kilolo sasa aulize swalı lake.

Na. 25

**Mkakati wa Kitaifa wa Kupunguza Vifo vyakina  
Mama na Watoto**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO** aliuliza:-

Kulingana na mkakati wa kitaifa wa kupunguza vifo vyakina wanawake na watoto wa 2016 – 2020 Tanzania inakusudia kuongeza matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango kutoka 32% ya 2015 hadi 45% ifikapo 2020 na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka 556 kwa kila vizazi hai 100,000 ya mwaka 2015 hadi 292 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo 2020. Hii ni kutokana na Tanzania kuwa sehemu ya mpango wa kimataifa uitwao *Ending Preventable Maternal Mortality (EPMM)* unaozitaka nchi zote kupunguza vifo hivyo hadi 140 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo mwaka 2030. Hata hivyo tafiti zinaonesha kasi ya sasa ya haiwezi kutufikisha kwenye malengo yaliyokusudiwa ambapo kasi 3.4% au zaidi ndiyo inaweza kutufikisha huko:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba malengo yaliyowekwa yanatimia?

**NAIBU WAZIRI AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venance Methusalah Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, Mkoa wa Iringa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli takwimu za mwaka 2016 zimeonesha kwamba vifo vy ya akina mama hapa nchini vitokanavyo na uzazi ni 556 kwa kila vizazi hai 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hapojuu napenda kullaarifu Bunge lako tukufu kuwa Wizara yangu inatekeleza Mpango Mkakati wa Pili wa Kuboresha Huduma ya Afya ya Uzazi, Mama, Watoto na Vijana kwa mwaka 2016 hadi 2020. Mkakati umejikita zaidi kutekeleza Malengo Endelevu ya Maendeleo (*SDGs*) Duniani na Mkakati wa Nne wa Sekta ya Afya. Mkakati huo umeeleza bayana kuwa ili kupunguza vifo tunahitaji kuhamasisha matumizi ya uzazi wa mpango, matumizi mazuri ya wataalam wa uzazi kwa maana wakunga na madaktari, uwepo wa huduma za dharura za uzazi na mtoto mchanga na kuwa na mazingira yaliyowezesha katika utoaji huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kuboresha huduma bora za dharura za uzazi na mtoto mchanga zenyе uwezo wa kufanya upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni (*caesarean section*) kwa kusogezza karibu na wananchi ambapo ujenzi na ukarabati wa vituo zaidi ya 208 unaendelea nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeajiri watumishi wapya wenye nia ya kuziba pengo la uhitaji na watumishi wengine wamepelekwa kusoma kupata kada zinazohitajika kufanya upasuaji mfano watoa dawa za

usingizi, manesi watanza vyumba vya upasuaji na kadhalika. Sanjali na hilo upatikanaji wa damu salama sasa ni lita 239,937 malengo ni yalikuwa ni lita 700,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha jana tarehe 6 Novemba, 2018 hapa Jijini Dodoma Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia suluhu Hassan alizindua kampeni ya Jiongeze Tuwavushe salama ambayo ni kampeni ya Kitaifa iliyolenga kuzuia vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga hapa nchini. Madhumuni ya kampeni hii ni kuhamasisha viongozi wa Serikali, viongozi wa dini, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, wadau wa maendeleo, watoa huduma za afya, familia na jamii kwa ujumla ili kuchangia katika juhudhi za Taifa za kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi na vifo vya watoto wachanga. Sherehe pia iliudhuriwa na Wakuu wa Mikoa kumi kwa niaba ya Wakuu wa Mikoa wote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhemwi Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na jitihada kubwa ambazo Serikali inafanya kupunguza vifo vya akinamama na watoto na kwa takwimu ambayo ninayo kila siku mama 30 wanafariki na kwa mwezi akinamama 916 na kwa mwaka akina mama 11,000, naomba niombe Serikali kwa kuwa tulitoa hamasa kwa wananchi kwenye kata na vijiji kwamba wajenge kwa nguvu zote zahanati ili kupambana na jambo hili na baadhi ya zahanati hasa kwenye Jimbo langu la Kilolo hazijaezekwa pamoja na wananchi kufanya jitihada hizo, je, Serikali sasa haioni ni wakati muafaka wa Wizara ya Afya na Wizara ya TAMISEMI kushirikiana kwa pamoja ili kuweza kumalizia zahanati hizo ambazo wananchi wametoa nguvu zao nyingi katika kujenga? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili pamoja na jitihada kubwa ambazo imefanywa na Serikali lakini jambo

lingine ambalo linachangia vifo hivi ni umasikini ulikithiri na sasa hivi ninavyozungumza bei za mbolea kwenye vijiji ni imekuwa ni balaa, mwaka jana imepanda kwa 10% ukilinganisha na bei ya mwaka jana hivyo kuongeza ongezeko la umaskini kwenye vijiji vyetu na kuongeza vifo kwa sababu akinamama wengi wanashindwa kupata lishe bora kwa sababu wanashindwa kupata mbolea.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuangalia upya bei ya mbolea ili kupunguza vifo hivyo vya akinamama na watoto? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hapa si ujenzi wa zahanati, tunachohitajika kufanyika ni kuhakikisha akinamama wajawazito kwanza wanakwenda kupata huduma za afya pindi pale wanapobaini wanapata ujauzito. Kwa takwimu ambazo tunazo sasa hivi ni kina mama wanaokwenda mara moja katika kipindi kizima cha ujauzito ni kama 90% lakini ambaao wanakwenda mara nne kwa mujibu wa taratibu sisi zetu watu wa afya ni takribani 65% hivi na akinamama ambaao wanajifungulia katika vituo vya kutolea huduma ya afya ni takribani kama 64%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi kama Serikali tunahimiza kina mama kwanza kuwa na afya bora ya uzazi kwa maana kupanga idadi ya watoto ambaao wanahitaji na ambaao wanaweza wakawahudumia, lakini la pili tunasisitiza kwamba kina mama pindi wanapokuwa wajawazito waweze kwenda kliniki ili kuweza kupata ushauri mzuri kwa kitabibu. Lakini vilevile tumekuwa tunahimiza kina mama wajawazito kujifungulia katika vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya. Vifo vya akinamama vinatokea katika maeneo gani, maeneo makubwa matatu; kwanza mama kutofika katika kituo cha kutolea huduma kwa wakati, lakini pili pale mama anapofika katika kituo cha kutolea huduma kwa wakati je, alipata huduma sahihi kwa wakati na alionwa

na mtu ambaye ana utalaam ule kwa wakati; tukiweza kuyaweka hayo yote kwa na ambayo na sisi kama Serikali tunaendelea kuyafanya nahakika kabisa vifo hivi vingi tunakuwa tumevipunguza na mimi niendelee kumweleza Mheshimiwa Mbunge kweli kwa sababu hizi takwimu ambazo tunazo sasa hivi ni za mwaka 2015/2016 ninaamini tutakapofanya tena utafiti wetu mwaka 2019/2020 tutaona kwamba kumekuwa na pungufu kubwa sana vifo vyakina mama na watoto kwa sababu Serikali imeweke mikakati ya kuhakikisha kwamba tumevipunguza vifo hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swalii lake la pili Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na hali ya umaskini, ni kweli vifo vingi na idadi ya watoto kwa akina mama takwimu zinaonesha kwamba mwanamke anapokuwa anapata elimu zaidi idadi ya watoto inapungua, lakini vilevile mwanamke anapokuwa hali yake ya umaskini imepungua idadi ya watoto nayo inapungua na watoto wake wanaweza wakaishi vizuri na ndio sisi kama Serikali kwa kushirikiana na Wizara nyingine tumeweka msisitizo kuhakikisha kwamba watoto wote wanapata elimu bure ambayo kwanza inamsaidia kumuweka mtoto wa kike hadi anafika kidato cha nne ambapo anakuwa na miaka 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo kwa kupitia mpango wa TASAFU tumeweza kuziwezesha kaya maskini hili la pembejeo na uwezeshaji mwagine ambao tumeufanya kupitia Wizara yangu ya kuwezesha vikundi vyakina mama na vijana ni moja ya mikakati ya Serikali kuhakikisha kwamba tunanyanya wanawake kiuchumi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa umuhimu na maslahi ya wanawake na watoto Tanzania naomba nitoe fursa kwa watu wawili tuulize Mheshimiwa Khadija Nassir na Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. KADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *rate* ya watoto wenye udumavu inakadiriwa kuwa 34% nchini ukizingatia Tanzania tunongoza katika uzalishaji wa chakula. Sasa ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuanzisha programu ya lishe bora kwa wamama wajawazito katika vituo vyetu vya afya ili kupungu za tatizo hili? Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo zuri kabisa na muhimu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Khadija Nassir kwa kufanya ufuatiliaji mkubwa sana kuhusiana na masuala ya lishe kwa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa takwimu; hali ya lishe inaendelea kuboreka n dani ya nchi yetu. Utafiti tuliofanya mwaka 2010 hali ya udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano ilikuwa ni asilimia 42. Baada ya miaka mitano (mwaka 2015) hali ya udumavu imeshuka mpaka asilimia 34 n a mafanikio haya ya takribani asilimia kumi yanatofautiana sana kwamba miaka kama kumi iliyopita kwa maana kuanzia 2090 hivi hali ya udumavu ilikuwa imekaa katika *level* moja kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo tumepata mafanikio makubwa sana ndani ya muda mfupi.

Sambamba na hilo, niseme tu kwamba katiak nchi ambayo tunazalisha chakula kwa wingi na hali hii ya udumavu tumeiona katika mikoa ambayo inazalisha chakula kwa wingi, maana yake ni kwamba bado Watanzania tunakula bora chakula kuliko chakula kilicho bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini sisi kama Seriakli tumefanya? Kwanza tumeweka mkakati wa kuzalisha mazao lishe, tuan viazi lishe, tuna nafaka mbalimbali ambazo sasa hivi tunazalisha zenye lishe. Lakini sambamba na hilo, tumeweka utaratibu wa kuweka virutubishi katika baadhi ya nafaka ikiwa ni pamoja na unga wa mahindi pamoja na unga wa ngano.

Vilevile tumehakikisha kwamba tunaboresha mifumo ya lishe nchini kwa kuajiri Maafisa Lishe katika ngazi mbalimbali za mikoa na wilaya. Lakini sambamba na hio, hivi karibuni sisi kama Wilaya tumevida marufuku televisheni zote ambazo ziko ndani ya vituo vyetu nya kutolea huduma za afya kuonesha tamthilia, mpira wala muziki na badala yake sasa hivi zitakuwa na ujumbe mahsus kuhusiana na masuala ya afya ili wagonjwa wanapokuja pale hopsitali wapate elimu mbalimbali kuhusiana na changamoto ambazo ziko katika sekta ya afya na jinsi gani ya kujikinga ikiwa ni pamoja na masuala ya lishe kwa akina mama ambao wanakuja kliniki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo, swali fupi la nyongeza.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri na wote tunakiri kwamba uzazi wa mpango ni jambo la msingi sana katika kupunguza vifo nya akinamama, lakini hivi karibuni na sio mara ya kwanza Mheshimiwa Rais amekuwa akitoa matamko ya kuhamasisha akinamama wazae. Kule Dar es Salaam alisema "wafyature" lakini kule Meatu mwezi wa tisa amezungumzia hivyo hivyo na Serikali kupitia Wizara hii imetoe barua kusema kwamba Chama cha Uzazi waache kuhamasisha masuala ya uzazi wa mpango.

Nataka kupata ufanuzi kutoka Serikalini kwa sababu Rais akisema jambo ni kama sheria. Je, tunafuata kauli ya Rais au tunafuata uzazi wa mpango kama ambavyo tuko kwenye Mpango wa Maendeleo? Ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri hilo swali jepesi sana tena jibu kwa ufupi wala halina mkanganyiko.

**MBUNGE FULANI:** Tunazaa!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali hatujaweka ukomo wa idadi ya watoto mwananchi anatakiwa kuzaa, naomba hilo lieleweke. Serikali haijaweka ukomo wa idadi ya watoto mwananchi anatakiwa kuzaa, tunachosisitiza sisi kama Serikali ni kuhakikisha kwamba kila mtu awe na idadi ya watoto ambao anaweza kuwamudu kuwatunza na hilo ndilo msisitizo wetu. Kwa hiyo, sisi kama Serikali hatujatoa tamko la kusitisha huduma ya uzazi wa mpango. Hioo barua haipo na wala haitakuwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niweke tu vizuri kwamba *context* ambayo Mheshimiwa Rais alikuwa anaiongelea ni hii ambayo kuhakikisha kwamba mtu anakuwa na idadi ya watoto ambao anaweza kuwazaa na kuwatunza, lakini sambamba na hilo kuhakikisha kwamba afya na ustawi wa mama na mtoto unakuwa ni kipaumbele.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, hilo swalii ni zuri na jepesi kama nilivyo sema na mimi nakubaliana kwamba hata Mwenyezi Mungu katika dini zetu amesema tuje duniani tuongezeke, tuzaane lakini tujiongeze. Kwa hiyo, Serikali iko sahihi na Mheshimiwa Rais yuko sahihi.

Tunaendelea na Mheshimiwa Azza Hillal Hamad Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 26

**Kufungua Dirisha la Benki ya Wanawake Tanzania  
Mkoa wa Shinyanga**

**MHE. AZZA H. HAMAD** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaweka dirisha la Benki ya Wanawake katika Mkoa wa Shinyanga ili wanawake wa Mkoa huu waweze kupata huduma ya mikopo ya benki hiyo kwa karibu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO, alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Shinyanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjulisha Mheshimiwa Azza Hillal Hamad Mbunge wa Viti Maalum na Bunge lako tukufu kuwa Benki ya Wanawake Tanzania iliunganishwa na Benki ya Posta Tanzania mnamo tarehe 3 Agosti, 2018 kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuboresha ufanisi na utendaji wa benki hizo ili ziweze kuwashudumia wanawake na wananchi wengine kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Benki ya Posta Tanzania imeanzisha dirisha maalum kwa ajili ya kushughulikia huduma za kibenki kwa wanawake kwa maana ya *Women's Banking Window* ambalo liko chini ya Idara ya Uendeshaji na Mawasiliano ya benki hiyo. Vilevile Benki ya Posta Tanzania imeanzisha tawi la huduma kwa wanawake (*Tanzania TPB Women Branch*) katika ofisi zilizokuwa Benki ya Wanawake Tanzania Mtaa wa Mkwepu, Dar es Salaam na linaendelea kutoa huduma za kibenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Posta Tanzania kwa kushirikiana na Wizara yetu inaangalia namna bora ya kuendeleza huduma na bidhaa zilizokuwa zinatolewa na Benki ya Wanawake Tanzania. Mchakato huu unatarajia kukamilika mwezi Desemba mwaka huu. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa ifikapo Januari, 2019 dirisha la wanawake linafunguliwa katika matawi yote ya Benki ya Posta Tanzania ikiwemo tawi la Shinyanga na Kahama.

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Azza swali la nyongeza.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa dhumuni la kuanzisha Benki ya Wanawake ilikuwa ni kuwasaidia wanawake kupata mikopo yenye riba nafuu, naomba kumuuliza Naibu Waziri maswali ya nyongeza, je, Benki ya Posta haioni ni vyema sasa wakaendeleza lengo lile lililokuwa limekusudiwa kwa kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake ili mikopo hiyo iweze kutolewa kwa riba nafuu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni nini hatma ya wanawake waliokuwa na hisa katika Benki ya Wanawake? Nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza alitaka kujua, je kutakuwa na muendelezo wa mikopo ya riba nafuu baada a benki hizi mbili kuunganishwa. Jibu ni ndiyo na ndiyo maana wakati Serikali imefanya azimio la kuunganisha benki hii, moja ya sharti ilikuwa ni kwamba dirisha la mikopo kwa ajili ya wanawake liendelee ndani ya benki hii. Niendelee kusisitiza kwamba sharti hili la Serikali litazingatiwa na linaendelea kuzingatiwa baada ya hizi benki mbili kuunganishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ilikuwa je, zile hisa ambazo zilikuwepo katika benki hizi zitakuwaje. Niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hisa zote ambazo zilikuwepo kwa wale wote ambao walichangia na kununua hisa katika benki hii haki zao zitalindwa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Mwisho tunamalizia Wizara ya Madini, Mheshimiwa Susanne Peter Maselle, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 27

**Mgogoro Kati ya Wachimbaji Wadogo wa Madini na  
Mwekezaji – Mwanza**

**MHE. SUSANNE P. MASELLE** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na mgogoro kati ya wachimbaji wadogo wa madini wa Ishokelahela na mwekezaji anayebebwa na mamlaka ya Kiserikali Mkoa wa Mwanza na Misungwi.

Je, Serikali imeshindwa kutatua mgogoro huo na kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata haki zao?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H.  
NYONGO) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susanne Peter Maselle, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro katika eneo la Ishokelahela ulitokana na wachimbaji wadogo kuvamia na kuchimba katika leseni kubwa leseni kubwa ya utafiti ambayo ilikuwa inamilikiwa na *IAMGOLD Tanzania Ltd.* yenye namba PL 1568/2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014 ili kumaliza mgogoro huo Serikali ilijadiliana na mmiliki na kumtaka kutoa leseni yake ili kuwasaidia wachimbaji wadogo waliopo eneo hilo ili waweze kurasimishwa kwa kuwapatia leseni. Mmiliki huyo alikubali kutoa sehemu ya eneo la leseni yake kwa kutoa kiasi cha hekta 20 kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 4 Julai, 2014 kikundi kilichojulikana kwa jina la *Isinka Federation* cha mwaka 2014 *Co-operative Ltd. Tanzania* kiliomba leseni mbili za uchimbaji mdogo (PL 001268LZ na PML 001269LZ) na kupatiwa leseni hizo,

hivyo kumaliza mgogoro huo katika eneo hilo. Aidha, Oktoba 2015 leseni hizo waliamua kuziunganisha (*amalgamation*) na kutengeneza leseni moja ya uchimbaji wa kat i (ML 555/2015).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susanne Maselle swali la nyongeza.

**MHE. SUSANNE P. MASELLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza maswali 12 juu ya mgogoro huu lakini cha kusikitisha Serikali imekuwa ikija na majibu tofauti juu ya maswali haya. Nataka Serikali ituambie je, inaficha nini au inafaidika na nini katika huu mgogoro ambaao unakandamiza wananchi wa Wilaya ya Misungwi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali ilikiri hapa kwamba leseni ya huyu mwekezaji imeisha tangu tarehe 4 Agosti, sasa Serikali imejipangaje kumaliza kabisa huu mgogoro badala ya kuja na majibu ambayo yanachanganya kila wakati katika Bunge hili? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi ya maswali hayo ua nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimuombe Mbunge kwa sababu amekuwa anauliza mara kwa mara kuhusu mgogoro katika eneo hili. Mgogoro wa eneo hili umeshakwisha kwa sababu wachimbaji wadogo walikuwa wanavamia eneo la utafiti la mwekezaji wa *Carton Ltd.* baada ya kuomba yule mwekezaji aachie eneo, mwekezaji akaachia eneo na kuna makundi mawili yakajitokeza, kuna kundi la Buhunda na kuna kundi la Basembii, makundi yale mawili tukayapa maeneo wakaanza kuchimba na mpaka

sasa hivi wameamua kuunganisha yale maeneo, wameamua kufanya *amalgamation*, wamepata ML ambayo ni namba 555 ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida mtu anapopata *mining license* inadumu kwa miaka kumi na hawa wachimbaji wadogo baada ya kuunganisha hizo leseni wameungana na mchimbaji wa kati sasa hivi wameshanunua mitambo ya kuweza ku-*process* ile ore ambayo wanaichimba na wamekwishachimba kiasi cha tani 227,000 wameshazirundika na sasa hivi mitambo inatoka China na wakato wowote mwezi ujao wanaanza ku-*process*. Huo mgogoro haupo! Kama kuna mgogoro naomba nikutane na Mbunge anieleze ni nani anayelalamika tuweze kutatua mgogoro huo. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Swali letu la mwisho...

Mheshimiwa Waziri majibu ya nyongeza.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuongezea majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza kama ambavyo Naibu Waziri ameeleza hatuna ambacho tunakificha na amekuwa mara kwa mara akiuliza masuala haya na tumekuwa tukimuambia hata kumkaribisha tuko tayari kwenda pamoja na yeye kujiridhisha kama kweli mgogoro huu umeisha. Tupende kumthibitishia kama ambavyo Naibu Waziri amesema, mgogoro huu umeisha na hata Serikali ya Kijiji cha Buhunda ilishiriki, Mwanasheria wa Halmashauri ameshiriki na uongozi mzima wa hapo. Kwa hiyo nipende tu kusema kwamba mgogoro huo umeisha lakini kama ana mambo mengine basi alete *fact* mezani ili tuweze kuona nini hasa ni tatizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya nyongeza. Tunamaliza swali letu la mwisho kwa siku ya leo kuititia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 28

## **Kutosikika kwa TBC Katika Baadhi ya Maeneo ya Pwani**

**MHE. ZAYNAB M. VULLU** aliuliza:-

Je, ni changamoto zipi zinazopelekea *TBC* kutoshika katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO,** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu Mbunge wa Viti Maalum kamaifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC* inayo mitambo ya kurushia matangazo ya redio ya masafa ya *FM* katika Wilaya ya Kisarawe Mkoani Pwani; mitambo hii hufikisha matangazo ya redio kwa wananchi kwa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani katika masafa ya 87.8 MHz kwa idhaa ya *TBC* Taifa, 90.0 MHz kwa idhaa ya *TBC FM* na 95.3 MHz kwa idhaa ya *TBC International* inayotangaza vipindi vyake kwa lugha ya kiingereza. Pamoja na uwepo wa mitambo hiyo, tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa usikivu wa *TBC* katika baadhi ya maeneo ni hafifu na ni azma ya Serikali kupanua usikivu wa *TBC* nchi nzima. Katika bajeti ya mwaka jana, mwaka 2016/2017 kwa mfano; *TBC* ilitekeleza mradi wa upanuzi wa usikivu katika wilaya tano zilizopo mipakani mwa nchi; yaani Longido Mkoani Arusha, Rombo, Kilimanjaro, Tarime, Mara, Nyasa, Ruvuma na Wilaya ya Kibondo Mkoani Kigoma. Aidha, bajeti iliyofuatia ya 2017/2018 *TBC* ilitekeleza mradi wa upanuzi wa usikivu katika Mkoa wa Mtwara na wilaya ya Lushoto Mkoani Tanga. Kufikia Juni 2018, *TBC* ilikuwa na vituo 33 vya kurushia matangazo katika masafa ya *FM* kwenye Wilaya 102 kati ya Wilaya 161 nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC* inaendelea na mpango wa kupanua usikivu nchi nzima kutegemea na upatikanaji wa fedha ili kuyafikia maeneo yote yaliyobaki. Katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2018/2019 *TBC* inatarajia kupanua

usikivu katika maeneo ya Unguja na Pemba, Mikoa mipy ya Simiyu, Njombe na Songwe, Mkoa wa Lindi maeneo ya Nangurukuru na Mkoa wa Morogoro maeneo ya Morogoro Vijijiini, Bondwa na Mahenge. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vullu kama una swalii la nyongeza.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ya kuonesha juhudhi za *TBC* ambacho ni chombo cha Taifa cha redio na televisheni kutaka kuwafikia wananchi maeneo mbalimbali na pamoja na kwamba amezungumzia habari ya minara kuwepo Wilaya ya Kisarawe ambayo ni sehemu ya Mkoa wa Pwani, lakini bado tatizo la usikivu katika maeneo ya Mkoa wa Pwani na yeye amekiri kuwa yapo hajaelezea ni lini atatatua maeneo hayo. Kwa mfano, baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani ni visiwa, Kisiwa cha Mafia hawasikii kabisa redio na televisheni ya Taifa.

Je, ni lini Serikali itahakikisha *TBC* inajиidesha bila kutegemea bajeti ya Serikali na kuweza kufikia lengo la kuwafikia wananchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; kwa kuwa *TBC* ni chombo cha kuwezesha wananchi kupata habari na taarifa mbalimbali tumeona na tumeshuhudia matangazo mubashara na mengine yanayofanywa na *TBC* hii inamaanisha kwamba Serikali inategemea *TBC*, lakini na Serikali imeshahamia Dodoma ambako ndiyo Makao Makuu, Serikali inaendesha shughuli zake hapa.

Ningependa kujua ni lini Serikali itahamisha *TBC* ihamie hapa na kuboresha miundombinu ya kuwezesha redio na *tv* katika kituo cha Dodoma kufanya kazi kwa ufanisi na kwa urahisi? Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishamueleza Mheshimiwa Mbunge hili ni suala endelevu la ujenzi upanuzi wa usikivu wa *TBC*. Kama nilivyosema, sasa hivi tuna vituo vya kurushia matangazo 33. Mwaka 2010 tulikuwa navyo 12 nchi nzima na tunaendelea kuhakikisha kwamba maeneo 59 yaliyobaki tutahakikisha tunayatafutia pia mitambo ya kurushia matangazo na hiyo itahusisha vilevile Mkao mzima wa Pwani. Sasa hivi tunashambulia Unguja na Pemba na kwa jiografia iliyopo pale hata vilevile kuweka mitambo Unguja na Pemba kutapeleka sehemu nyngi za Mkao wa Pwani kupata matangazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nikuhakikishie kwamba tuna mpango mahsus wa kujenga studio mpya Dodoma na tumeshaanza. Vilevile tulikuwa na mtambo hapa wa kurushia matangazo wa *medium wave* ambao umechoka, tutauondoa na kama nilivyosema wakati fulani hapa hapa Bungeni Bunge liliopita kwamba tunanunua mtambo mpya wa *kilowatt 70* hapa Dodoma pamoja na Mbeya ili kuongeza usikivu wa redio kutoka Makao Makuu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo na Waheshimiwa Wabunge muda wetu wa maswali umekwisha na umepitiliza kwa kweli kwa raha ya maswali. Sasa ni wakati wa matangazo, tutaanza na wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Kwanza waeni waliopo jukwaa la Mheshimiwa Spika, tuna wageni wanenye wa Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Tulla Ackson (Mbunge) ambao ni Mwenyekiti wa Idara ya Vyuo Vikuu na Mjumbe wa Baraza Kuu - UVCCM Taifa Ndugu Maranatha Baraka, karibu sana Mwenyekiti. (*Makofi*)

Tuna Mchungaji wa Kanisa la *FPCT Katubuka* la Kigoma Ndugu Japhet Nicholas, karibu sana. (*Makofi*)

Lakini pia tuna Mchungaji Msaidizi Kanisa hilo la *FPCT Katubuka*, Kigoma Ndugu Benjamin Buromela, karibu sana

na pia tuna Muinjilisti Kanisa la *FPC* Katubuka Kigoma, Ndugu Abel Mlala, karibuni sana wageni wetu kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika. (*Makof!*)

Wageni wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kuna wageni 17 wa Mheshimiwa Justin Joseph Monko ambao ni walimu na wanafunzi kutoka Shule ya Msingi Kinyamwenda, Mkoani Singida wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Shule Ndugu Hamisi Ngura na Msaidizi wa Mbunge, Ndugu Richard Kwidha. Shule ya Msingi Nyamwenda iliyopo Kata ya Itaja, Wilaya ya Singida, imeshika nafasi ya kwanza kiwilaya kati ya shule 93 na nafasi ya nne kimkoa. Wanafunzi wote 26 waliofanya mtihani walifaulu, 14 kwa daraja A na 12 kwa daraja B. Hongereni sana na karibuni sana katika Bunge letu. (*Makof!*)

Mbona siwaoni wamesimama, wako wapi? Hawajafika? Haya, tuwapongeze hivyo hivyo.

Wageni 52 wa Mheshimiwa Salum Khamis Salum ambao ni viongozi wa CCM kutoka Jimbo la Meatu. Karibuni sana katika Bunge letu. (*Makof!*)

Na wageni saba wa Mheshimiwa Mariam Mzuzuri, Mbunge, ambao ni wajasiriamali kutoka Mkoani Dodoma wakiongozwa na Ndugu Jamal Adam. Karibuni sana katika Bunge letu. (*Makof!*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Joseph Mhagama, Mbunge, ambao ni viongozi kutoka Kijiji cha Lutukila, Madaba, Mkoani Ruvuma wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kijiji cha Lutukila, Ndugu Christian C. Mapunda. Karibuni sana wageni wetu. (*Makof!*)

Wageni wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni viongozi wa CCM kutoka Mkoani Iringa. Katibu wa Vijana CCM, Ndugu James Mgego na Katibu wa Tawi CCM Kilolo, Ndugu Mohamed Wanda. Karibuni sana viongozi wetu. (*Makof!*)

Wageni wengine ni wageni 16 wa Mheshimiwa John Heche, ambao ni Kikundi cha *VICOBA* kutoka Tarime Mkoani Mara, wakiongozwa na Ndugu Gema John na *NGOs* ya Haki Rasilimali kutoka Jijini Dar es Salaam, wakiongozwana Ndugu Rachel Chagonja. Karibuni sana latika Bunge letu wajasiriamali wetu. (*Makofi*)

Wageni wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Omary Mgumba, Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni watoto wake kutoka Jiji la Dodoma, Ndugu Adam Omary Mgumba na Ndugu Otham Omary Mgumba. Karibuni sana ndugu zetu. (*Makofi*)

Wageni watatu wengine wa Mheshimiwa Seif Gulamali, Mbunge, ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Manonga, Mkoani Tabora, Mwallimu Joseph Ngomuo, Ndugu Sabi Mohamed na Ndugu Dotto Joseph. Karibuni sana katika Bunge letu. (*Makofi*)

Na wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 107 na walimu 7 kutoka shule ya *Ihsan Islamic Secondary* ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wanafunzi wetu wa kike kwa wakiume katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Matangazo mengine ni kikao cha Kamati ya Bunge ya Bajeti, Wajumbe wanatangaziwa kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati ya Bajeti leo tarehe 7 Novemba, 2018 kwa ajili ya kupitia na kujadili Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo ya Fedha (*The Microfinance Bill, 2018*). Kikao kitafanyika katika Ukumbi wa Msekwa B kuanzia saa 7:00 mchana, hivyo wajumbe wote mnaombwa kuhudhuria.

Tangazo lingine ni Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kwamba, leo Jumatano tarehe 7 Novemba, 2018 saa 07:00 mchana mara baada ya kusitishwa shughuli za Bunge kutakuwa na Uzinduzi wa Mkakati wa Bunge wa Masuala ya Jinsia katika Ukumbi wa Msekwa. Mgeni rasmi

katika shughuli hiyo atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kushiriki bila kukosa.

Tangazo la mwisho ni wachezaji wote wa *Bunge Sports Club* ambao watakwenda kwenye Mashindano ya Mabunge ya Afrika Mashariki wanatakiwa leo waende dispensaryya Bunge kwa ajili ya chanjo ya kwanza ya *Hepatitis B* na chanjo ya pili watapata tarehe 28/11/2018. Sababu ya kupata chanjo ya kwanza ya B ni kuwa baada ya mwezi mmoja ambapo wanapaswa kupata chanjo ya pili watakuwa Burundi. Karibuni sana. Hayo ndio matangazo yetu kwa leo. Katibu tuendelee.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Mipango.

**MWENYEKITI:** Kamati ya Mipango.

#### **KAMATI YA MIPANGO**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mtuvumilie, muda wetu wa maswali umechukuliwa na miongozo kwa hiyo, miongozo kwa leo hakuna.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, cha muhimu hiki.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na wewe umekuwa mhuni siku hizi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### KAMATI YA MIPANGO

**Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa  
Kutekelezwa na Serikali pamoja na Muongozo wa  
Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa  
Fedha 2019/2020**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Mipango, tunaendelea na mjadala. Tutaanza na Mheshimiwa Mbilinyi na baadae Mheshimiwa John Heche ajiandae.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Katika kujadili mpango naomba kwanza Dkt. Mpango aniambie toka Awamu ya Tano imeingia kuna *FDIs* ngapi zimeshakuja nchini, naomba anipe takwimu, *FDIs* ni *Foreign Direct Investments*. Naomba kujua ni ngapi toka Awamu ya Tano iingie madarakani, zimeshakuja nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda nijue toka Awamu ya Tano kwenye *Arbitration Courts*, kwenye Mahakama za nje kuna migogoro na kesi ngapi dhidi yetu? Maana tunasikia tu ACACIA wameenda Mahakamani, mara *Pan African Energy* wako Mahakamani kutudai kwa hiyo, tunaomba tujue pamoja na gharama ya fedha ambazo wanataka tuwalipe kupitia hizo mahakama? *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu katika haya mambo *no one is perfect*. Na sisi kazi yetu kushauri humu ndani na ninyi huko mnatakiwa Mawaziri mnatakiwa mumshauri Rais msimuogope, tunarudia kusema hiki kitu. Na ndio maana kwa sababu, hakuna mtu *perfect, even the President can not be perfect every time* na ndio maana pamoja na mbwembwe zote tukasubiri Baraza la Mawaziri kachukua *time* sana kutangaza Baraza la Mawaziri, lakini

mpaka leo bado ameshatumbua Mawaziri 11. Kwa hiyo, kama angekuwa *perfect* wale aliochelewa kuwateuwa ina maana wangkuwa sawasawa na angeenda nao mpaka leo, lakini mpaka sasa hivi 11 wameshatumbuliwa, hii inamaanisha kwamba *no one is perfect* na muendelee kumshauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana nimuunge mkono *my friend*, Mheshimiwa Lusinde katika Bunge liliopita 2010/2015 alikuwa na hoja yake anapenda sana kuisema Bungeni kwamba, viongozi tupimwe afya ya akili. Hili alilisema sana Mheshimiwa Lusinde wakati ule sikumuelewa, lakini kwa *trend* ya mambo yanavyokwenda sasa hivi katika hii nchi kwa kweli, naomba ni ... halafu nimuunge mkono Mheshimiwa Lusinde ile hoja yake kwamba kuanzia sasa viongozi wote kuanzia chini Serikali ya Mtaa, Diwani, Mbunge, Rais, hakuna kuchaguliwa kama hajaenda kupimwa afya ya akili kwa sababu mambo yanavyokwenda sio sawasawa kabisa, angalia wanachofanya ma-*DC*... (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...angalia wanachofanya ma-*RC*, eeh, ma-*RC*. Watu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi naomba usubiri. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumze Kuhusu Utaratibu.

Kwanza ni Kanuni ya 68(1) lakini Kanuni ya 64 na Kanuni ya 64 nitakwenda kwenye Kanuni (e). Kanuni (e) inatukataza sisi wote tunapozungumza ama kuchangia Bungeni kuzungumzia mwenendo wa Rais katika kufanya...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,  
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** ...katika utendaji  
wa kazi wowote ndani ya Serikali. Kwa hiyo, kwanza hilo tu  
naomba niliweke sawa, hata kama ana *interest* ya  
kuzungumzia viongozi, lakini ninaomba kwenye eneo  
hiliasiendelee kumjumuisha Rais katika utendaji wa kazi katika  
nchi na ndani ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo lingine ambalo  
naomba kulizungumza la utaratibu; hatasema vibaya na  
kutumia lugha ambayo ni ya kuudhi na inayodhalilisha watu  
wengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, anapotaka kum-*quote*  
Mheshimiwa Lusinde kwa michango aliyotoa kwenye Bunge  
lililopita utaratibu wa kikanuni, Bunge lililopita linakufa na  
mambo yake yote.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,  
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** ...huo ndio  
utaratibu wa kikanuni ambao tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kutumia kauli ya  
Mheshimiwa Lusinde kwa Bunge lile alichokisema na  
alichomaanisha pale hawezi kuchukua jambo hilohilo  
akawajumuisha viongozi wote kwa sababu hapa hayuko  
*specific*. Viongozi wote kuanzia ngazi za vijiji mpaka Taifa  
wapimwe akili, hiyo ni lugha ya kutudhalilisha na ni lugha ya  
kuudhi, haiwezi kukubalika. Na kama ana hoja mahususi  
ajikite kwenye hoja mahususi, kwa jambo mahususi, kwa mtu  
mahususi, lakini huo sio utaratibu wa kikanuni na ninaomba  
*seriously* niseme haoa tunavunja utaratibu wa kikanuni.

**MWENYEKITI:** Umefahamika Mheshimiwa Jenista, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Sasa yeote atakayekiuka kanuni, kama tunataka kwenda kwenye uzuri wake wa mjadala tuone raha, yeote asizungumze lugha yoyote ya kuudhi inayoenda kinyume na utaratibu, ambaye ataendelea hataweza kuruhusiwa kuendelea na mjadala.

Tunaomba uendelee Mheshimiwa Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, kanuni haiwezi...

**MWENYEKITI:** Endelea na mchango wako usimwambie Mheshimiwa Waziri.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...aaahh.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa lazima ijibiwe.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Kanuni haiwezi kuzidi Katiba. Mambo mengine ni matakwa ya kikatiba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu sikum-*cite* mtu, *individual*, nimezungumzia mfumo wa uteuzi. Ndio kitu nilichozungumzia hapa, mfumo wa uteuzi kwamba, tunavyoteuwa kuanzia Diwani, Mbunge kwenda juu, pengine hata Mwenyekiti wa Kiti na Spika nao inabidi wapite katika huo mchakato, lakini ninyi kwa sababu mtakuwa mmeshachekiwa kama Wabunge kwa hiyo, mtakuwa *safe* kukaa kwenye hicho kiti kwa hiyo, *it is not personal*.

**MWENYEKITI:** Sasa hiyo sio lugha maana humu ndani kuna watu wengine ambao hawana? Mkiwemo na niny upande huo au mtakubalana na mie? (*Kicheko*)

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Yeye ana *plate number* kifuani ya jela.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tuendelee na mjadala, hayo sio maneno hayo ya kuzungumza.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natumaini unanitunzia dakika zangu ili nifanye kazi yangu ya Kibunge kwa sababu hii nchi tunafika hapa, tunafunganafungana hovyo, tunapiganapigana risasi hovyo kwa sababu ya unafiki, watu hawataki kusema ukweli. Angalia walichokifanya wale Maprofesa wa Chuo Kikuu juzi pale Mlimani, *Nkrumah Hall* ni sehemu ya tafakuri ya Taifa. Hayati Mwalimu Nyerere alikuwa anaenda pale kukutana na wasomi ku-*discuss* mustakabali wa nchi, leo hii maprofesa watu wazima kabisa wanamuita pale kiongozi wanaanza kumsifia, sio vibaya kusifia, lakini wange-*balance* wamwambie na mapungufu yake kwa maslahi ya nchi hii, hicho ndio tulichotakiwa kufanya, hakuna anayemwambia ukweli kiongozi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa nje watu wanalia, na mimi najua, Mheshimiwa Msigwa anajua, Mhesimiwa Jesca anajua, Mheshimiwa Mhagama unajua, AG unajua, Waziri Mkuu unajua, nje watu wanalia *we are not happy, the nation is in sombre ... the nation is not happy*. Tuambiane ukweli, ili tusonge mbele. Unaona sisi mnatufunga tunatoka tunatabasamu ni kwa sababu ya Taifa hili. Kwa sababu ya mslahi ya Taifa hili na si vinginevyo, lakini tungetoka tumenuna tungezidi...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi Taarifa iko huko nyuma yako. Mheshimiwa Bwege.

## TAARIFA

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa Taarifa Msemaji, usiogope lolote kusema katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni haki yako, sema. (*Makof/Kicheko*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi endelea, lakini uwe na tahadhari, sio kila kitu unasema tu popote.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea Taarifa ya Mheshimiwa Bwege.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lina uwoga ndugu zangu, Taifa lina woga, sasa hatuwezi kujadili maendeleo kwenye uwoga. Jana...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi subiri Taarifa hiyo ya mwisho.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *I hope you are keeping my minutes though.*

## T A A R I F A

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Taarifa msemaji, wanaolalamika wote ni mafisadi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi, pokea taarifa hiyo.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu naye ndio anasababisha hoja yangu kwamba *nobody is perfect* kwamba hata wale waliochaguliwa kwa mbwembwe wametumbuliwa, huyu ni mmoja wa waliotumbuliwa katika wale 11, unaona. Huyu ni mmoja wa waliotumbuliwa katika wale 11. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *we are serious here*. Hapa ndugu zangu tuko *serious, we love this country*. Sisi wengine mnavyotuona tumetokea mtaani mpaka hapa

tulipofika tunaona Mheshimiwa Kikwete alipotufikisha na mapungufu yake yote alipotufikisha, lakini *at least* tulikuwa tunaona mwanga, sasa mnatuingizaje kwenye giza na mmekaa tu hapa jamani mnasema tujadili mipango? Tunajadilije mipango polisi wanauwa watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, polisi wanatuhumiwa kuuwa watu kila kona. Tukisema kwamba uchunguzi ufanyike mnatukamata badala ya kutuomba ushirikiano tuwape *information*. Jijini Mbeya kwangu mimi, watoto wawili, vijana wawili wamekufa mikononi mwa polisi, Allen Mapunda wa Kata ya Ihyela amekufa mikononi mwa polisi, Kijana Kapange mpaka leo maiti yake iko *mortuary* kwa zaidi ya siku 160 kwa sababu familia imegoma inasema tunataka uchunguzi huru, sio polisi wajichunguze, tunataka uchunguzi huru. Mpaka leo maiti ya kijana siku 160 iko imelala *mortuary*, hili Taifa gani? Halafu mnasema kwamba watu wanafuraha katika Taifa kama hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawana furaha ndugu zangu. Polisi wanatuhumiwa kuuwa watu *with impunity*, hakuna mtu anayeingia, hakuna tunachofanya, angalia afya, nilikuwa namuuguza mama pale Hospitali ya Taifa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Kangi, hebu kaa bwana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri jamani, naomba...

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si kuna muda wa Mawaziri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi, muda wako unatunzwa, Mheshimiwa Waziri toa taarifa yako.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba utulie muda wako unatunzwa, tumsikilize Mheshimiwa Waziri mhusika mara moja. Mheshimiwa Waziri?

### **KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashangaa hawa amba wanaanza kutukana polisi wakati polisi wangu wako humu ndani. (*Makofii*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu. Sina haja ya kupoteza muda kunukuu kwa sababu, Kanuni zetu za Kuhusu Utaratibu zinafahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mchangiaji badala ya kujikita kuliambia Bunge lako tukufu kwamba polisi wanauwa watu, jambo hili ni zito sana. Tukimtaka Mheshimiwa Mbunge leo aniletee taarifa ya polisi ambao wameuwa watu katika nchi hii ailete kwako, lakini pamoja na hayo polisi wangu hawahawa na wao wamekuwa wakiuwawa, mbona Wabunge hawa hawawazungumzii polisi wanaouwawa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wasitumie Ibara ya 100 ya uhuru wa kuzungumza kuwapaka matope askari wetu wa Jeshi la Polisi wanaofanya kazi nzuri katika Taifa letu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wabunge wasitumie Bunge lako tukufu kama kichaka cha kuchochea, kutoa kauli za uchochezi juu ya Jeshi la Polisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ameeleweka, Mheshimiwa Mbilinyi naomba uendelee, jamani naomba tujikite kwenye hoja.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kangi *is my friend, my brother*. Yeye mwenyewe ni mhanga wa sintofahamu za Awamu ya Tano, alipigwa kesi ya rushwa sijui iliishia wapi? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipigwa kesi, hawa ndio walikuwa ni wahanga wa mwanzo kabisa wa vurugu *match*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi unapoteza muda wako au hujasoma mpango?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Alipigwa kesi ya rushwa sijui imeishia wapi, kwa hiyo Waheshimiwa... (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi naomba utoe maoni yako kwenye mpango.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Hapa tunaongea masuala ya afya, tunaongea masuala ya mpango wa nchi, lakini mambo hayaendi, kwenye afya tumekazana kujenga majengo, wataalam hatuna, nilikuwa pale Muhimbili, mama anahitaji huduma moja inaitwa *vascular surgery* naambiba daktari yuko mmoja tu halafu hayupo ameenda Hijja. Hijja ni kitu kizuri huwezi kumzuia yeye kwenda Hijja, lakini jukumu lenu ni ninyi kuhakikisha kuwa kuna watalaaam wa kutosha kwa sababu hilo hitaji ni kaja kugundua ni wagonjwa wengi sana wako *lined up* na wanapoteza maisha na vile na kila kitu kwa sababu ya kukosa wataalam.

Sasa wewe mtaalam wa *vascular surgery* Taifa kama hilli yuko mmoja, halafu mnasema tunaenda vizuri afya, tunaenda nini tunafanya vipi mnakazana kusema kwamba bajeti ya dawa imeongezeka iko bilioni mbili.

Mimi nitasikia raha mkiniambia bajeti ya dawa imepungua na hiyo bilioni 200, 300 pelekeni kwenye maji na vyanzo vingine sehemu nyingine ambazo ni chanzo cha magonjwa ili bajeti ya dawa ipungue na sio kuongeza bajeti ya dawa halafu kudhani kama ni sifa. Mnasema sasa hivi ni bilioni 200 mwakani mtasema bilioni 400, mwaka unaofuata mtasema bilioni 600 kwenye madawa sio sifa, sifa ni kupunguza bajeti ya madawa maana yake kwamba Taifa lina afya watu hawaugui na si vinginevyo ndugu zangu. (*Makofii*)

*Kwa hiyo, hii nchi haina mipango ina events, ndio maana vijana huko chini hawapewi instrument za kazi zao wakiteuliwa hawa RC, DC wakiamka wanakurupuka tu kila mtu huyu ana hili, leo mtu anakuja sijui madawa ya kulevyia, sijui wameshafungwa wangapi madawa ya kulevyia kwa yule bwana wa Dar es Salaam (Bashite), mara sijui watoto waliotelekezwa, mara sijui imeishia wapi, mara sijui nitatoa bima za afya, mara juzi amekuja na hiyo sijui ya mashoga, wakati yeye mwenywewe katajwa na hajaenda kupima, wakati*

**kiongozi. (Makofi/Kicheko) [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi unatakiwa kuishi kwa mfano, wewe umetajwa kabla watu hawajatajwa, leo hii wenzako wanatajwa mwaka mmoja, miaka miwili baadae halafu unaanza kuwa-*harass* na kuwafanya hivi wakati... (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi taratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wetu ndani ya Bunge, ukienda Kanuni ya 64(g) kwa kweli haturuhusiwi kabisa kusema lugha ambazo zinadhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini vilevile hii sio lugha ambayo inaweza kutumika pia ndani ya Bunge, nikuombe sana kwa kutumia utaratibu wa kikanuni, Mheshimiwa Mbunge jambo hilo aliondoe kwenye mjadala wetu leo, halileti hadhi ya Bunge hili kudhalilisha watu wengine kwa kiasi hiki na wakati watu hao hawapo ndani ya Bunge hili na kupata nafasi ya kujitetea. Kama ana hoja yake ya msingi akaipeleke mahali ambapo anaotaka kuadhalilisha watakuwa na haki pia ya kujitetea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa mujibu wa kanuni hizi kwa kweli jambo hili ningeomba Mheshimiwa Mbunge aliondoe lisiwe *part* ya mjadala wetu hapa ndani kwa sababu ni jambo ambalo linakiuka kanuni zetu na nisingependa kurudia hicho alichokisema wakati anamalizia, sitaki kuwa *part* ya mtu ambaye anaeleza jambo hilo kwa kukiuka pia kanuni ndani ya Bunge lako lakini yeye anajua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, umeeleweka.

Mheshimiwa Mbilinyi naomba ufute hiyo kauli kwa vile huyo uliyemtaja hayumo humu na hawezi kujitetea kweli, lakini pia kwa vile umerejea muda wako umekwisha.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Kwa sababu Waziri hajasema hicho ninachotakiwa kufuta sasa sielewi nifute nini, sasa labda mfute mchango wote kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kufanya kazi ya kibunge jamani ee!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi umemtaja mtu huyo mtu uliyemtaja naomba uondoe kauli hiyo.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Bashite ni nani?

**MWENYEKITI:** Ndo huyo huyo uliyemtaja, ondoa kauli yake.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Aaaaa.

**MWENYEKITI:** Ondo kauli yake. Kwa hiyo hayo maneno mimi kama hutaki kuyafuta kwa namna ambayo ilivyo basi haya mimi nayaondoa. Lakini kwa vile umerudia tena kukiuka utaratibu muda wako umemalizika.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Aaaaa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Yaani hata ninyi hamtetei?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche! Mheshimiwa Heche! Karibu. (*Makofi*)

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1966 Chinua Achebe aliandika kitabu cha *A Man of the People* na kwenye kile kitabu kuna *character* mmoja anaitwa *Chief Nanga*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Chief Nanga* alikuwa mwalimu na baadae akawa Waziri. Na nikiangalia ile picha ambayo Chinua alikuwa anajaribu kui-portray kwenye uandishi wake na nikiiangalia Tanzania leo, namuona Chinua Achebe alikuwa anaandika kuhusu Tanzania. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mpango ameleta vitabu hapa, vingi sana anazungumza kuhusu mipango ya Taifa ya maendeleo ambayo kila mwaka tunajadili hapa. Kwenye mipango yake Waziri Mpango, mwalimu hajazungumza kuhusu kuongeza mishahara ya watumishi ambao ndio anategemea wampe ufanisi kwenye utendaji kazi wake. Hajazungumza kuhusu ajira mpya, huyu Waziri Mpango na Serikali yenu, mmekuwa leo ni *propaganda*. Watu wakitaka kuzungumza mnageuza lile jambo, lione kane ni jambo baya kwenye *society* na watu waonekane wanatumiwa na mataifa ya nje. Kuna kauli imekuwa maarufu sana, wanatumiwa kuhujumu uchumi na watu wasiopenda Taifa letu. Hawa watu hamuwataji lakini wapo mnawajua ninyi.

Sasa Waziri Mpango wewe unaishi maisha mazuri kama uzalendo ni kuwa masikini kuishi vibaya, kuendesha gari mbaya tuoneshe wewe mfano huo wa uzalendo, kwa nini wewe huutaki huo uzalendo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo uzalendo wa kutokukaa sehemu nzuri ambao mnataka muwaanimishe Watanzania kwamba uzalendo ni umasikini, kwa nini wewe huupendi huo uzalendo? Kwa nini unaendesha *V8* ya Serikali, mafuta ya Serikali, una wasaidizi, nyumba nzuri wote humu Bungeni. Hampendi uzalendo ninyi, mnataka uzalendo huo kwa watumishi wa umma tu. Watoto wa watu wamemaliza

shule. Mwaka 2015 Serikali yenu hii inayokusanya mapato kuliko Serikali zote zilizopita haijaajiri mwaka 2015, hamjaajiri mwaka 2016, hamjaajiri mwaka 2017, hamjaajiri mwaka 2018. Na mnakunakusanya kuliko wote.

Sasa tuje kwenye takwimu zenu, Serikali tukufu mnaokusanya kuliko wote, mwaka 2016/2017...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wana nafasi ya kutujibu, wata-*windup* tafadhali unamaliza muda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche, maneno mengine unayozungumza yanataka uthibitisho sasa unazungumza tu Serikali miaka minne haijaajiri, hayo maneno ni sahihi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MENYEKITI:** Mheshimiwa Heche endelea

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mwaka 2016/2017 Serikali hii inayokusanya kuliko zote ilitenga bajeti ya maendeleo shilingi triliuni 11.8 kwa mujibu wa kitabu cha Kamati. Pesa za maendeleo zilizokwenda ni shilingi triliuni 6.4 ambayo ni asilimia 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ni nini, maana yake ni kwamba asilimia 45 ya miradi yote ya maendeleo

iliyopangwa haitafanyika kwenye mwaka huo asilimia 45 ya miradi ya maendeleo. Ina maana shule asilimia 45 hazikujengwa, maji asilimia 45 hayakwenda kwa wananchi, barabara asilimia 45 hazikutengenezwa, miradi yote iliyoibuliwa kutoka kwa wananchi 45% haikutekelezwa, Serikali Tukufu inayokusanya kuliko zote ya akina Mpango. Mkikaa hapa mnaimba *Stiegler's Gorge, SGR, flyover* kana kwamba mwananchi wa kijijiini kwangu kule Nyamwaga au Nyanungu anajua *SGR* maana yake ni nini au mwananchi wa kijijiini kwetu kule Sirari anajua *flyover* ya Dar es Salaam inamsaidiaje. Leo mmekuja hapa unatuambia kwenye kitabu chako Mpango kwamba kilimo kimekuwa 7.2; sasa mimi nakuuliza Mpango, kilimo kilichokuwa kwa asilimia 7.2 mmenunua mahindi kiasi gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayokusanya kuliko zote mmeingia mmekuta gunia la mahindi shillingi 100,000, sasa hivi gunia la mahindi haliwezi kununua hata mfuko mmoja wa mbolea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ununue mfuko mmoja wa mbolea, unahitaji kuuza mahindi gunia tatu, Serikali inayopigania wanyonge, wanyonge mnaojiita ni ninyi mnaoendesha *V8*. Lakini mnyonge wan chi hii hakuna mnyonge hata mmoja mnaempigania, na mimi nilitegemea Mheshimiwa Mpango muingie hapa, msjisifu Serikali ya wanyonge tuambleni mlikuta wanyonge milioni ngapi, na kwa miaka mitatu mmepunguza wanyonge milioni ngapi, mnataka ku- *indoctrinate* watu mambo ya ajabu, mnataka kuwaaminisha watu kwamba eti umasikini ni sifa, wakati nyie wenyewe mnaogelea kwenye maisha mazuri. Mnakuja hapa mwaka uliofufata mmetenga bajeti ya maendeleo shillingi trilioni 12 na bila aibu kila mwaka mnaongeza *digit* na namba hazidanganyi. Mwaka huu mmetenga shillingi trilioni 12 mkatoa ile ile shillingi trilioni sita asilimia 57, sasa mimi najiuliza hizo pesa Mheshimiwa Mpango mnazotuambia mmekusanya kuliko wote mnalia au ziko wapi? (*Makofii/Kicheko*)

Kwa sababu kwa wananchi hazipo, kwenye ajira hamna, kwenye barabara hatuoni, kwenye Halmashauri leo

mnaondoa *Capital Development Grant* (*Local Government Capital Development Grant*) mmeiondoa kwa sababu kila siku inawaletea *query* hamjapeleka hata shilingi mia moja, Tarime mwaka 2016 hamkupeleka, mwaka 2017 hamkupeleka, mwaka 2018 hamkupeleka. Pesa zote tunazofanya maendeleo tumejenga vituo, tumejenga barabara, *own source* ya wananchi wa Tarime hakuna shilingi mia moja mlioleta Mpango, pesa hizo ziko wapi? Ziko wapi hizo pesa ambazo mnakusanya?

Haya mmekuja hapa wewe Mpango unaesema unakusanya sana na mkasema mnaweza kununua kama mnanunua ndege mtanunua korosho na wakulima jana, wanunuzi wa korosho jana wametoa *statement* kwamba hawatanunua tena korosho...

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** ...na mimi namtaka Waziri Mpango wakati anajumuisha hapa atuambie wanunua korosho za wakulima zote ambazo ziko kwenye maghala, kwa sababu hili jambo mliambiwa hapa wananchi walipanga kufikia mwezi wa tisa huu, mwezi wa kumi, mwezi wa 11 wao wameuza korosho zao wapeleke watoto wao shule. Wawe wameuza korosho zao wanunue walau bodaboda, wengine walipe kodi za nyumba, wengine wafanye nini, tunataka Waziri Mpango unapokuja hapa jibu la kwanza utuambie kwa sababu mlisema mtanunua korosho, utuambie mnaanza lini kununua korosho na kwa bei ya shilingi 3,000 kwenda juu hakuna kushuka hata shilingi 100. (*Makofî*)

Ninyi msifikiri Watanzania hawawaoni haki za binadamu zina *tolerate*, watu wameuawa Waziri pale anasimama anasema aseme Waziri, aseme polisi aliyeua mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mdogo wangu ameuawa kituo cha polisi halafu mnasimama hapa

mnasema eti polisi hawaui watu! Mheshimiwa Zitto juzi ametoa taarifa polisi wameua watu wengi hamjaita kuhoji, mmeita kumtishia na yuko hapa na Zitto mimi nataka uendelee kusema humu Watanzania wajue hatusemi uongo. Mnatishia watu wanaowashauri, mnawawinda wengine tunaishi kwa kuhamahama kwa sababu mnatuwinda kila dakika. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Heche muda wako umemalizika, tunaendelea na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein na baadae Mheshimiwa Munde ajiandae. Mheshimiwa Yussuf naomba mjikite kwenye mpango tafadhalii.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya tatu asubuhi ya leo, mbele ya ma-sterling. Lakini nashukuru leo nachangia mpango wakati Waziri Mkuu yumo humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisema mara nyingi na tumekuwa tukiishauri Serikali mara nyingi juu ya nchi yetu twende vipi, lakini Waheshimiwa kabla sijachangia nataka niwaeleeze Waheshimiwa Wabunge kwamba tunailamu Serikali hii na zaidi Serikali ya Awamu ya Tano lakini mimi naona wa kulaumiwa ni sisi Wabunge, je, Wabunge tunatimiza wajibu wetu? Kazi yetu sisi Wabunge kwa mujibu wa sheria kwa mujibu wa Katiba ni kuisimamia Serikali, je, tunaisimamia Serikali hii? (*Makofii*)

Kwa hiyo Bunge hili limeshindwa kutekeleza wajibu wake na ndio maana Serikali ikayumba hiyo, hiyo Serikali kama inayumba haifanyi vizuri ni kwa sababu sisi Wabunge tumeshindwa, kwa hiyo, Bunge hili limepoteza nguvu yake, limepoteza hadhi yake, tunashindwa kuisimamia Serikali na ndio maana Serikali inafanya itakavyo. Haiwezekani Bunge hili tupitishe bajeti, sisi sheria inasema, Katiba inasema kwamba tukishapitisha bajeti tuisimamie Serikali, Serikali haifanyi halafu tunaiachia tu hiyo Serikali. Wabunge hatujiamini, tumegawanyika, hatujui wajibu wetu na sidhani

kama tunafaa kuwa katika Bunge hili wote humu ndani. Haiwezekani huo ndio wajibu wetu sisi kuisimamia hii Serikali na hatuisimamii, kwa hiyo, Serikali inafanya itakavyo kwa sababu msimamizi ambao ni sisi Wabunge hatufanyi kazi yetu. Tujitathmini sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mpango mimi nakushauri tena, na naiambia tena Serikali na Waziri Mkuu yupo, ubaguzi huu tunaokwenda nao kwenye nchi hii kubaguana, kutoshirikiana hatuwezi kufikia maendeleo kamwe na kama nchi. Ni lazima tukae kama nchi, tuwe na mpango angalau wa miaka 50 tutakaokubaliana kwamba huu ndio Mpango wa Taifa, hii ndio *vision* ya Taifa, Rais ye yeyote, Waziri ye yeyote, Mkuu wa Mkoa ye yeyote, kiongozi ye yeyote anaekuja aende hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa natoa mifano mara zote, Serikali ya awamu ya nne tulikopa fedha nje ya nchi kwa sababu ya gesi. Leo kaja Rais ana interest nyingine gesi tumeacha Deni la Taifa, hatuwezi kwenda na huwa nasema huwezi kupima maendeleo ya nchi kwa miaka miwili, mitatu, mitano au kumi ni lazima tuwe na mpango ambao kwa muda wa miaka 50 Rais ye yeyote anayekuja, Waziri ye yeyote anayekuja, kiongozi ye yeyote anayekuja ataenda hapo. Sasa kama hatuko hivyo sisi tunaendelea kubaguana tu hapa, tunaendelea kuwawinda wapinzani, tunaendelea kusema huyu mbaya, huyu hivi, hatuwezi kufikia maendeleo, ni lazima tuache tofauti zetu kama Watanzania tunataka maendeleo tukae kitu kimoja tuweke *vision* tunataka nini ndani ya nchi yetu. Ubaguzi huu unaoendelea hatuwezi kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikwambie kama kitabu hiki cha Bunge maana yake ushauri wa Kamati ya Bunge ndio Bunge lenyewe kama huu tutaufuata haya yaliyomo humu tu basi nchi yetu itaondoka hapa ilipo na kupiga hatua mbele. Lakini niulize vitabu kama hivi vimeandikwa vingapi na kipi kimetekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nikuombe pamoja na kwamba nazungumza hunisikilizi, nikuombe

Bunge hili tukitoka tuseme kwamba hili Bunge limeiagiza Serikali moja, mbili, tatu. Tukija Bunge la Januari hapa katika Mkutano wa Kumi na Nne kama Serikali, turudie kwanza yatokanayo na Bunge la Kumi la Tatu je, Serikali tulitaka mfanye hivi mmefanyaje? Kama Serikali haikufanya basi sisi tuchukue hatua kama Bunge kama tunataka maendeleo. Hatuwezi hivyo Waheshimiwa hii ni *mark timer* tunadanganyana. Ukisoma hiki kitabu cha Kamati watu wamekaa, wameandika vitu vizuri, vitu vyatya maana, vitu ambavyo vitatupeleka kwenye maendeleo ya kweli ya nchi yetu, lakini hakuna hata kimoja kinachofanyika.

Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Dkt. Mpango, hebu kaeni, hebu Waziri Mkuu tuondoeni hizi tofauti zetu za kisiasa tulizonazo tukae kama Taifa moja tupange mipango ya nchi yetu tujueni tunakwenda vipi, anayekuja kiongozi yeoyote aende hapo isiwe kila mtu anakuja na *interest* zake hatuwezi kufika. Huwa siku zote naisema na nakuomba hebu tuweke majoribio tu Bunge hili tuliagize Serikali halafu Bunge ljalio tuiulize Serikali kama itakuwa imefanya. Kwa hiyo, hatuwezi kwenda katika mfumo huo tukapata maendeleo kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiyumkiniki nchi zina miaka 48 ya Uhuru wao wana chumi 2 wana mafuta na dhahabu, lakini wametupita mara 5930 sisi tuna miaka 57 ya Uhuru bado tunapiga *mark time* eti leo Tanzania asilimia 16 ya ardhi ya Tanzania maji, lakini Mbunge anasimama hapa anaomba maji kwa Waziri wa Maji si aibu hiyo? Nchi hii kuna mikoa inalalamika njaa wakati asilimia 53 ya nchi hii ni ardhi ambayo ni *productive land*.

Kwa hiyo, hatujajipanga sisi wenyewe na tunakaa sisi wenyewe na kutegemea labda misaada, mikopo na ufadhili lakini sisi wenyewe kama nchi hatujajipanga na hatuwezi kufikia hapo kwa mfumo huu wa kubaguana, kwa mfumo huu wa kunyoosheana vidole lazima tukae kama Taifa Waheshimiwa mimi naomba tuiulize tuna laana gani kwenye nchi hii kila kitu tunacho kila kitu tunacho labda tunapitwa na kwa Afrika tunapitwa na DRC tu, labda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nchi nyingine zote tena kwa *item* moja moja tu lakini vitu vyote tunavyo tuna misitu ya kutosha, tuna maji ya kutosha, tuna ardhi ya kutosha ya kilimo hasa nini tunakuwa hivi ni kwa sababu Serikali hamjaamua sasa na kwa sababu sisi Wabunge tupo hivi labda tuiombe Serikali sasa tuwapigie tena magoti muamue kukaa chini ebu mje tuweke Mpango wa Taifa ambao utatupeleka.

Narudia atamaliza miaka kumi Rais Magufuli pamoja na nguvu yote anayoitumia ataacha hivi katika lawama, lakini ebu tujeni akiondoka Rais Magufuli kama amezisha hiyo reli ya kat iatakayekuja aendeleze asije akiachaka hapa Dodoma kama itakuwa imefika ili tufikie sasa ile lengo, lakini hivi tunavyokwenda hatuwezi kwenda. Mimi napenda kumshauri Waziri katika mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, pato letu dogo kama nchi mahitaji makubwa mahitaji ni makubwa, kwa nini tunaenda kwenye miradi mikubwa ambayo inagharimu pesa nyangi na itachukua pesa nyangi na itachukuwa muda mrefu kuanza kuzalisha tusiende katika miradi midogo ambayo itazalisha kwa muda mfupi? Nilisema hapa kwa mfano kama tutajenga mahotelii 100 katika ukanda ule wa bahari Dar es Salaam au Mtwara mpaka Tanga tukajenga mahotelii 100 hali yanachukua mwaka moja kuyajenga baada ya mwaka tunaanza kuzalisha tunaanza kupata fedha ambazo tutazipeleka kwenye *Stiegler's Gorge*, tutazipeleka kwenye reli na mambo mengine. Leo tunaanza kufanya miradi ambayo inachukua labda miaka mitano, miaka 10 hajjamaliza inakula fedha halafu hatuna njia nyingine ya kupata fedha kwa nini tunaunga kimo kwa kwa kinu? Mheshimiwa hebu twendeni kwenye miradi midogo midogo ili tupate tija kwenye nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein kwa kujikita kwenye mpango naomba na wengine

tuendelee hivyo hivyo. Mheshimiwa Munde baadae Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia Mpango wa Serikali.

Kwanza kabisa ni pongeze Serikali ni mpongeze Rais wangu John Pombe Magufuli, kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini kwa kweli kwa dhamira ya dhati kabisa nimpongeze Waziri Dkt. Mpango hakika Dkt. Mpango amekuwa mvumilivu, amekuwa kiongozi wa mfano, amevumialia mno matusi maneno lakini amefanya kazi kubwa ndani ya miaka mitatu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano Waziri Mpango amefanya kazi kubwa ya kuleta nidhamu ya kuleta pesa za umma, wote tunajua, mmejenga mfumo sahihi ya ukusanyaji wa kodi hakuna asiyejua, kila mwaka mapato yetu ya ndani ya kodi na yasiyo ya kodi yanakuwa yakiongezeka hii yote ni kazi ya Dkt. Mpango, Naibu wake, na Wizara nzima ya Fedha mimi binafsi kwa dhati yangu nawapongezeni sana. Maana kila siku tunawasema kwa mabaya yale mema wanayoyafanya tunashindwa hata kuwatia moyo. Kwa kweli Uwaziri wa Fedha ni kazi kubwa sana lazima tuwapokengeze. (*Makof*)

Nimesikia wapinzani wanasesma utekelezaji wa bajeti hauridhishi, lakini hawasemi bajeti hii imekuwa ikiongezeka kila mwaka, hawasemi wanasesma tu kwamba hairidhishi, kwa sababu tulianza na asilimia arobaini na kidogo tukafata na asilimia hamsini na kidogo sasa hivi tupo na asilimia 57 lakini hivi asilimia 57 zinaonekana kazi inayofanyika inaonekana unawenza ukasema tumetekeliza kwa asilimia 80 lakini ukiangalia kazi haionekani hakika Serikali inafanya kazi kubwa na inastahili kupon gezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nimesikia kuna Mheshimiwa Mbunge amesema Mheshimiwa Rais atamaiza kumi hakuna kilichofanyika amenishangaza sana, mimi niwaambieni

niwaombe mchukue kalamu na karatasi, niwaambie Rais Magufuli ikifika mwaka 2020/2025 ataacha *legacy* kubwa hata sahaulika katika nchi hii ya Tanzania, naomba niwaambie Rais Magufuli ataacha amejenga reli andikeni? Msinitizame Rais Magufuli atajenga *Stiegler's Gorge* na umeme huo mtautumia kwa bei rahisi. Rais Magufuli ataacha amejenga zahanati za kutosha, amejenga vituo vya afya vya kutosha mpaka sasa hivi vituo vya afya ni zaidi 300 ndani ya mikaka mitatu, lakini toka tumepata Uhuru tumejenga vituo vya afya 500 Rais Magufuli miaka mitatu amejenga 300 leo unaniambia Rais Magufuli ataacha amefanya chochote ndani ya nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mimi nasema viongozi wetu labda akili zao zimezidi maana wanafanya mambo makubwa ambayo hatukuyategemea, hatukutegemea kabisa kwamba Rais anawenza kutujengea reli ya kisasa, hatukutegemea kama watoto wetu wasoma elimu bure, lakini leo watoto wetu pamoja na wakwenu wasoma elimu bure.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Hatukutegemea kama mikopo ya vyuo vikuu kuongezeka kwa kiwango hiki, lakini leo watoto wetu wanapata mikopo na wasoma. Hatukutegemea upanuzi mkubwa unaoendelea wa viwanja vya...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bwege kaa chini, taarifa zimefungwa...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Eee!

**MWENYEKITI:** Hakuna taarifa sasa hivi.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Haloo!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munde endelea!

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, zaidi atanunua korosho.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** *Crystapen* tulieni ziwaingie vizuri, mnapiga kelele za nini?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Na korosho atanunua, zaidi atanunua na korosho, itakuwa ni vizuri zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba utulie huko uliko.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanani potezea dakika zangu.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mikopo mikubwa iliongozeka vyuo vikuu na watoto wao wanaosoma kwa mikopo hiyo, tumeshuhudia upanuzi wa viwanja vya ndege, upanuzi wa bandari, ujenzi wa *flyover*, ununuzi wa ndege ambao na wao wanapanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anayesema mpango huu haufai mimi nasema mpango huu unafaa na unaendelea vizuri. Nimesikia Mheshimiwa Mbunge anaongelea kwamba hakuna ajira tangu Rais Magufuli ameingia, jamani tuone aibu, tumuongope Mwenyezi Mungu sisi wote tuna dini humu ndani, tumeapa kwa *bible* na wengine tumeapa kwa misahafu tumuongope Mwenyezi Mungu, tumeajiri walimu 13,000, tumeajiri watu wa afya 8,447 na tumeajiri watendaji wa kata, lakini kila siku ukifungua *website* ya Wizara ya Utumishi wanatangaza nafasi za kazi juzi tu nilifungua namtafutia mwanangu nimeona *UTT* wametangaza, nimeona *SUMATRA* wametangaza, nimeona *TANESCO* wametangaza, nimeona Bandari wametangaza, leo hii mnakuja mnasema hakuna ajira muogopeni Mwenyezi

Mungu, pale tunapofanya kazi nzuri semenii mmeefanya kazi nzuri, pale tunapokosea sio mseme jumla kwa chuki zenu binafsi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia wenzetu hawa sana wanaongea kuhusu swala zima la Katiba, kwamba Katiba imeachwa, Katiba imefanya nini mimi niwaambie ndugu zangu hawa waache kutafuta kiki za kisiasa, tulivyokuwa kwenye Bunge la Katiba walitoka nje, Katiba ilipitishwa na watu wachache kwa busara ya viongozi cha Chama cha Mapinduzi wakasema mapendekezo ya wachache yatachukuliwa na yatakwenda kuwaambia wananchi kupendekeza Katiba. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza walijiunga kama UKAWA wakatembea nchi nzimaya Tanzania kwamba Katiba Isiungwe mkono iliyopendekezwa leo nawashangaa watu hawa yametoka wapi leo nawashangaa watu hawa wanaililia Katiba ninyi si mlkwenda nchi nzima kusema Katiba inayopendekezwa isichukuliwe? (*Makof!*)

**MHE.AMINA SALEH MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina tuvumiliane nilisema taarifa basi.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu wanani potezea muda wangu.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasinilisema taarifa basi tunaomba tukae tuvumialiane.Mheshimiwa Munde naomba tuendelee.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru lakini naomba walionipotezea muda wangu waniangalizie dakika zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu hawa walienda nchi nzima wakajiunga UKAWA wakaanza kusema Katiba iliyopendekezwa isiungwe mkono leo nashangaa wanasema Rais anakataa Katiba Mpya, mimi naomba nimuombe Rais wangu asitoke kwenye reli, Rais Magufuli wakati anaomba kura aliwaahidi Watanzania maendeleo, hakuwaahidi Watanzania Katiba, wananchi wanataka maendeleo, wananchi wana taka reli, wanataka zahanati, wanataka maji wanataka dawa, wananchi awataki Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna mkakati, wa kumtoa Rais Magufuli achukuwe mamilioni aweke kwenye Katiba tushindwe kutimiza malengo waje watuhoji, mimi niwaambie hatutakubali. Mhe.Rais usikubali ujinga huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Katiba limeeleweka naomba sasa kuhusu suala zima la usalama. Kumekuwa na masuala ya usalama yanaongeleva kwamba nchi hii haina usalama, nchi hii watu wanatekwa, nchi hii watu wanauwawa, suala la usalama ni suala la janga la dunia, Marekani wanalindwa kwa mitandao kwa mitambo kwa *satellite* lakini nikwambie kwa siku wanatekwa zaidi 240 kwa siku. Mimi nadhani imefika wakati sisi Wabunge tupige kelele tuiambie Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi iongeze pesa kwenye vyombo vyetu vya usalama, iongeze *training* za vijana wetu wa usalama, *training* za polisi, *training* za jeshi letu ili kukabiliana na janga kubwa liliopo la uwaliu katika nchi yetu linalotaka kungia hili ni janga la dunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia juzi mwandishi wa habari kule ametekwa, ameuwawa mpaka leo wenzetu wale wamesonga mbele kiteknolojia bado hawajapata uhakika nani kafanya. Lakini leo likitokea Tanzania imefanya Serikali, mimi napata taabu Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Tabora kutoka nikiwa mdogo kule kwetu mauwaji ya vikongwe yanaendelea, mauaji ya kimapenzi yanaendelea,

wanauwaga polisi kila siku? Mbona yapo na Serikali zote zipo zimepita na Serikali zinapambana na hayo mambo.

Kwa hiyo, mimi nitoe rai yangu Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu unanisikia upo humu ndani, niombe sana Serikali iongeze pesa kwenye vyombo vya usalama, wakawasomeshi watu waweze kukabiliana na teknolojia za hawa watu wahalifu wao na teknolojia za kisasa na sisi tupate teknolojia za kisasa ili tuweze kukabiliana nao ili ndiyo naweza kulisema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo Tume Huru ya Uchaguzi watu hawa wamekuwa wakiongea kwamba tunataka tume huru Katiba mpya ibadilike mimi naomba niwalilize humu ndani wapo zaidi ya asilimia 30 waliingiaje kama hakuna Tume Huru waliingiaje ndani watu hawa, wamezidi zaldi ya 100 tupo Wabunge 300 na kidogo wenzetu hawa wako zaidi ya 100 walifikaje humu ndani kama wako zaidi 100 kama hakuna Tume Huru ya Uchaguzi wasitake kututoa barabarani, wasitake kututoa kwenye reli tunataka maendeleo kama anavyosema Rais wetu John Pombe Magufuli. Tunamuombea kila heri Rais wetu amkinge na mapala na manuksi ya maneno yenu ya ajabu ajabu *inshallah*. Ahsante kwa kunipaa nafasi hii. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Munde kwa mchango wako na kwa ushauri wako mzuri kwa Serikali. Tunaendelea na Mheshimiwa Richard Ndassa na baadaye Mheshimiwa Deo Sanga ajiandae.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii niunge mkono Mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2019/2020 pia naunga mkono mapendekezo na maoni ya Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binadamu na wanyama kimahitaji tunafanana ila tofauti binadamu anaufahamu na kujitambua; mnyama ajitambui lakini binadamu anaufahamu wa kujitambua, inapotokea binadamu akajitoo ufahamu wa kujitambua huo ni uvivu wa kufikiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapotokea Mheshimiwa Mbunge aliyeCAA miaka mitatu ndani ya Bunge aliyeCAA miaka mitano ya nyuma ndani ya Bunge asitambue yote yanayofanyika huo ni uvivu wa kufikiri kutokuona yote hayo hata huu mpanga bahati nzuri Mheshimiwa Mpango umetuambia vizuri sana jamani eeee naomba tujikite kwenye mpango ili kusudi maoni, ushauri na mapendekezo yenu baadaye sasa iwe mpango sasa wa maendeleo uwigizwe kwenye Mpango wa Maendeleo wa 2019/2020 ulitushauri hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inasikitisha badala ya kuzungumzia mpango wenyewe kwa mfano mimi nitashauri tukiachana na haya mengine Mheshimiwa Mpango nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wa kuthubutu wala kutokuogopa mtu wala nchi yoyote ile kuhusu mradi wa *Stiegler's Gorgen* hili Mheshimiwa Mpango, Waziri wa Mipango sisi hapa kama mradi huu ukikamilika tutapata *megawatts* 2,100 ni tija kwa Taifa hawa wanaosema eti watu wa nje wakichukia, sisi tulikuwa tunaitaji kilometa za mraba 100 wala siyo zaidi ya hapo kilometa 50 urefu na kilometa mbili upana ili tupate *megawatts* 2,100 hivi kweli hii ni rasilimali ya Taifa rasilimali ya nchi hii tumepewa na Mungu hivi unapoogopa kutumia cha kwako utumie cha nani? Eti kwa sababu watu wa nje watanuna wache wanune hili ni Taifa huru. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Mpango katika mpango wako kuna mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma ili nafikiri tangu ukiwa Katibu wa Mipango limekuwepo, tumelisema, tumelisema sasa tuondoe kwenye *story* sasa tuweke kwenye uhalsia ebu tufike mahala sasa tuamue kwamba je? Huu mradi wa makaa ya mawe Liganga na Mchuchuma bahati nzuri mmewakabidhi *NDC* hebu sasa tufikie pahala tumalize hili suala baada ya kukaa kila mwaka inakuja, lakini ili tuendane na sekta ya viwanda ni lazima Mheshimiwa Mpango kuna maeneo mawili/kuna viwanda viwili; *Kilimanjaro Tools* na *Mang'ula Tools* hizi kama zitaimarishwa zitaenda kulisha mitambo ya viwanda vyetu, naomba hili tusilionee aibu lazima tulitekeleze. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ushauri katika kuboresha shirika letu la ndege la *Air Tanzania* tunategemea ikifika Oktoba 2019 tutakuwa na ndege nane, lakini tatizo kubwa ambalo lipo ni upungufu wa marubani. Marubani walipo leo ni 33, marubani 16 wameenda mafunzoni na ndege hizi nane zinahitaji jumla ya marubani 70; marubani hao 70 ni lazima wawe wazalendo. Na wewe kwenye kitabu Mheshimiwa Dkt. Mpango umeandika kwamba kusomesha kwa wingi katika fani na ujuzi adimu na maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii fani ya urubani ni fani maalum na adimu na lazima tupate marubani wetu wazalendo ili waje waendeshe ndege zetu hizi ili kupunguza gharama. Tukitegemea marubani wa nje gharama itakuwa kubwa zaidi.

Nimuombe sana Mheshimiwa Dkt. Mpango, hili la marubani nafikiri ni jambo jema tukapata marubani wetu wakaenda wakafanya mafunzo kwa sasa kabla ndege zingine hazijaja hizi maana zingine zikafika mwezi wa kumi na moja nyingine mwakani. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Mpango, ndege hizi zitahitaji marubani wazalendo wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Dkt. Mpango, Kanda ya Ziwa tunalima sana pamba, lakini bahati mbaya hatuna viwanda vyatago sasa mazao yanayotokana na pamba hivi tunafurahia sisi kusafirisha marobota kutoka Sumve kuyapeleka Dar es Salaam.

Kwa hiyo nikuombe sana Mheshimiwa Dkt. Mpango katika mpango wako kwa sababu hii ni Serikali ya viwanda na mazao yale yapo sasa kama pamba hebu tuwe na utaratibu agalau wa kusimamia Wizara ya Viwanda na Uwekezaji hebu Bwana Mwijage aje na mpango maalum na kamati yake kuhusu mazao ya biashara pamba, korosho, kahawa ili mazao hayo ikiwezekana yawe yanabanguliwa humu ndani na kufanya *packing* humu ndani ili baadae tuuze

sasa badala ya kuuza *raw material* tuuze bidhaa ambayo imechambuliwa tayari na kwenda nchinje kwa ajili ya kuongeza thamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni kuombe sana suala la Mkoa Mwanza, Simiyu, Mara lazima tuwe na kiwanda kinchotengeza nguo na inawezekana basi angalau kimoja tu Mheshimiwa Mpango kimoja tu kanda ya ziwa angau kwa kuanzia ili zao lile la pamba liweze kutumika badala ya kusafirisha marobota, tupate kiwanda kimoja cha kutengeneza nguo na mahitaji ni makubwa sana ya nguo za aina mbalimbali huo ndio ulikuwa ushauri wangu Mheshimiwa Mpango na nikushukuru sana na nikuombe usiogope hizi kelele za huyo, huyo, huyo, wewe songa mbele tu watu wapige kelele lakini si tunajua tutafika wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndassa, tunaendelea na Mheshimiwa Deo Sanga baadae Dkt. Kamala ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niungane na wenzangu kujadili Mpango huu wa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii ya kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano ya Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli pamoja na Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa, pamoja na Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri ambayo leo tunajadili hapa ya Dkt. Mpango, kwa kupitisha bajeti ile ambayo tulikuwa tunakaa hapa na ndio sasa tunayaona yaliyokuwa yanafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mpango tunakupongeza sana na timu yako na wataalam wako na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo ipo mbele yetu, kwa kweli lazima tuwe wakweli,

nianze na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Mpango imezungumzwa hapa kuna baadhi ya watu wanasesma bajeti iliyoongezeka zaidi ya bilioni mia mbili na kitu bado hawaoni maana yake, mimi nimebaki nashangaa Waheshimiwa Wabunge. Hivi bajeti ile si baadhi ya vituo, zahanati na vituo yya afya ambavyo vimejengwa si lazima fedha ziongezeke? Kazi nzuri imefanywa sana na Serikali. (*Makofii*)

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa, hii sio bajeti ajikite kwenye mpango.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ikiwepo kwenye jimbo langu vituo afya viwili vimeongezeka na hospitali ya Wilaya ya Halmshauri, lazima tuipongeze Serikali kwa kazi nzuri ambayo inafanywa hivi sasa kituo cha afya kwenye jimbo langu mwezi wa pill kinafunguliwa kwa fedha ambazo Serikali ya Awamu ya Tano kama walivyosema wenzangu vituo zaidi ya 300 na kila Jimbo nadhani vituo hivyo visto. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali hata mwenzangu jirani ananiambia hata Tarime visto, eeh kwa hiyo lazima tuipongeze sana Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tukija kwenye upande wa maji, mwenye macho haambawi tizama maji katika nchi nzima asilimia kubwa imepungua hata kwenye jimbo langu tu suala la maji ipo miradi inaendelea pale iko miradi mingi katika jimbo langu, ni fedha tu kwa hiyo Mheshimiwa Mpango tunakupongeza. Ipo miradi ile 26 ya maji katika nchi, katika miradi 26 mradi mmoja upo kwenye jimbo langu katika mpango huu wa wewe Mheshimiwa Mpango. Sasa tunaipongeza sasa Serikali ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija miundo mbinu ya barabara za kuunganisha mikoa kwa mikoa, leo mtu anatoka kule Mbinga kwa Mheshimiwa Mapuda, anatoka Mbinga asubuhi ikifika usiku anakuwa Mwanza, barabara zimetengezwa ni fedha hizi za Awamu ya Tano. Kwa hiyo tunaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija barabara pale kwangu pia kwenye jimbo langu barabara za lami zinatengenezwa, ukitoka pale iko barabara ambayo barabara kuu ya kutoka Dar es Salaam - Zambia sasa hivi kwenye jimbo langu pale Makambako barabara na viunga vyake vinapendeza sana, kwa hiyo tunaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumzia hapa reli wenzenetu wa kanda ya ziwa wamekuwa wakipata taabu sana juu ya reli hii ya katiki, Serikali imechukua jukumu ya kuishughulikia reli hii, watu wanasema aaa mpango sio reli; kupanga ni kuchangua. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Mpango kwa namna ambavyo umeelezea hapa kwamba reli hii lazima inakamilika songa mbele kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Ndassa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukija upande wa ndege, nimewahi kusema hapa Bunge la mwaka 2013 hapa na baadhi watu walikuwa wanazungumizia hapa duniani kokote kule hamuwezi kuwa mkawa hamna ndege za nchini kwenu, Rais amechukua jukumu la kununua ndege katika nchi yetu, tunaipondeza sana kwa taarifa hii ambayo kuna ndege zingine zinakuja mwakani mwezi Novemba, tunakupongeza Dkt. Mpango na Serikali ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri ambapo ndege hizi zitapunguza kero mbalimbali ambazo watu walikuwa wanapata tabu kusafiri lakini zitaongeza utalii wa ndani, Mheshimiwa Mpango songa mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipofanya ziara kwenye Jimbo langu mikutano 65 nimefanya kila siku nilifanya mikutano mitatu hakuna mwananchi hata mmoja aliporuhusiwa kuuliza maswali aliyezungumzia Katiba hayupo hata mmoja hayupo! Hata mmoja hayupo, watu walikuwa wanaauliza habari ya maji, barabara, pembejeo na kadhalika hakuna. Sasa leo tuanze kupoteza fedha kwa ajili ya Katiba, niombe sana Serikali na Rais na Waziri Mkuu upo hapa msijadili habari Katiba wananchi sio tatizo Katiba. Tatizo ni maendeleo katika maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kazi iliyofanya Serikali ya Awamu ya Tano, tumuombe Mheshimiwa Spika na Wabunge wote baada ya kumaliza Bunge hili sijajua linaisha lini tufanye *party* ndogo ya kuipongea Serikali kwa kazi nzuri iliyofanywa, kwa hiyo, nikuombe Mwenyekiti jambo hili lipewe kipaumbele tufanye *party* ndogo ya kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo inafanya kazi na leo narudia, kwa kazi iliyofanywa kwa miaka mitatu unadhani ni kazi ya miaka 20 huo ndio ukweli. (*Makofi*)

Sasa narudia kwa maneno haya niliwahi kusema Bungeni hapa, Rais wa China kwa kazi nzuri amekuwa akifanya na Marais wengine nchi mbalimbali wenzetu kule walisema awe Rais wa maisha. Narudia Rais huyu awe Rais wa maisha kutokana na kazi nzuri anayoifanya, lazima tuwe wa kweli, lazima tuwe wa kweli hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maeleo hayo naunga mkono hoja, ya Mpango wa Dkt. Mpango kwa kazi nzuri, songa mbele na nakushuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Sanga tunaendelea na Dkt. Kamala na baadaye Mheshimiwa Elibariki Kingu ajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba nianze na kusema kwamba naunga mkono hoja lakini pia naomba nijikite kwenye changamoto ya kwanza ambayo Mheshimiwa Waziri ametueleza katika kitabu chake cha hotuba kwamba ndio changamoto kubwa ziko nyingine, lakini yenyewe ni ya kwanza ambayo ilichangia katika kutekeleza vizuri kama tulivyokusudia na changamoto yenyewe ni kwa sababu tuna wafanyabiashara walio kwenye sekta binafsi hawana sehemu maalum, hawatambuliki, kwa hiyo inakuwa ngumu kwa Serikali kukusanya kile ilichokusudia kukifanya. Kwa hiyo, ningependa kushauri mambo yafuatayo kuhusiana na jinsi ya kukabiliana na changamoto hiyo.

Kwanza, naishauri Serikali wakati umefika kwa kutumia *Geographical Information System (GIS)* katika kuwatambua wajasiliamali katika kukusanya kodi katika kujua nani amelipa na nani hajalipa. Ninaposema *GIS* sitaki sihitaji kusema maneno mengi kwa sababu ndio mfumo wa kisasa unaotumika, na habari nzuri hapa Tanzania wataalam wa kuandaa mifumo hii wapo na kuna kampuni moja ambayo imeandaa mfumo inaitwa *Digital City Services* Mheshimiwa Waziri utakuwa unafahamu kwa sababu nina uhakika wataalam wako wanajua kuhusu kampuni hii na kampuni hii imefanya kazi kule Njombe kuhusu *property tax* walipohamishia zile shughuli kwenda kule Wizarani hiyo *project* ikasinzia, lakini pia hivi sasa Manispaa ya Iringa ipo mbioni ku-*adapt* utaratibu huu kwa *GIS*. Sasa kama hili jambo lipo na linawezekana na mfumo huu ni mwepesi maana tunatumia simu tu, utaalam tuanao Mheshimiwa Waziri nashauri uangalle eneo hili na tuone jinsi gani tukatumia *GIS* katika kukabili changamoto hii.

Ushauri wa pili, Mheshimiwa Waziri unapoangalia wajasiriamali mfumo wetu wa kodi tatizo ninalolliona moja unavyomuangalia mama ntilie ndio hivyo hivyo unavyomwangalia mfanyabiashara mkubwa au kampuni kubwa kama *TBL*. Sasa unapokuwa na mfumo unaofanana katika ukusanyaji kodi huo huo unaupeleka kwa mfanyabiasha mkubwa kama *TBL* mfumo huo huo unaupeleka kwa majasiriamali mdogo, lazima utapata shida Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, ushauri wangu na wataalam wapo wa kusaidia katika hilo tuandae *tailor made regime* kwa ajili ya *informal sector*. Tukifanya hivyo Mheshimiwa Waziri tutakuwa tumepiga hatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa tatu ni kuhusu kodi katika *economics* nyepesi lazima iwe *certain*, lazima mtu awe anajua akiagiza bidhaa atalipa shilingi ngapi, sio baada ya kuagiza anapofika pale kuanza kulipa anakuta mambo yanabadilika, nasema hivyo kwa sababu tatizo kubwa tulionalo hapa ni kwamba unaweza kukaagiza vitu kwenye kontena lile lile, vitu kutoka sehemu ile ile, waagizaji tofauti lakini kila mtu anaambiwa kodi yake ya

kulipa. Sasa hii sio sawa Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo lazima tuweke utaratibu ambao utakuwa *certain* ili mtu yejote mfanyakibasha anapoenda Dubai, anapenda China anapoenda popote duniani awe anajua akija pale bandarini alipa shilingi ngapi na hilo lisibadilike badilike. (*Makofii*)

Kwa taarifa yako Mheshimiwa Waziri wapo wananyabiashara wengi wa Tanzania wamaamua kutumia bandari za nchi nyingine kwa kuogopa kwamba watakapofika pale kwenye bandari yetu wataambiwa bei ambazo ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa nne ni utararibu wetu, hili ni jambo la *capacity building* tusitarajie kukamua maziwa kutoka kwa mfugo kama unafunga ng'ombe huwezi kukawa unapanga kukamua maziwa mengi bila kumlisha ng'ombe huyo vizuri. Nasema hivyo kwa sababu hawa wajasiriamali wetu hawa watalipa kodi kama wataweza kuwazeshwa masuala mbalimbali mojawapo ni vitu vidogo tu kwa mfano tulikiwapa *simple skills* za *accounting* wakazijua, unaweza ukaanzisha programu ya *accounting system* nyepesi tu ya kufundisha tu hata unawezana ukatumia hata wanafunzi ukitoa elimu hiyo kwa wajasiriamali wetu watawea kutambua nini wafanye ili waweze kulipa kodi vizuri na Serikali inanufaika na utaratibu huo.

Jambo lingine ni elimu ya kodi, tatizo kubwa tunalolipata katika biashara hizi wafanyakibasha wadogo wadogo/wajasiriamali au wataalam wetu wa kodi anapoenda kwa mfanyakibasha huyo anaanza kumwambia hiki mbona hujafanya, hiki hujafanya, kile hujafanya, hiki hujafanya, kwa hiyo na huyo kwa kuwa hajui basi anaishia kukimbia mwengine anaishia kujificha au kulazika kulipa kodi kubwa ambayo siyo, hii ni kwa sababu kutokuwa na elimu hiyo. Sasa kwa kuwa muelekeo Watanzania wengi watakuwa wajasiliamali wakati umefika katika mitaala ya elimu ya msingi kuanza kutoa elimu ya kodi. Mheshimiwa wa Waziri wa Elimu atusaidie katika hili lakini Serikali ijpange

tuone ni kwa namna gani vijana katika shule za msingi kuanzia kule wanaweza kuanza kupata elimu ya kodi ili wanapofika kwenye kujajiri isije kuwa jambo jipya.

Ushauri wangu mwingine ambao napenda niutoe haraka haraka lazima tu-*simplify system* yetu ya kodi, iwe nyepesi, lakini pia ambapo ni jambo dogo ukiliangalia upokuja kwenye kulipa kodi kuna suala la kandaa *returns*, kuna suala la manunuzi na mauzo, mfanyabiasha wa mchele kwa mfano anayefanya biashara ya mchele anapoenda kununua mchele wake ananunua maeneo mbalimbali huko vijijini na mara nyingi hizi risiti zinakuwa hazipo. Lakini ukimuuiliza ya mauzo risiti atakuwa nayo ya mauzo unapomuuiliza risiti ya manunuzi hana tatizo linaanza, lakini kwa mfano ukaenda pale Mwenge ukakutana na wafanyabiasha wa vinyago yule mfanyabiasha wa vinyago ukimuuiliza risiti za mauzo anaweza kuwa nazo, lakini ukimuuiliza risiti za manunuzi ya kinyago kile mpaka kimefikia pale hana, tatizo linaanza.

Mheshimiwa Waziri uanglie ni kwa jinsi gani tunaweza tukasimplyeneo hilo ili kuweze kuondoa huo utata ambao unasumbua. Lakini pia ukienda kule Kanda ya Ziwa bidhaa nyingi tunatumia za kutoka nchi za jirani hakuna *Special Economic Processing Zone* na shauri izingatiwe na nishauri poa kule Kajunguti ambapo tulilikuwa tujenge uwanja wa kimataifa wa ndege sasa hatujengi, lakini tuweke *Export Processing Zone*, tukifanya hivyo tunaweza tukatumia lile eneo vizuri na kuendelea kupiga hatua.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kamala tunaendelea na Mheshimiwa Elibariki Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mimi kuweza kuwa na mchango wangu kama Mbunge katika kuishauri Serikali yangu, Serikali ya Chama cha Mapindinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa unyenyekevu mkubwa kabisa kutambua kazi kubwa na *commitment* kubwa inayofanya na uongozi wetu katika kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi, ikiongozwa na jemedari wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *its an disputed* kabisa kwamba amesema dada yangu Mheshimiwa Munde, *legacy* ambayo inakwenda kuandikwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Tano *is an questionable* na inakwenda kuonesha vitu ambavyo Taifa litakumbuka vizazi na vizazi.

Mimi nitumie fursa hii kwa dhati ya moyo wangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye kwa muda mwingi tumekuwa naye humu Bungeni, tumekuwa tukisema na kupongeza watu wengine lakini tumemsahau kiongozi huyu mkubwa kabisa wa shughuli za Kiserikali Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa amekuwa akifanya kazi kubwa ya kuhangaika mikoani na kwenye majimbo kupambana na mambo ya kahawa, kupambana na mambo ya korosho, kupambana na mambo ya maji, Mheshimiwa Waziri Mkuu leo mimi kijana wako nataka nitambue kazi yako kubwa unayoifanya katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitumie fursa hii kumpongeza sana kaka yangu Dkt. Mpango, *the good thing* kwa Dkt. Mpango ninachokiona mimi mionganini mwa viongozi wenye msimamo hasa katika sekte na Wizara nyeti kama hii, Dkt. Mpango ninakupongeza. Mimi nimebahatika kufanya kazi na Dkt. Mpango nikiwa Mkuu wa Wilaya ya Igunga, kuna kipindi nilifanya *coordination* ya kuwa-*organize* vijana wa vyuo vikuu katika sekte ya kilimo, Dkt. Mpango akiwa anafanya kazi Tume ya Mipango alifunga safari kuja kutembelea miradi ya vijana kwa muda wa siku tatu Igunga na kutoa ushauri. Kwa hiyo Dkt. Mpango mimi ninakupongeza

wewe ni mزالendo na kubwa zaidi ni kiongozi usiyeyumba katika masuala ya kodi, hiyo ni sifa kubwa sana kwa kiongozi. (*Makof*)

Naomba nijikite katika mchango wangu kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, kwanza, Rais wetu amekuja na *vision* akitekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi ya ku-*industrialize* nchi, hili nimelisema toka nilipoingia hapa katika Bunge hili kikao cha kwanza kabisa, tunapozungumzia habari ya kutaka ku-*industrialize* nchi hatuwezi kuacha kuweka *connectivity* kati ya mambo ya *industrialization* na masuala mazima ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niishauri Serikali ya Chama cha Mapinduzi, katika sekta ya kilimo mwanzo tulivyoanza nilianza kuona kwamba tunakwenda vizuri, lakini katikati naona kuna mahali tuna-*stuck*, tulianza kuzungumzia mazao ya kimkakati, Bunge la kwanza nilizungumzia na kaka yangu Dkt. Mpango uko hapa nilizungumzia habari ya wakulima wa pamba wa *lake zone*, nilizungumzia habari ya wakulima wa mazao ya alizeti katika mikoa ya kanda ya kati na baadhi ya mikoa ya mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema Tanzania (Taifa letu) tunapoteza fedha nyingi sana katika kuingiza mafuta kutoka nje ya nchi mafuta ya kula nikasema *potential* tuliyonayo katika kilimo cha alizeti tukiamua kufanya *intensive investment* Taifa letu litaondokana na habari ya *importation* ya mafuta tuta-*save foreign currency* na tutaweza kuinua uchumi wa nchi. Ninachokisema ni kwamba siaona *connection* iliyopo kati ya Viwanda na sekta ya kilimo hasa katika kilimo cha alizeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali, ni wakati muafaka sasa kuhakikisha ya kwamba Serikali inatoa *incentive package* kwa wakulima wa mazao ya alizeti, kaka yangu Dkt. Mpango lichukue hili na mwakani kwenye bajeti

lilete toeni *incentive* katika mbegu za alizeti, toeni *incentive* katika masuala mazima ya pembejeo tuweze ku-*boost productivity na kuongeza tija* ili Viwanda viweze kupata *raw material*. Mimi hapa ninapozungumza Jimbo langu linapakana na Jimbo la Iramba, kuna kijana mmoja mjasiriamali amefungua Kiwanda cha Alizeti hapa ninapozungumza amepata *market Rwanda*, anauza Congo, anauza Zambia...

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Anaitwa Yaza.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Anaitwa Yaza, ahsante Mheshimiwa Mama Martha Mlata. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya tukiweza kufanya Mheshimiwa Waziri tutaweza kulisaidia Taifa hili na tutaweza kutengeneza wajasiriamali wa katil watakaoweza kufanya *investment* kwa sababu hawa ndio wazawa wenye uchungu na hili Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ushauri wangu ninaoutoa kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, tunazungumzia suala la viwanda, Rais John Joseph Pombe Magufuli amekuja na *ideology* ya kutoa elimu bila malipo shule ya msingi, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango uko hapa na mama yangu Mheshimiwa Profesa Ndalichako najua uko hapa ninajua wewe ni mama bingwa ni Waziri uliyeimudu Wizara yako ya Elimu, mimi ninakupongeza sana mama yangu ushauri wangu ninaoutoa, mwakani njooni na mpango wa kuhakikisha *vocational education* inakwenda kuwa bure kuanzia mwakani, tukifanikiwa kuweka *vocational education* kuwa bure tutaweza kutengeneza *class* ya *technocrats* ambao watakwenda kutumika katika viwanda ambavyo tunampango wa kuhakikisha kwamba Taifa letu linakwenda kuwa Taifa la viwanda. Kama tumeweza kutoa elimu bila malipo kwa shule za msingi Mama Ndalichako ukiwasiliana na Mheshimiwa Dkt. Mpango mkafanya *coordination* ya kuangalia tuna vyuo vingapi vya ufundi Tanzania, *skills zinazohitajika* kwa ajili ya kwenda ku-*feed* watu kwenye viwanda, tukawekeza kwa vijana wetu wa *vocational*

*education mimi nataka niwaambie in next ten years viwanda vinavyojengwa hatutategemea technocrats kutoka nje ya nchi tutawatumia wazawa kutoka katika nchi yetu. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango huu ndio ushauri wa Kibunge mimi nataka muuchukue achaneni na watu wanaopiga blaa blaa! Watu wanaotaka kutukatisha tamaa, kazi ya Wabunge ni kuja kuishauri Serikali na kutoa mawazo mbadala kwa maslahi ya kuhakikisha Taifa letu linasonga mbele, habari ya kuja hapa kuja kuanza kumtukana Dkt. Mpango sijui mpango umefanyaje. Mimi nataka niwaambie jimbo ninalotoka la Singida Magharibi nimezaliwa kijijini mimi baba yangu alikuwa ni mwalimu *for almost 30 years* chini ya kipindi hichi nimeshuhudia kwa macho yangu najengewa vituo karibu vinne vyta afya *on the spot* mambo haya hayakuwepo kwani hizi fedha zamani hazikuwepo? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza habari ya kuja uchumi wa nchi ni pamoja na ku-*improve social service* ku-*improve social welfare* za watu wetu. (Makof)

Mheshimiwa Dkt. Mpango ushauri wangu mwingine ninaoutoa tuiangalie sasa sekta binafsi kwa kuwaangalia *entrepreneurs* wa Kitanzania tuwaangalia entrepreneurs wa Kitanzania na kuwalinda. Ndugu zangu nataka niwape mfano mdogo kwa nini tunasema kwamba *Kenya is one of the largest ten investors* kwenye nchi yetu, Kenya ni miongoni mwa mataifa kumi yaliyowekeza Tanzania sana kwa sababu gani wamekuwa wajanja sana wanachukua *private sector* yenye teknolojia kutoka nje, wanakuja wanazisajili kwao kazi zote zinatoka *East Africa* wanatokea Kenya wanakuja Tanzania wanachukua kwa sababu wameangalia fursa kwa jicho la pili. Niwashauri Mheshimiwa Dkt. Mpango na timu yako tusi-*discourage private sector* kwa maana ya kuwalinda Wazawa wanapokuwa wamebuni na kuanzisha vitu ninaiomba Serikali yangu ya CCM iangalie hili kwa jicho la ukaribu sana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti tutakapoweza kutengeneza *middle class* na entrepreneurs ya kwetu hawa ndio watakaokwenda kuwekeza kwenye Viwanda vya korosho tunavyovitaka hawa wahindi wanaokuja Wafanyabiashara tunawapenda hawawezi kuwa na uchungu kwenda kuwekeza kwenye viwanda vya kubangua korosho tukiwezesha *middle class* ya kwetu, *entrepreneurs* wa Kitanzania hawa Mheshimiwa Dkt. Mpango wanatakuwa na uchungu viwanda ambavyo Rais Magufuli anavipigia kelele vitafunguliwa ninawashauri kwa dhati ya moyo wangu kila mahali alipo *entrepreneur* wa Kitanzania tusimvunje moyo, ninawashukuru sana ninajua hili linalelewka na ninajua mna-take note na ninajua kaka yangu Dkt. Mpango unaelewa mdogo wako ninachokisema. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Ahh! Muda umeisha?

**MWENYEKITI:** Tayari ya pili.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kidumu Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea sasa zamu ya Mheshimiwa Silinde baadae akitoka huyo atakuja Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kunipa fursa hii kuchangia Mapendekezo ya Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamezungumza ndani ya Bunge lako Tukufu walau kuna waliota mchango wa maana kuna wengine wameingiza kidogo siasa, lakini ndio maana ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niende kwenye mpango na ninataka Dkt. Mpango unisikilize vizuri kweli kweli ukipitia hotuba yako ukurasa wa 34 ambapo unajadili changamoto za utekelezaji wa mpango wa maendeleo na bajeti:-

(i) Serikali inasema ugumu wa kukusanya kodi kutoka kwa wafanyabiashara waliopo katika Sekta isiyo rasmi kwa kuwa hawana sehemu rasmi za kufanyia huduma ya Kibashara, hiyo ni moja Serikali imekiri.

(ii) Kutofikiwa kwa lengo la Kodi zinazotokana na ajira (*Pay As You Earn*) kilichosababishwa na kutofikiwa kwa malengo ya ajira mpya na kutokuongezeka kwa mishahara kwa wafanyakazi kama ilivyokuwa imetarajiwu haya Serikali inakiri. Hebu *imagine* Serikali ilikuwa inaanizisha chanzo haijui kama mishahara itaongezeka halafu leo tunakaa ndani tunajadili, Serikali yenyewe inakiri kwamba jamani tumeshindwa kwa sababu mishahara haijaongezeka kama tulivyokuwa tunatarajia tulikuwa tunapitisha mpango wa nini?

(iii) Sasa unakuja inakwambia kushuka kwa biashara za Kimataifa kulikopelekewa kutofikiwa malengo ya uagizwaji wa bidhaa kutoka nje, Serikali imekiri, watu wanazungumza yenyewe imekiri, imeandika ukurasa huu wa 35.

(iv) Upungufu wa Wafanyakazi na Vitendea kazi ndani ya Mamlaka ya Mapato Tazania yaani mpaka leo Serikali yaani wakusanyaji mapato hawana Vitendea kazi mnajadili nini yaani hapa tunajadili nini?

(v) Kupungua kwa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo wakati wa utekelezaji wa bajeti.

(vi) Changamoto ya masoko na bei ndogo za mazao kwa wakulima, Serikali imekiri yenyewe mapungufu.

(vii) Kuendelea kuwepo kwa madai mbalimbali yakiwemo ya wakandarasi, watoa huduma, wazabuni na watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikiria malalamiko ya Serikali ambayo yalivyo *genuine*. Sasa kazi ya Bunge ambayo ilipaswa leo tuijadili hapa cha kwanza ilikuwa ni kwa namna gani tunaweza tukatoka hapa, *that was number one*. Mimi nimejaribu kuitia mpango hapa tangu jana napitia nimeangalia kila nikijaribu kuangalia sasa Serikali imekuja na mpango itautekelezaje mwakani kwa sababu mpango bila fedha ni kazi bure, *is a nonsense. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi zote zinazopigwa hapa zitabaki kuwa stori tuu sasa unakuja kugundua, mimi wiki iliypita, wiki mbili nilikuwa Rwanda kuna kitu nimejifunza na ningependa Tanzania ikajifunza. Nchi ya Rwanda kabla Mawaziri hawajateuliwa na Rais Kagame wanapewa *perfomance contract* unasema mimi Waziri wa Fedha nikiwa Waziri nitafanya moja, mbili, tatu, nne, tano, ukishindwa kutekeleza unaondoka *automaticaly*, hakuna mjadala.

Sasa leo kwetu humu ndani unakuta mtu analinda Uwaziri kwa kusifia sio kwa kutenda kazi, leo tukiwapima Mawaziri hapa tukasema Waziri gani *number one* na wa mwisho ni nani? Sisi wenyewe Wabunge tunajua nani anapiga porojo hapa ni waongo tu, nani wanamdaganya Rais tunawajua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tunawajua hapa wote ninyi mlivyo, sasa matokeo yake mtu anayejua kusifia sana ndio anayeonekana anafanya kazi, tunaliangamiza Taifa hili. (*Makof*)

Sasa ukipitia hapa unaenda unaangalia mafanikio ya utekelezaji wa mpango unakuta Serikali imeandika pale kwamba ulipaji wa madai, eti Serikali mafanikio kulipa madai mlikuwa mnakopa mlikuwa hamjui hamtalipa? Yaani ipo kabisa kwenye hotuba ukurasa wa 31 eti madai, kulipa madai kweli jamani? Kwenye hotuba kabisa unaandika kabisa

kabisa yaani na watu wanavuka kama hawaelewi unakuta mtu anakuja anaandika hapa kwamba huduma za maji, kwa mfano soma ukurasa wa 31 mimi imenishtua ndani ya miaka mitatu kwamba ukurasa wa 31 wa hotuba inasema; "Miradi 1595 ya maji vijijini imekamilika inayohudumia watu milioni 31,652,000" uongo uliotukuka, *is a complete lie*, kila Mbunge hapa analalamika maji watu milioni 31 jamani over sixty percent ya wananchi ndani ya miaka ya tatu kweli tunajadili mambo ya namna hii? *A total lie.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo unaweza kuyakuta Tanzania tu lakini muangalieni mwenzenu Mheshimiwa Rais Kagame, Kagame *is a different man*, pamoja na matatizo yake mengine lakini nimeona ni mtu tofauti. Rais ana bodi ya ushauri ambayo inamshauri, hiyo ina vikao viwili tu, mwezi wa sita wanakaa Kigali, mwezi wa kumi wanakaa Washington, Marekani. Bodi yake allyounda kuna Rais Clinton, kuna kina Tony Blair kuna ma-CEO wa makampuni makubwa yote yanamshauri kuhusu uchumi wa Rwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mradi unatekelezwa Rwanda bila kupitia *level* tatu za utathmini, anaitwa *consultant number one*, anakuja namba mbili, anakwenda namba tatu akishauriwa Rais Kagame hapo arudi nyuma ndio mtu akipinga atapotea katika mazingira ya kutatanisha, sio mawazo tu ambayo mtu mmoja anaweza akatoa wazo likaanza kutekelezeka halafu tathmini baadae, *this is a nonsense*, hatuwezi kuendesha nchi katika huo mfumo. (Makofi/Kicheko)

Sasa leo tuna *SGR* (reli), Kenya wakati wanaanzisha *SGR* walihakikisha wanapanua bandari ya Mombasa, *that was they did Kenya*, leo una *SGRTanzania* bandari wanasema tunarekebisha gati *one* wakati mipango ya miaka yote tunapitisha ndani ya Bunge tumepitisha gati 13, gati 14 yamefutwa kwenye mpango sasa unategemea hii reli ikishakamilika fedha tunaturudisha vipi za miradi ya reli? Tumeshindwa kuiga Kenya wanavyofanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unasema mradi unaanza Disemba unakwenda mpaka Isaka sijui baada ya hapo unakwenda Makutupora wakati Rwanda mwenzako anakwambia Mradi wa *SGR* ataufadhili kwa kutumia *PPP*, wewe unasema nitaufadhili kwa kutumia fedha za ndani yaani unakuja kugundua yaani sijui tuna watu wa namna gani kwenye nchi yaani tuna watu *they can not think* unaweza kuwa *Ph.D holder you can be a Professor* lakini *real life* inakuwa *determined na uwezo na capacity* namna ambavyo mtu anavyoweza kutekeleza na kusikiliza. Kwa hiyo, mimi niliona nilisemee hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ukiifananisha na Rwanda ni vitu viwili tofauti *strategically* sisi tumezungukwa na nchi karibu tisa ambao hizi zote zinategemea Tanzania. Nchi ya Rwanda hawana rasilimali mtu atajenga hoja wanaiba Congo, lakini si kweli mtu anasema Rwanda ni kanchi kadogo si kweli mtu atakuja anahoja Rwanda kuna *vision*, Rwanda kuna *commitment* watu wako tayari kutumikia Taifa lao Tanzania hakuna *commitment* iko labda kwa mtu mmoja tu *the rest* ni blaa blaa tu kudanganya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali inapokuja mwishoni ije na mpango, itueleze hapa namna gani tunaweza tukakusanya triliuni 22 ili tuweze *ku-finance* mpango, lakini ukiangalia hapa nilikuwa naangalia vilevile kwenye huo ukurasa uliokuwa unafuatia namna ambavyo mkakati wao hamna mkakati tutaimarisha *TRA* kwa kukusanya kodi yaani ni kile kile waje watuambie namna gani sasa tutapata fedha kwenye vyanzo vya uhakika ili nchi iweze kufaidika. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Silinde tunaendelea na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete baadae Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia juu ya hoja iliyowekwa mbele yenu na Mheshimiwa Waziri

wa Fedha na Mipango kuhusu mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoendelea kufanya mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Kazi kubwa inafanyika lakini kweli kwamba katika mambo yote ya kufanya kazi changamoto hazikosekani, hata sisi wenyewe kule majimboni tunafanya kazi nzuri lakini bado changamoto zimeendelea kuwepo. Mimi naamini kwamba tukipeana muda tukapeana mawazo yaliyo sahihi tutafika katika malengo makubwa tunayoyataka.

Mheshimiwa Waziri katika kitabu chako cha hotuba yako ya juu ya mipango yako mambo ya msingi ambayo mimi nimeyaona na ninataka niyagusie hapa, lakini katika eneo litakuwa ni kuongeza juu ya yale mambo mazuri ambayo mmeyasemea nataka nianze na jambo la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la kilimo nimeona kwamba shughuli kubwa inayofanyika ya kujenga maghala, lakini Mheshimiwa Waziri ni ukweli kabisa kwamba bado sijaona ile nia ya dhati kabisa Serikali yetu kukifanya kilimo chetu kikawa cha kibiashara. Nimeona maeneo mengi mmezungumza lakini mimi nataka nizungumzie hasa katika kilimo cha mpunga.

Mheshimiwa Waziri kama unakumbuka vizuri wakati wa hotuba ya bajeti tulichangia na kueleza kwa wazi kabisa juu ya ambavyo mabonde yetu makubwa Tanzania kwa mfano kama lile la Ruvu pale linavyoweza kuwa chanzo kizuri cha kuzalisha chakula cha kutosha lakini katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri nimeona mmezungumzia sana jambo la eneo la Kilombero kwa maana ya bonde lile la Morogoro, lakini Mheshimiwa Waziri kiukweli kabisa Tanzania inayo mabonde mengi sana ambayo kama yatatumika vizuri kilio cha watu kulia njaa kukosekana kwa chakula kitakwisha kabisa na hata itaweza kufika sehemu kwamba tuna uwezo wa ku-*supply* chakula kwa nchi za nje na kuuza kwa ajili ya kupata fedha za kigeni.

Sasa Mheshimiwa Waziri nikuombe utakaposimama utuambie juu ya mpango mkakati mlionao wa kuendelea kutumia mabonde haya kwa ajili ya faida ya Watanzania hasa hasa mimi nazungumzia hapa Bonde la Ruvu ambalo tunalo kwa sisi wenyeji wa Pwani hasa maeneo ya Chalinze na Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo Mheshimiwa Waziri nikupongeze, nimeona katika taarifa nilizozisoma juu ya benki yetu ya kilimo jinsi ambavyo imeweza kuwasaidia *AMCOS* zinazolima pamba kwa kutoa vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.5 kusaidia kuweza kuvuna pamba na kuiweka katika maeneo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikuombe sana kwamba kilimo kipo cha namna nyngi lakini pesa hizi naamini kwamba zipo na mahitaji ni makubwa sana. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri muendelee kuangalia maeneo mengineyo pia, kilimo sio pamba tu peke yake, tunacho kilimo cha korosho, kahawa, alizeti na mazao mengineyo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameeleza hapa kama walivyotangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia Mheshimiwa Waziri nimtoe wasiwasi ndugu yangu Mbunge wa Sumve amezungumzia juu ya pamba kukosa maeneo na kwamba pamba nyngi inasafirishwa nje. Sasa hivi pale Chalinze tunajenga kiwanda kikubwa sana ambacho kinakuja kutengeneza vitambaa na *material* zote zinazotokana na pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana aende akawahamashe wananchi wake wa Sumve na maeneo yote ya wakulima wa pamba kwamba sasa pamba ile itakuwa haifiki Dar es Salaam bandarini isipokuwa itakuwa inaishia Chalinze pale kwa ajili ya kuchakatwa na kutengenezwa *material* ambazo zinakwenda kuwa sehemu kubwa ya kutatua tatizo kubwa la kupatikana kwa vitambaa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo, nizungumzie kidogo katika eneo la mifugo. Nimeona kazi kubwa na nzuri sana ambayo inafanywa na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na wizara yake kwa ujumla lakini bado tumekuwa na tatizo kubwa sana la kuchunga au kugeuza nchi nzima kuwa ni sehemu ya machungio. Mheshimiwa Waziri kiukweli kabisa nyama nzuri haiwezi kupatikana kwa ng'ombe kutembea kutoka Sumve huko Mwanza mpaka Chalinze. Ng'ombe mwenye nyama nzuri anapatikana kwa kutunzwa, kulishwa vizuri na matunzo yakawa yenyе kutengeneza ubora huo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nimeona hapa mmezungumza jinsi ambavyo mnataka kuhakikisha kwamba ng'ombe wetu wanakuwa wana uwezo wa kuzalisha maziwa yenyе ubora zaidi. Mheshimiwa Waziri nataka nikukumbushe kama vyombo havitosimamia ile Sheria ya Usafirishaji wa Mifugo kilio hiki na matatizo haya yataendelea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana wewe na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, namuona ndugu yangu, Mwenyekiti wangu Bwana Ulega anafanya kazi nzuri sana lakini kama hatutoweza kusimamia sheria hizi hatuwezi kupata nyama iliyo bora au maziwa yaliyo bora. Itaishia kila siku ng'ombe ambao unatarajia watoe lita 12 mpaka 14 watakuwa wanatoa lita mbili au lita moja kwa sababu ya kuchoka kwa kutembea umbali mrefu na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo nizungumzie pia jambo la afya, ni kweli kwamba fedha nyingi sana zinapelekwa katika afya. Mimi binafsi nawashukuru sana mmeendelea kutuangalia watu wa Chalinze kwa jicho la huruma zaidi, kituo changu cha afya cha Kibindu sasa kinakamilika na Lugoba kule mambo ni mazuri zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia wameeleza waliotangulia juu ya ufinyu wa watoa huduma

za afya. Mimi nikuombe sana hili jambo ni jambo *sensitive* sana, tunaweza tukawa na majengo mazuri sana lakini kama majengo yale hayafanani na huduma zinazotolewa itakuwa ni jambo ambalo kwa kweli mwisho wa siku wananchi hawatotuelewa. Nikuombe sana tuendelee kuliangalia jambo hili na kulipa kipaumbele chake kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nikushauri Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali yangu katika eneo la bima ya afya. Sasa hivi kwa bima kubwa kabisa kwa mfano tunalipa shilingi 1,500,000, hii shilingi 1,500,000 kwa mwananchi wangu anayetoka kule Talawanda kusema kwamba akalipe kwa kweli ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kama tutaaamua kuja na mkakati wa kuwawezesha wananchi kulipa kiwango hiki cha shilingi 1,500,000 ambacho kinatakiwa kulipwa kwa mwaka kikalipwa katika *installments* za kila mwezi. Kwa maana sasa kwa kila mwezi mwananchi akawa analipa *at least* shilingi 125,000. Hili jambo wanaliweza na wananchi pia wapo tayari kufanya hivyo. Leo hii unaweza kukuta mama ana tatizo labda ana uvimbe tumboni, anatakiwa alipe shilingi 3,000,000 ili aweze kupata matibabu, lakini mtu huyu kama angeweza kulipa shilingi 1,500,000 maana yake angeweza kupata matibabu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukaja na mkakati mzuri ambao unaweza ukasaidia kupunguza matatizo na machungu kwa wananchi wanyonge ambao tuliwaahidi kwamba tutaendelea kuwaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo limetokea jana Mheshimiwa Waziri hasa Waziri wa Afya nikupe tu taarifa kwamba Kituo chetu cha Afya cha Msata kimepata nyota nne na kimekuwa cha kwanza Mkoa wa Pwani kwa ubora. Haya ni mambo ambayo yanaendelea kufanyika katika Halmashauri ya Chalinze na sisi tunaendelea kusimamia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee kabisa niwashukuru sana wenzangu ambao wanafanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba mambo haya yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la viwanda kwa kipekee kabisa nimpongeze sana Mkuu wangu wa mkoa *Engineer Evarist Ndiyilo* kwa jinsi ambavyo anaendelea kufanya kazi kubwa ya kusimamia kuhakikisha mapinduzi ya viwanda kwa Chalinze yanakuwa ni kweli lakini kwa Mkoa wa Pwani kwa ujumla wake.

Ninachokuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha muendelee kuhakikisha kwamba yale maeneo tengefu ambayo tumeyatenga mnayapelekea fedha ili zile fidia ambazo zimeahidiwa kulipwa wananchi zilipwe, lakini pia yale maeneo ambayo tumetenga kwa ajili ya viwanda nayo pia mnaendelea kuweka msisitizo na msukumo kuhakikisha kwamba viwanda vile vinakamilika mapema iwezekanavyo na Serikali iweze kufikia malengo yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la *Hydro-Electric Power Rufiji*; Mheshimiwa Waziri nikuhakikishie wananchi wa Chalinze wanasubiri kwa hamu kubwa sana mradi huu wa umeme. Mradi huu wa umeme unakuja kutatua kero ambayo sasa tumeanza kuipata ndani ya Chalinze, umeme hauji vizuri kwa sababu wananchi wanagawana umeme na viwanda. Viwanda vimekuwa vingi, Serikali yetu imesisitiza juu ya viwanda na sisi Chalinze tunatimiza kwa vitendo, lakini kwa kweli adha hii inayoanza leo tunaogopa isijekuwa ngumu halafu baadaye wananchi wakaja kuuliza kwamba sasa viwanda hivi mlivileta ili vitusaidie nini kama sio kuja kutuongeza tabu katika maisha yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pamoja na...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, nimekuongezea sekunde kadhaa.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru na naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza mawazo mazuri yaliyotanguliwa na Wabunge wenzangu hasa wa Chama cha Mapinduzi kwa kuwa wamedhamiria kuweza kuunga mkono na kumtia moyo Rais na jemedari wetu mzalendo namba moja Dkt. John Joseph Pombe Magufulsi kwa kazi nzuri anayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote na vilevile pongezi za pekee ziende kwako wewe Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuwa wewe umekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba Mheshimiwa Rais anakwenda kufanya na kutimiza yale alioahidi, aliwaambia Watanzania alipokuwa akiomba kura mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona katika mpango Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kutekeleza yale ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi katika llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015. Nina furaha kuona kwamba katika bajeti ya elimu ni kwa jinsi gani ambavyo Serikali ya Awamu ya Tano na hasa ilivyojidhatiti katika kuhakikisha kwamba elimu ni bure, tumeona kwa jinsi ambavyo hivi sasa idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa katika shule za msingi na sekondari imeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii pia imewawezesha hata wale wanafunzi ambao kwa namna moja au nyingine hawakuweza kupata elimu wazazi wao hivi sasa wamepata ahueni ya kuwaandikisha watoto wao na ndio maana leo hii tunajivunia kwa kuona kwamba idadi kubwa imeongezeka, pongezi za dhati kabisa kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi na mpaka kufikia hivi sasa kwa mujibu wa taarifa ya jana inaonesha kwamba ni bilioni 20.9 ambazo zinatolewa kwa kila mwezi. Utaona kwamba hizi kwa mwaka mzima zinakwenda bilioni 250.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mapendekezo ya mpango tumeona kwamba kuhusiana na suala zima la umeme wa *REA* ni kwa jinsi gani ambavyo Serikali imeweka nguvu kuhakikisha kwamba wananchi na hasa wa maeneo ya vijijini kuelekea uchumi wa kati wanapata umeme. Tunafahamu umeme na hivi sasa katika suala zima la viwanda umeme unahitajika sana. Jumla ya vijiji 557 tumeona kwamba hivi sasa tayari vimekwishapata umeme huu wa *REA* na hii itawawezesha wananchi waweze kujikita katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni jitihada nzuri za Mheshimiwa Rais wetu ambaye anawapenda na anawapigania wananchi wake kuhakikisha kwamba anatutoa hapa tulipo na kufika katika uchumi wa kati mwaka 2025. Hili ni jambo la kujivunia na nawapongeza tu Mawaziri na Waziri mwenye dhamana ya umeme basi endeleva jitihada hizo na sisi tunakuunga mkono tupo nyuma yako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika mabadiliko ya Sheria za Madini tumeona ni kwa jinsi gani zimeongeza pato na hasa katika ujenzi wa ukuta kule Mererani. Kwa mujibu wa taarifa tumeona kwamba hapa ukuta huu ambao una kilometra 24.5 mapato yameongezeka toka bilioni 194.4 kwa mwaka 2015 na kuendelea lakini hadi mwaka 2018 sasa hivi ni bilioni 301.2. hizi ni jitihada njema kabisa za Serikali ya Awamu ya Tano katika kuhakikisha kwamba madini yanawafaidisha wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema tu kwamba nimpongeze pia hata katika Bunge la Afrika nilimuona mmoja wa Wabunge kwa kweli Mheshimiwa Silinde nikupongeze umeona jitihada hizi na ukapongeza kwamba kazi nzuri inayofanywa na Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa mabadiliko ya sheria zilioletwa hapa Bungeni zimeweza na ukawataka pia Wabunge kutoka Mabunge mengine ya Afrika nao waige mfano kwa Rais wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Hii ilikuwa ni jitihada na *credit* nzuri kwa nchi yetu na hongera sana kwa huo uzalendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona ni kwa jinsi gani katika vituo vya afya vimeboreshwa, wananchi wengi maeneo mengi walikuwa hawapati huduma ya afya. Mimi naamini kabisa kwamba jitihada hizi zitakwenda kupunguza vifo vya wanawake na watoto, lakini vilevile wananchi wengi watapata huduma hii kutokana na vituo hivi vinavyojengwa maeneo mengi hakukuwa na hivyo vituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa Rais kuhakikisha kwamba tunatumia nguvukazi ya wananchi, vituo hivi vimejengwa katika ubora na vilevile gharama zake zimeweza kupatikana yale majengo yote yaliyotakiwa. Naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa jitihada hizi kuhakikisha kwamba wananchi wake kwa sababu ili tuwe na uchumi ulio imara tuweze kuzalisha mali tunahitaji afya na kwa wananchi wakipata afya basi uzalishaji mali utaongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kwamba kutokana na jitihada hizi na vilevile kwamba wenzetu wanasesma Serikali imewekeza sana katika vitu, ni kweli tunawekeza katika vitu kwa mfano barabara ili tuwawezeshe wananchi waweze kufika kutoka eneo moja na lingine. Vilevile wananchi hawa wataweza kusafirisha biashara zao na kusafiri wao wenyewe tofauti na hapo awali ilivyokuwa na ndio maana leo hii ukitoka Arusha mpaka Tunduma kwenda

mpakani mwa Zambia na Tanzania ni barabara ya lami kutokana na jitihada nzuri za Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, tunaona kwamba katika suala zima la kilimo kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu jitihada zinavyofanyika hivi sasa ambapo amekuja na mipango/mikakati ya kuhakikisha kwamba wanawawezesha vijana katika kilimo. Wao wamedhamiria kwa dhati kabisa kuhakikisha kwamba tunaingia katika kilimo cha vitalu (*green house*). Huu ni mpango mzuri na jitihada zinazofanywa na Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu ili vijana waweze kujilingiza kwenye kilimo na siyo kwa kufanya hivyo tu. Serikali yenye we inawawezesha vijana hawa kwa kupitia mikopo mbalimbali ili waweze kujipanua zaidi katika suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari njema ni kwamba na masoko pia tayari kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu wamekwishaanza kuwatafutia vijana hawa. Kwa hiyo, napongeza sana jitihada hizi kupitia kwa Waziri Mkuu, kupitia kwa dada yetu Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu wako kutokana na kazi nzuri mnayofanya. Nina imani kubwa kabisa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile vikundi vyatujasiriamali vimeweweleshwa na siyo hao tu, nina furahi sana kupitia sheria ya 442 ambayo itawawezesha makundi ya wanawake, vijana na watu wenyewe ulemavu kupata mikopo na tayari baadhi ya Halmashauri zimekwishaanza kutekeleza hili, hii itatusaidia pia kupunguza umaskini. Pia itatusaidia kupunguza ile hali ya kuwa tegemezi na yote haya ni kutokana na mipango mikakati mizuri iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanasema hakuna usalama, nchi hii ni mionganini mwa nchi ambazo zinaongoza kwa amani. Wenzetu walipo nchi jirani wanajivunia Tanzania na kuitolea mifano, ndugu zangu tuendeleze amani tuliyonayo na amani hii ndiyo itakayotuwezesha kufika katika

uchumi wa kati mwaka 2025. Kwa maana hiyo kwamba kukiwa na amani watanzania wataweza kwenda kufanya shughuli zao mbalimbali za ujasiriamali lakini vilevile kwenye kilimo na shughuli zingine ambazo zitawawezesha wao kuongeza kipato chao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kutokana jitihada nzuri za Mheshimiwa Rais wetu mzalendo namba moja, Rais ambaye katika dunia hii wanamtolea mfano na waswahili wanasema kwamba kwenye miti, hapana wajenzi. Mimi nasema kwamba wajenzi ni sisi wenyeewe na ni kutokana na Rais huyo basi atatufikisha katika uchumi tunaoutarajia kufikia uchumi wa kati mwaka 2025. Tumuombee Rais wetu na tumuunge mkono ambaye ameruhusu wajasiriamali waweze kuingia maeneo mbalimbali kujipatia kipato. Hivi sasa hata wizi umepungua kutokana na vijana wengi wanajishughulisha katika shughuli za kujilletea vipato. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wabunge wenzangu tuendeleee kuungana na Mawaziri na kumuunga mkono Rais wetu kuhakikisha kwamba yale aliyoyaahidi mwaka 2015 anayafanya kazi na kuyatimiza. Jambo la muhimu ni kuona kwamba ni kwa jinsi gani amedhamiria miradi mikubwa ya umeme kwa mfano *Stiegler's Gorge* na mradi wa reli ambao tayari umekwishaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ssa katika Jiji la Dar es Salaam hata foleni zimepungua kutokana na miundombinu inayojengwa na kwa mfano daraja la *TAZARA*. Hizi ni jitihada zinazoonyeshwa na Rais wetu kwa kipindi kifupi, tunatarajia kwamba kwa miaka mitano itakayokuja kutakuwa na mafanikio makubwa zaidi na endapo tutaendelea kumuunga mkono. Mungu akupe maisha marefu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, tunakupenda, tunakuhitaji sana na tunaona kwamba wewe umedhamiria kuwakwamua wananchi wako na una dhamira ya dhati kabisa katika kuhakikisha kwamba unatutoa hapa tulipo kufika katika uchumi wa kati. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, ahsante sana kwa mchango wako.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge kabla ya kusitisha shughuli za Bunge tuna tangazo moja hapa, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba leo Jumatano tarehe 7 Novemba, 2018 saa 7:00 mchana mara baada ya kusitishwa shughuli za Bunge kutakuwa na uzinduzi wa Mkakati wa Bunge wa Masuala ya Jinsia katika Ukumbi wa Msekwa, mgeni rasmi katika shughuli hiyo atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kushiriki bila kukosa. (*Makofii*)

Pia kabla sijamaliza shughuli za leo naomba niwataje kabisa wajumbe ambao wataanza kuchangia jioni ili wajiandae. Tutaanza na Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Joram Hongoli na Mheshimiwa Rashid Akbar na wengine watafuata.

Waheshimiwa nawashukuru sana kwa kazi nzima ya leo asubuhi, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11:00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## **KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:  
HOJA ZA SERIKALI**

**Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa  
Kutekelezwa na Serikali pamoja na Muongozo wa  
Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa  
Fedha 2019/2020**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na mjadala wetu, tunaanza na Mheshimiwa Hasna Mwilima, atafuatia Mheshimiwa Oran Njeza na baadae Mheshimiwa Joram Hongoli ajiandae.

Mheshimiwa Mwilima hayupo, Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu ili na mimi niweze kuchangia na kutoa maoni kwenye Mpango wetu wa Maendeleo kwa mwaka kesho 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri na timu yake yote. Kwa kweli huu mpango ni mzuri sana, umeangalia vipaumbele vyote muhimu na umetengenezwa kitaalam sana kiasi ambacho hata ukiangalia na maoni ya Kamati nayo yamefanya kazi nzuri sana, yameuchambua vizuri na maoni yake yote naomba niyachukue na mimi labda niongezee pale tu ambapo hayakugusa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika huu mpango wetu ukiangalia vilevile unaangalia tulikotokea, tumefanya nini katika miundombinu, katika kilimo, uvuvi, elimu na

kadhalika. Na ukiangalia mwenendo *trend* inaonesha tumefanya vizuri katika sehemu nyingi, zinaridhisha. Na kwa kujikumbusha tu kwamba bajeti haina maana ya kwamba umepewa *license* ya kutumia, hapana, ni matarajio, ni mategemeo. Kwa hiyo, kwa kiasi pale ambapo tumefanya vizuri mimi nilikuwa namuomba Waziri aangalie ni namna gani tuweze kuboresha huko nyuma wakati tunaangalia na mipango ya vipaumbele vya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukifanya vizuri sana katika uboreshaji wa bandari, ununuzi wa ndege na ujenzi wa reli. Tumefanya vizuri katika hayo maeneo, lakini mimi naomba tu napendekeze, kwa sababu kwa Bandari yetu ya Dar es Salaam tu sasa hivi ina ushindani mkubwa sana kutoka kwa majirani zetu, ukanda wa kusini, nchi kama Angola, Namibia na Msumbiji. Hizo nchi zimelilenga soko letu na zimelilenga soko la Bandari ya Dar es Salaam. Sasa je, sisi tumejipanga vipi kupambana na hilo? Kwa sababu huwezi kuzuia watu wasikuingilie kwenye soko lako, wewe ndio unatakiwa ujipange namna ya kuijimarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maboresho niliyokuwa napendekeza mimi kwa sababu hili soko bado tunalihitaji sana pamoa na utengenezaji na ujenzi wa *standard gauge* lakini soko la nchi za DRC, Zambia na Malawi ni soko muhimu sana kwa Bandari yetu ya Dar es Salaam na kwa uchumi wa nchi yetu. Sasa wenzetu wamefanya nini, wamejenga reli ya kutoka *Lobito Port*, Angola kuja kwenye nchi za DRC na wanazipeleka mpaka kwenye machimbo, reli ambazo ni za kisasa ni *standard gauge* ambazo zinaweza kuchukua mzigو mkubwa sana na hizo reli vilevile zinalenga kuziunganisha Bandari za Msumbuji lakini na kwa kiasi fulani wanalenga vilevile na kuiunganisha na Bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa angalia nia yao nini hawa; wamepunguza gharama zao kwa kiasi kikubwa, gharama zimekuwa ndogo kiasi wafanyabiashara wote sasa hivi wanaangalia ni namna gani watumie Bandari ya Lobito ambayo ni kilometra 1,300 tu kutoka DRC ukilinganisha na sisi zinakaribia karibu kilometra 2,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya kwangu kwenye mpango wa mwaka kesho, Serikali ilikuwa inafikiria kujenga bandari kavu Mbeya na hiyo bandari kavu ni muhimu kwa vile imekaa mahali kwa kimkakati ambapo inaliangalia soko la Malawi, soko la Zambia na soko la Kongo, lakini kwa miaka miwili sasa hivi Mamlaka ya Bandari haijaruhusiwa kuwalipa fidia wananchi waliota maeneo yao kwa ajili ya kujenga bandari kavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wenzetu malengo yao ni kujenga bandari kavu nyangi kwenye nchi za Namibia – kuna sehemu inaitwa *Walvis Bay*, Namibia, lakini vilevile na Angola nako wanajenga bandari kavu, ukija Msumbiji nao wamejiimarisha, nao wamejenga reli kutoka kwenye bandari ambayo ni kubwa namba mbili kwa Msumbiji inaitwa Nacala, wamejenga hiyo bandari mpaka nchi ya Malawi na sasa hivi wanalenga kuingia Zambia na wakiishaingia Zambia wanalenga vilevile iende mpaka DRC, sasa ukiangalia sisi tutabaki na nini tusipokwenda kishindani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba katika huu mpango nimeona kwamba kuna jitihada za kuboresha *TAZARA* ambazo ni jitihada nzuri, zitasaidia, lakini mkazo uwe hapo; hatutatumia pesa nyangi sana lakini ukiweza kwenda pamoja ku-*improve* ile mipango ambayo wameshaitekeleza inasaidia vilevile hata kutekeleza mipango inayokuja ya mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la umeme tumefanya vizuri sana, *REA* inakwenda vizuri na pesa nyangi ambazo kwa kiasi kikubwa ni za ndani zimefanya kazi nzuri sana. Sasa je, katika mpango wetu tutaboresha vipi hii mipango ya umeme vijijini iwe endelevu? Sasa huioni moja kwa moja kama iko kwenye hii mipango kwa sababu bila hivyo kama hakutakuwa na mipango ya kuifanya hii mipango yetu utekelezaji wetu unakuwa endelevu tutakuwa tunapoteza hela bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia kwa hizi pesa nyingi tulizotumia, je, zimeigia katika Mfuko wa *TANESCO* kama *capital*? Na kama imeingia *capital* mbona inaonekana ni hela nyingi sana, je, zinaisadia vipi *TANESCO* kupata faida?

Sasa wakati Waziri anaangalia namna ya kuboresha mapato ya ndani aangalie ni namna gani wakati hizi pesa nyingi tunaweza kwa wakati mwagine tunasahau kwamba pesa zote ambazo tumezitumia kwenye ujenzi wa umeme vijiji (REA) zimehamishiwa *TANESCO* kama kuziongezea mtaji, je, ule mtaji unatuzalishia kiasi gani? Je, tunaiona hiyo? Ukiangalia vijiji vingi sana sasa hivi vimeongeza wateja kwa *TANESCO*, je, tuione wapi hiyo faida ya *investments* ambazo tumeziweka kwenye umeme? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye maji villeville pesa nyingi sana tumezitenga kwa ajili ya miradi ya maji lakini ukirudi nyuma kuangalia ufanisi wa miradi ya maji huwezi kuiona kwa sababu nayo hatukuiwekea mipango endelevu ya hii miradi ya maji.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Oran Njeza muda wako umeisha.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joram Hongoli baadae Mheshimiwa Rashid Akbar ajiandae.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia huu mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kuipongeza Serikali, kumpongeza Mheshimiwa Rais mwenyewe kwa namna anavyofanya, kwa namna alivyoanza kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi. Wamesema hapa kwamba tayari

Rais ameweza kuhakikisha kwamba mipango ya ununuzi wa ndege imekamilika na inaendelea vizuri, barabara za lami zinaendelea kutengenezwa lakini pia reli inaendelea kujengwa, reli ya kisasa kabisa ambayo ni *standard gauge*, lakini pia ujenzi wa meli katika maziwa makubwa nao unaendelea na mipango mingine mingi mizuri inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa namna anavyoismamia vizuri hii Wizara ya Fedha na Mipango, kweli anaitendea haki anaisimamia vizuri sana. Nimpongeze pia Naibu Waziri wake, anafanya kazi nzuri, tuombe Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki waendelee kufanya kazi na hatimaye sisi Watanzania tuweze kupata maendeleo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nichangie kidogo kwenye kilimo; Sekta ya Kilimo kwa sehemu kubwa Tanzania ndiyo inayotegemewa zaidi. Zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanajihuisha na kilimo cha mazao mbalimbali, lakini pia kuna zao hili la mahindi ambalo sehemu kubwa, karibu nchi nzima tunalima, lakini pia mikoa sita ya Nyanda za Juu Kusini; Mbeya, Rukwa, Katavi, Ruvuma, Songwe na Njombe ndiyo wanaolima sana haya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukienda kwenye mikoa hii mahindi ya mwaka jana yamejaa kwenye nyumba na mwaka huu yamejaa, wakulima hawajui wafanye nini na wakati huo huo msimu wa kilimo umeshaanza lakini hawajauza mazao yale na mbolea inauzwa bei juu, kwa hiyo sasa hatujui namna gani Serikali itatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombi Serikali, ili tusiweze kuwa na hali kama hii huko mbeleni tujitahidi kuwa na kitengo maalum ambacho kitahusika sanasana na utafiti wa masoko ya mazao yote ya kilimo kwa maana ya mazao ya biashara na yale ya chakula, kuwe na kitengo hicho ambacho kitazunguka nchi nzima na kufanya utafiti ni wapi zao lipi litauzwa ili tuondoe hii adha kubwa ambayo wakulima wanalima halafu mwisho wa siku haya mazao yanabaki bila kupata soko na mwisho wa siku inakuwa ni hasara kubwa kwa wakulima na pato la Taifa linapungua

kwa sababu tunakuwa tumezalisha kitu ambacho hakiwezi kuuzwa kinabaki tu kwa ajili ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana hiki kitengo kitatusaidia kuhakikisha kwamba mazao yote yanapata masoko huko duniani kwa sababu sasa hivi tuna masoko pale DRC, wanahitaji mahindi, Kenya wanahitaji mahindi, sasa sijajua kuna tatizo gani kwa nini mahindi hayaendi huko DRC au hapo Kenya ambapo wana shida ya chakula. Kwa hiyo, tufanye hivyo, tuanzishe kitengo maalum ambacho kitafanya utafiti wa masoko hasa masoko haya ya mazao ambayo tunazalisha hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo lingine juu ya Mradi wa Mchuchuma na Liganga, ule wa makaa ya mawe na chuma. Huu mradi ni wa muda mrefu na umesemwa muda mrefu sana kwenye vitabu toka mwaka 2016 tulivyoingia Bungeni lakini mpaka sasa bado haujaanza, taarifa zinaonesha kwamba bado mazungumzo yanaendelea. Sasa tunaomba kujua ni lini mazungumzo haya yataisha? Kwa sababu huu mradi ni muhimu; kwanza unakwenda kuzalisha chuma ambacho kitasaidia kutoa *raw material*/kwenye viwanda vyetu. Lakini pili utazalisha umeme ambaao utasaidia sasa, utawezesha hata viwanda vidogo vidogo viweze kufunguliwa kwa sababu kutakuwa kunawaka umeme na utakuwa wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe Serikali mchakato huu wa mazungumzo ni vizuri uwahi basi ili angalau huu Mradi mkubwa wa Mchuchuma wa makaa ya mawe na chuma uweze kuanza ili mwisho wa siku tuweze kupata faida hizo na pia tufungue fursa za vijana kupata ajira kwenye maeneo hayo ambako chuma kitazalishwa, lakini pia kutakuwa na makaa ya mawe, lakini kwa maeneo hayo pia na viwanda vingi vitaongezeka kwa sababu tuna *raw materials*sisi wenyelewe lakini pia tuna umeme wa kutosha nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme juu ya uvuvi, niipongeze Serikali, imeendelea vizuri lakini pia nipongeze

Wizara inaendelea kudhibiti uvuvi haramu, nawapongeza sana mnafanya kazi kubwa maana tukiacha samaki wakapotea itakuwa ni mbaya, lazima tuwe na samaki waendelee kuzaliana na tuendelee kuuza na nipongeze kwamba tayari Serikali imeanza mpango wa kujenga bandari ya uvuvi, nipongeze sana, tunataka twende kwenye uvuvi, siyo tu ule wa mwaloni, siyo tu ule uvuvi wa *territorial*, twende sasa kwenye uvuvi wa ndani, twende kwenye *EEZ*, kwenye *Exclusive Economic Zone*, ndivyo nchi zilizoendelea zinavyofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake Nchi kwa mfano Korea Kusini, Mauritius lakini pia nchi kama Seychelles, wale wanafanya uvuvi wa ndani na kupitia uvuvi huo wanaingiza pato kubwa sana. Kwa hiyo mimi naamini kwamba tukianza sasa tukajenga hiyo bandari lakini pia tukanunua meli ya uvuvi tukaweza kuvua mpaka ndani ya bahari tutaweza kuinua uchumi wa nchi yetu kwa kasi kubwa sana. Kwa hiyo niombe sana jambo hili tulifanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nakumbuka Mheshimiwa Zungu, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, amekuwa akilisemea sana hili jambo. Kwa hiyo niombe Serikali yangu muweze kufanya kazi hili mapema ili angalau tuingie kwenye uvuvi ambao unaweza ukawa una manufaa kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme juu ya soko, hasa soko la zao la chai; kwa kweli sielewi kwa nini hatuleti ule mnada ambao unafanyika kule Kenya. Miaka mingi tumesema na wenzetu Wakenya wanafaidika sana kufanya mnada kule kwa hiyo sisi tunazalisha chai nyingi na ni wazalishaji wazuri na tunazalisha chai bora, kwa nini tunapeleka kuuza Kenya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inavyoonekana duniani inaonekana katika *East Africa* inayoongoza kuzalisha chai ni Kenya na chai ya Kenya ni bora, kumbe kwa sababu chai hiyo inauzwa Kenya. Kwa hiyo, niombe Serikali yangu, na

Waziri wa Fedha na Waziri wa Kilimo mpo hapa, mfanye utaratibu wa kuhakikisha kwamba mnada wa chai ufanyike hapa hapa nchini. Ukifanyika hapa nina uhakika tutapata bei nzuri kuliko ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kilo inauzwa shilingi 314, ni hela ndogo sana, lakini ikiuzwa hapa, mnada ukawa hapahapa nchini naamini hata zile kodi nydingine, kodi pengine za soko zile, zitabakia hapa hapa nchini. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali yangu tujitahidi tuhakikishe kwamba soko au mnada wa chai unahamia Tanzania haraka iwezekanavyo ili faida zinazotokana na kuwepo na huo mnada tuweze sisi Watanzania kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyokwenda kuuza Kenya wanaofaidika ni Wakenya na sasa hivi karibia viwanda vyote wanachukua Wakenya. Sasa lazima tujulize kwa nini wanachukua Wakenya hivi viwanda? Inawezekana pengine agenda ni hiyo kwamba tuendelee kuuza hiyo chai ule mnada uendelee kufanyika kule Kenya. Kwa hiyo niombe sana Serikali yangu, mimi naamini ni Serikali sikivu mtayafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya niunge mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hongoli. Tunaendelea na Mheshimiwa Ajali Akbar na baadae Mheshimiwa Albert Obama ajiandae.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kunipa nafasi ili nitoe mchango kwa mpango huu ambao ndugu yangu, Mheshimiwa Dkt. Mpango, anaufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumsifu Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha, kwa mipango yake, yeye ni mtaalam sana katika kuandaa mipango hasa ya kukusanya kodi. Ila tatizo la Mheshimiwa Dkt. Mpango ambalo mimi huwa naliona siku zote ni kwamba

hafanyi *coordination* kati ya mpango mmoja kwa maana ya kwamba kushirikisha wale watu ambao wanazalisha, kwa mfano kushindanisha watu wa kilimo, watu wa uchumi na watu wa viwanda na kilimo kinaingiaje, yaani hao mahusiano hao watu anawezaje kuwaweke pamoja wakahusiana. Maana yake akishafanya *coordination* kati ya hivi vitu vyote basi Mheshimiwa Dkt. Mpango atakuwa mzuri sana katika bajeti. Kwa hiyo mimi naomba Mheshimiwa Dkt. Mpango nimshauri kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mpango, kabla ya uhuru au baada ya uhuru mwaka 1961 na baada ya uhuru, Mheshimiwa Rais wetu mstaafu ambaye ni hayati sasa hivi, Baba wa Taifa alikuwa na Jeshi maalum ambalo baada ya kupata uhuru aliona kwamba nchi hii haiwezi kujiongoza peke yake mpaka nchi yote ya Afrika iwe huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo baada ya kuona kwamba nchi yoyote haiwezi kuwa huru baada ya kuwa wameungana na Zanzibar kitu kilichofuata pale, Mheshimiwa Rais au Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichofanya ni kuhakikisha Jeshi letu linakuwa Jeshi la Ukombozi la Afrika na Jeshi letu lilikuwa limepelekwa kila sehemu katika Afrika kwenda kufanya *participation* katika kuhakikisha kwamba zile nchi nyingine zinakuwa huru. Zile nchi huru zote leo zimekuwa huru lakini leo tulitarajia kwamba kwa kuwa kulitumia fedha zetu nyingi sana kwa kuweka makambi hapa nchini kwetu na sisi wenyewe tukabaki nyuma ndiyo hao hao ambao wametufikisha leo Tanzania tumekuwa nyuma wenzetu wamekuwa mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini kifanyike Mheshimiwa Mpango ni *coordination* ile ile kama jeshi letu wakati ule lilikuwa la kupigania uhuru, sasa hivi jeshi letu liwe ni jeshi la kiuchumi, tutengeneze jeshi wakati ule wakati tulikuwa na watu milioni tisa leo tupo watu milioni 50, tuna rasilimali watu ambao ni wengi sana ambao tukitengeneza jeshi wale ambao tumeshawatafutia uhuru na bado wanaendelea kupigana kama ndugu wanashindwa

kujiongoza sisi tunaenda kuwauliza eeh, bwana mmeshindwa kuelewana kujitawala si ndiyo, tunamgonga mmoja halafu wanatulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ndivyo jeshi la kisasa liliyvo duniani kote yaani tuwe na nguvu tuwe na jeshi lenye nguvu kama watu wanapigana na tuliwasaidia kukomboa uhuru wao mbona hawakuturudishia hizo gharama tutapataje. Kwa hiyo, maana yake kwa kuwa masuala ya ulinzi mara nyingi hatuwezi kuyazungumza wazi. Niombe Kamati ya Ulinzi na Usalama ifanye *coordination* na Bwana Mpango tuangalie namna gani tunaweza tukatumia jeshi letu kulishirikisha kwa wale watu wanaofanya fujo wakati tuliwasaidia kukomboa uhuru ili tunaona kwamba wanashiriki vipi kutulipa zile gharama kama wao wataendelea na ugomvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo mchango kwa upande wa *participation* kuangalia kuona nini jeshi linashiriki kiuchumi duniani kote na ndiyo maana jeshi watu wanalitumia kiuchumi kama ninyi tumewakomboa na bado mnaendelea kupigana siyo tunakwenda tunakuja hapa kila siku kuja kuwasuluhisha bila kutulipa haiwezekani kama unazalisha mafuta haya tupe meli 200 hapa halafu sisi tunaondoka zetu itakuwa ni moja ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine Mheshimiwa Mpango ambalo nataka nikushauri ni kwamba leo umeanzisha mradi wa kimkakati uwe na miradi ya kimkakati kwa mfano ile ambayo umesema kwamba kutakuwa na reli, reli kuanzia Mtwara kwenda hadi Mbambabay ule ni mradi wa kimkakati kwa sababu pamoja na mazao ya kilimo ambayo yatakuwa yanapita, lakini kule unakokwenda kunakuwa na makaa yale Liganga ambayo na kwenyewe kule kuna madini ambayo ni ya kimkakati ambayo yanaweza kutumika kwa ajili ya kuzalisha katika viwanda vingine. Maana yake hapo moja kwa moja hiyo miradi kama hiyo wewe unakuwa umeishirikisha kiuchumi kuliko kupeleka ile miradi ambayo inakuwa ikienda inakuwa moja kwa moja inakuwa ni mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Mpango ambalo mimi nataka kushauri nimeona jambo zuri sana wamefanya hawa watu wa Wizara na ambalo na wewe mwenyewe umeshiriki. Kuna *center for excellence* kwa mfano watu wa *excellence* kwa mfano hawa watu madini wamehakikisha kila kanda wanajenga mahala ambapo watu wenye fikra kuhusu utaalam wa madini unakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na sisi tufanye tunafanyaje sasa. Tunahakikisha kwamba yale mazao yote ya kilimo ya kimkakati yale tunaweka *center for excellence* kwa mfano hapa Dodoma tukiona kwamba watu wanalima zabibu, tunaangalia ile kwamba *center* wale Makutupora na wao wanalima zabibu ili tuweze kuuza katika viwanda vyetu, kama Singida wanalima alizeti tunahakikisha kwamba pale tunaweka *national service*.

Kwa hiyo, maana yake vijana wetu tutakuwa tumewaaajiri maana patakuwa na *center for excellence*, lakini wale watapata kuuza kwenye viwanda vyetu nya alizeti ambavyo vitakavyokuwepo Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda Pwani kuangalia je, Ukanda wetu wa Pwani una viwanda nya samaki, tunaweka vile tunaweka *camps* ambao tutahakikisha kwamba kutakuwa na uvuvi, lakini vilevile tutakuwa tunaweka viwanda ambavyo nya kuhakikisha kwamba vijana wetu wanakuwa wana *participation*. Kwa hiyo, maana yake Mikoa yote vijana wote watakuwa wanashirikishwa moja kwa moja kiuchumi na maana yake watakuwa wanafanya kazi kwa umoja wetu na utapata upinzani na ortalisha na watu ambao watakuwa hawana kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hautashirika hivo maana yake unazalisha bomu ambalo baadae litakuwa ni mzigo kwetu sisi kitaifa maana yake wale vijana wote tutakuwa na *center* ambazo kila mahala kama ni Mbeya, kama ni Kigoma kama kuna mawese sehemu fulani tutaweka

hayo tutangalia tusifanye mipango ya kukurupuka, tukisikia korosho leo imefikia shilingi 2000 basi tuna sambaza miche nchi nzima, haya leo imeshuka tunafanyaje yaani hiyo maana yake ni mipango ambayo hatushirikishi na tunashindwa kutumia nguvu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo maana yake kwamba panapotokea jambo hata kama madini leo ni shilingi 5000 tusifikirie kuangalia madini yale peke yake, tuangalie nini ambacho kinifuata ili tukifanye ili tuhakikishe kwamba uchumi wetu unakuwa uchumi imara. Lakini tuweke uchumi ambao ni mfumo, tuweke mfumo ambao utakuwa ni endelevu, leo umetengeneza huu mpango je, huu mpango ni endelevu? Kama leo baada ya mwaka mmoja akija mtu mwingine anaweza akaubadilisha? Kamwe tusimpe *loophole* mtu mwingine kutokana na mpango wako ambao umeutengeneza leo akapata nafasi kuuharibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie kama tumetengeneza mpango au watu wa Serikalini kwa mfano watumishi mimi nakumbuka wakati ule wakati tulipokuwa tunaa jiriwa tulikuwa tunalipwa posho, kuna *substance allowance* mtu akishaajiriwa analipwa malundo ya posho kiasi kwamba yeze hawezu kuingia tena kwenye *corruption*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo maana yake hawa watumishi wa Serikali lazima uangalie masilahi yao ili wao wanapoenda kufanya kazi miguu yaani watakuwa wanaishia huko. Lakini kama utakuwa unaangalia mpango tu wa kupata fedha Serikalini bila kuangalia hawa watumishi, Mpango utakuwa unajidanganya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jingine ambalo Mheshimiwa Mpango ambalo unatakiwa uliangalie ni kundi la wanasiaya, kundi ambalo ni kubwa sana Waheshimiwa. Mtu atakudanganya kwamba bwana *okaywewe* mpango wako angalia tu mambo ya kiuchumi. Lakini wanasiaya wapo na wao wana nafasi yao katika kufanya *participation* katika kufanya maamuzi sasa kama wao wanafanya maamuzi wamekaa humu ndani na wewe Mheshimiwa

Mpango umesikia wanalamika hapa watu kwamba wewe unatumia la *STL*, lakini hapa kuna Mbunge leo anaenda pale mpaka mnafika pale Kibaigwa unamkuta Mbunge gari yake ile aliyokopa ya milioni 60 hiyo mbovu imekufa, ameificha pembedi. Hivi wewe mtu kweli atakuunga mkono, kwa hiyo maana yake lazima uangalie...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Akbar.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watu watakuwa wanakudanganya, watakuudanganya kwamba sisi hatutaki maslahi yetu. Lakini nawasifu kwamba mmetengeneza vitu ambavyo vya kimsingi unatengeneza kabisa kuna ndege, kuna viwanda, kuna *participation* lakini kubwa je, maslahi ya hayo maamuzi ya hao wanasiasa inakuaje. Nakushukuru sana...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Akbar, ahsante sana muda wako nimekuachilia kama dakika moja.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado dakika moja eeh. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Mpango kwamba Mheshimiwa Karume wakati anaondoka pale alipojenga zile nyumba za Michenzani wale Mawaziri wake wake wote allwajengea nyumba moja moja hawakuchukua rushwa, sasa leo wewe Wabunge badala ya kuwaona kwamba hawa Wabunge na wao wana nafasi unawaacha hivi hivi halafu unawaambia wasichukue rushwa kwa kuwa tu rushwa tu haipo, naomba uangalie wanasiasa uangalie watu binafsi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Akbar.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Albert Obama baadae Mheshimiwa Saul Amon ajiandae.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia mpango huu.

Kwanza kabisa nimpongeze Waziri kwa wasilisho lake zuri, kwa kweli mpango tumeupitia, mpango wako ni mzuri kwa sababu umejaribu kuitia tulipotoka tulipo na tunakoenda. Kwa hiyo, nikupongeze kweli kweli na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, lakini kipekee naipongeza Kamati yetu ya Bajeti na mimi nipo kwenye Kamati hiyo tumeipitia bajeti yetu, tumetoa maoni yetu kwenye Kamati yetu ya bajeti nafikiri maoni yetu unayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi sitaki hata kupita sana kwa sababu yote tulishayasema kwenye Kamati na mengine tumekushauri ndani ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipekee niipongeze Serikali kwa mipangilio ambayo imeshatekelezwa na miradi iliyokwisha tekelezwa ni ukweli usiofichikwa kwamba mmefanya kazi nzuri na miradi hii ni miradi mikubwa ambayo kwa kweli inahitaji kuwa *serious* ili *uweze kui-achieve*, kama hautakuwa *serious* hautaweza ku-*achieve* kwa sababu inahitaji fedha ngingi. kwa hiyo nakupongeza sana Waziri nampongeza Rais, napongeza na chama changu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye mpango wenye kwenye sheria pale kwenye Sheria ya *PPP*. Pale umeandika kwenye *page* 43 kuna miradi ya maji nayo ambayo inatakiwa kwenda na *PPP*. Sasa mimi wazo langu ni kwamba ile miradi sasa ambayo ya maji ambayo unataka iende kwa *PPP* katika ile orodha ya miradi ambayo unataka iweze kuwepo kuwa *solicited* au iko *solicited* na Serikali hatujaweza kuipata, ni vizuri kwenye mpango unaokuja tuweze kuona kwenye maji, miradi ya maji ulivyoitaja ukurasa wa 43 ni miradi gani hiyo ili tuweze kuielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *page* ya 47 ya hotuba ya Waziri kuhusu miundombinu amesema tuweze kuunganisha Tanzania na nchi jirani kwa upande wa miundombinu. Wazo

langu langu pale sasa Mheshimiwa Waziri kwa sisi ambao tuko mpakani tunaomba kwenye mpango wako utuwekee madaraja kuunganisha nchi na nchi, tunayo matatizo specifically kwenye Jimbo la Mheshimiwa Obama pale tunatenganishwa Burundi na Tanzania na mto ambao sasa ule mto ni mkubwa tunahitaji madaraja. Kwa hiyo katika kupitia *page* yako ya 45 tunaomba madaraja pale uweze kuyaweka ili angalau iweze ku-*facilitate* biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa *page* 37 ya hotuba yako upande wa kilimo umetaja mambo ya michikichi tungeomba kwa sababu Waziri Mkuu alikuja kwa heshima kubwa sana Mkoa wa Kigoma akawa ameimiza michikichi. Kwa hiyo, tunaomba Wizara ya Kilimo iweze kulichukulia hilo na wewe umeliweka kwenye mpango ili iweze kuwa *serious* Mkoa wetu wa Kigoma michikichi mbegu na utafiti viweze kuwa vimelmarshwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo amelisema Ndugu yangu Silinde kwenye hotuba yake ame-*challenge* sana pale kwenye hotuba yako ukurasa wa 34 aliposema changamoto umezieleza pale, sasa siamini kama mpango wowote ule ambao unaweza ukawa umepita ambao changamoto hazipo. Sasa kutupia tu kwamba changamoto zipo sisi tulitegemea kama Wabunge sasa tutoke pale tumpe mawazo namna ya kwenda kwenye mpango unaokuja. Lakini kusema kwamba changamoto kwenye mpango wowote hamna mimi nafikiri siyo sahihi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho ni mifano ambayo sasa tunaanza kuingizia mfano nchi ya Rwanda, sisi ni Wabunge wa Tanzania tuko *proud* na mambo yetu ya Tanzania. Kusema kwamba Rais Kagame anawashauri wengine nchi za nje siyo sahihi na sina uhakika JPM kama anahitaji washauri kwa sababu kama niwashauri Rais Mstaifu Ali Hassan Mwinyi bado yuko hai, Benjamin William Mkapa bado yuko hai, Jakaya Mrisho Kikwete bado tuko hai Chama cha Mapinduzi ambacho ni imara bado kiko hai, Kamati Kuu

bado iko iamara Wabunge wa CCM tuko imara, tutaendelea kumshauri tuhakikishe kwamba nchi yetu inaenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Albert Obama tunaendelea na Mheshimiwa Saul Amon baadae Mheshimiwa Maftaha Nachuma na Mheshimiwa Catherine Ruge wajiandae.

**MHE. SAUL H. AMON:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza naomba niungane na wenzangu kupongeza uongozi wa Rais wetu Magufuli kwa kazi anayoifanya, kwa wote nadhani wanaona hakuna ambaye haoni na jinsi anavyotekeleza amekuwa ni mzalendo wa nchi hii pamoja na Mawaziri wake wote kwa pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naenda ninayo yangu matatu kwa Mheshimiwa Mpango. La kwanza kuna hili la mazao ghalani ambalo limeanzishwa kwenye kahawa, korosho na pamoja na kokoa. Kuna baadhi ya haya mambo ni mageni sana sana kama haya ya kahawa na kokoa yameanza sasa hivi, lakini yameanza kwa kishindo wananchi hawatuelewi, tunashindwa kupita vijijiini, naomba mpeleke ushauri ni namna gani hizi haya mazao ghalani yatakuwa yanafanywa yanawekwa na watu wana nunua namna gani. Sababu ya kuzungumza hivo kwa sababu unakuta mkulima ye ye amelima amechuma na hana hela za kuwapa wale vibarua waliokuwa wanamsadia, hata mimi mwenyewe nikiwemo, lakini tumepeleka kahawa yetu hatujue bei yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nyuma wakati tunakua kulikuwa na mauzo ya kahawa ambayo tulikuwa tunalipwa kwanza hela, lakini ikienda kuuzwa tulikuwa tunaletewa hela iliyobaki tulikuwa inaitwa mabaki. Lakini sasa hivi hawajui itauzwa bei gani, itauzwa na nani, lakini

tumekusanya tumeshaipeleka kwenye vyama vyetu nya ushirika, hilo nilikuwa najaribu tu kwamba kama Serikali iliangalie hilo ili tuepukane na hayo mabomu na maswali mengi tunayoshindwa hata kuyajibu kwa hao wakulima wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu kuna kodi ambayo kwa kweli si rafiki sana hii najaribu tu kukumbusha Bwana Mpango mwaka jana niliongelea na leo nazidi kuongelea. Kuna kodi ya mahoteli ya vyumba watu waliokuwa/wanaokusanya VAT kawaida walikuwa hawadaiwi hii kodi ya chumba ya asilimia kumi kwenda kwenye Halmashauri zetu au kwenye miji yetu. Lakini imekuja baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikidai lakini huyo mfanyakabiashara ambaye atakusanya asilimia kumi ya Serikali Kuu, asilimia kumi ya Halmashauri na vilevile kuna kodi zingine nyngi kuna *city service levy* zote zinakusanya na huyo huyo, je, huyu ambaye akusanyi VAT maana yake watu wote watakimbilia kwake na hili suala naomba liangaliwe kuna baadhi ya Halmashauri zimeanza hizo fujo, kuna baadhi ya Halmashauri zinataka kukusanya na kuwapeleka watu na mbaya zaidi hawatumii kama TRA wanavyosema kwamba sisi ni asilimia 18 anakuja anakuhesabia vyumba anahesabu na vyumba 50; mara 50,000, mara mwaka mzima hajui walilala watu au hawakulala anaku-*charge* na kukupeleka mahakamani, kwa kweli hilo ni kubwa na ni baya zaidi kwenye masuala ya kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hilo uliangalie ulisimamie kwamba je, huyu anayekusanya VAT je, naye anatakiwa alipe hiyo asilimia kumi ya *city service levy* naomba hilo uliangalia make pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ambalo hili ni kukumbusha ndugu yangu Mpango mmeefanya kazi kubwa sana nchi hii na hela zinazolipwa na wafanyakabiashara na kodi zinazolipwa zinaonekana zinatumika namna gani. Alie na macho haambawi tazama, mimi nina macho natembea nchi naona jinsi Serikali inavyofanya kazi. Lakini siamini kwamba Bwana Mpango na timu yako yote ya ukusanyaji

mapato mmewahi kujuliza kwanini watu wakimbie na kodi, kwa mfano *SADC* kodi zote ni sifuri, lakini mtu anashindwa kulipa, hamjilizi ni kwa nini. Mimi nitakupa hapa kwa nini na nakukumbusha kwasabau mwaka jana nizungumza na mwaka huu najaribu kukumbusha mamlaka zilizopo, *TRA* haina tatizo unapeleka wanakulipisha kodi yako, ukitoka *TRA* kwa mimi nizungumze mimi kama ndio mdau wa hiyo eneo nazungumza kwa upande wangu utakuja *TFDA* ndio waliopewa kwenye chakula na dawa kuangalia usalama wa chakula na dawa. Na wanautaraibu ambao unaeleweka vizuri, anakwambia bidhaa yako unataka kuingiza ulete tuijime tuisajili tutakupa kwa miaka mitatu, vizuri kabisa *TRA* anakwambia ingiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka *TRA* unakutana na *TBS* anakwambia upitishi huu mzigo sasa siuji nani ni nani hizi mamlaka zingejaribu kupewa kila kitu kila mamlaka nafasi yake ili watu wasiweze kukimbia, wanakimbia kwa sababu mamlaka ni nydingi, *TBS* ukimalizana nao anakwambia sasa kuna vipimo sasa sisi tunaoleta vikolokolo ni hatari kweli kweli, mtu wa *weights and measures* naye anataka apime kila chupa ya mafuta uliyoleta kila *ceiling board* uliyoleta, kila kigae ulicholeta mzigo hautoki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mzigo wa kutoka siku moja uliotolewa na *TRA* na *TFDA* utakwenda miezi miwili, miezi mitatu bado uko hapo hapo. Naomba hizi mamlaka na ningependekeza hizi mamlaka kila mamlaka ifanye kazi yake, lakini katika nyongeza hatutawakuza hawa wafanyabiashara wadogo, hapo Bwana Mpango uliangalie kwa kuititia mamlaka zako uangalie hasa *TBS* anakwambia ukifika kwenye nchi husika unatakiwa ukapate *certificate* ya kila aina ya mzigo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nishazungumza tena na hili nakukumbusha tu, wewe ni mfanyabiashara mdogo umeenda ku-*consolidate container* una bidhaa aina kumi utafute makampuni kumi yote yakupe *certificate* na wewe ulikwenda kununua kwa *supplier* hukunua *direct* kutona kwa

*manufacturer.* Kwa kweli hiyo ni kazi ni ngumu hatuta hawa Watanzania tunaotaka kuwainua kibashara hawataweza kuinuka au kuwe na sababu moja tu kwamba hakuna kuagiza mizigo au mizigo mbadilishe utaratibu wafanye kama wanavyofanya *TFDA* tusajili kwa sababu hakuna kilichofichika. Kwa mfano tunazungumza habari ya *SADC*, ....ipo *SADC*, *Uniliver* ipo *SADC*, hivyo unapokwenda kununua au kiwanda cha *ceiling board* kipo *SADC* sisi tuchukue kiwanda cha *ceiling board* kinachoelewaka na *address* inayoeleweka tulete *TBS* waisajili ili kesho na kesho kutwa nisiendelee kutaka *certificate* ya kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo mimi naamini tutawafanya Watanzania hawa amba ni wadogo wanaotaka kukua kwa sababu amini usiamini, hakuna aliye kua, wote tulizaliwa, tukawa na siku, mwezi, mwaka, miaka mpaka tukafika ikawa *S.H. Amonikawa brand* badala ya kuwa jina ikawa ni *brand.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo Bwana Mpango, kwa hiyo kama mimi nimefika pale nina vifurushi vyangu vya tani moja kwa nini nisiende porini pamoja na kwamba ni *zero rated* hata kama ni *zero rated* kwa nini mimi niende nikasumbuke nikae miezi kufuatilia? Nitapita porini na ndiyo maana unakuta watu wanapita porini, mngejiliza hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka yetu iko wazi, hilo ulielewe na ndiyo maana nakuambia kwamba *TRA* wewe kwa mfano umenunua mizigo *South Africa* hujashuka hapa unakuta karatasi zako zipo tayari za kwenda kulipia ushuru na unalipa. *TFDA* tayari ulishafika unalipa, lakini ukianza kusema kila *item* uende ukalipie, ununue *ceiling board* waende wakakague, ununue sijui kigae waende wakakague. Naomba sana sana ili watu wasiende porini, kwa sababu hapa nchi zote za *SADC* hakuna kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ukiniambia *VAT* ni kodi mimi kwangu *VAT* sio kodi, mimi nakukusanya na kukuletea, kwa sababu nitakuja kukudai, lakini unavyoniambia nikae

wiki tatu na mtaji wangu ni shilingi milioni mbili haiwezekani na huwezi kuwafanya Watanzania wadogo waanze biashara na wakue. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SAUL H. AMON:** Naomba mliangelie hilo. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amon.

**MHE. SAUL H. AMON:** ...mliangelie hilo, mkae, tuweze tuwe tunapata *certificate* kutoka *TBS* kama tunavyopata kutoka *TFDA* na kama tunavyopata kutoka *TRA* hatuna matatizo nako lakini hapa pana matatizo makubwa. Mimi huo ndio mchango wangu...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amon.

**MHE. SAUL H. AMON:** ...na ilikuwa ni ombi langu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja iendelee. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Maftaha Nachuma baadae Mheshimiwa Catherine Ruge na Mheshimiwa Ruth Mollel wajilanda.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuchangia mchango huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kufikiria na kusoma soma hivi vitabu vya mipango ambavyo tumekuwa tunaletewa hapa kwa muda wa miaka mitatu hivi sasa tangu nimekuwa Mbunge, lakini nimegundua kwamba mipango hi ni mingi sana, lakini siyo tu mingi, mipango hii inahitaji muda sana, lakini mipango hii inahitaji udadavuza wa kutosha kabisa ili kuweza kutekeleza mipango hii kutokana na *intricacies* zake zilizopo, Waingereza wanasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yangu ni nini? Kwa sababu Wizara hii imepewa majukumu mengi sana, Wizara ya Fedha kazi yake ni kuleta mipango yote ya fedha, kutengeneza bajeti ya fedha, kuzipa Wizara zote fedha na utekelezaji wake kufuutilia, lakini tumeipa kazoi nytingine ya kutengeneza mipango na kusimamia mipango. Mimi nilikuwa nashauri kwamba mamlaka zinazohusika Serikali itenganishe kuwe na Wizara ya Mipango na kazi yake iwe ni kutunga mipango na kusimamia mipango pekee, lakini kuwe na Wizara ya Fedha lakini kuichanganisha, kuziunganisha kama ilivyo hivi sasa ndiyo maana tunaona baadhi ya maeneo yanashaaulika, baadhi ya mambo ambayo yamepangwa na Serikali yanashindwa kufuutiliwa kwa sababu Wizara hii imepewa jukumu kubwa sana. Nashauri Serikali itenganishe ziwe Wizara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nilikuwa napitia mpango hapa huu muelekeo wa mpango kwenye changamoto hizi amezungumza Mheshimiwa hapa kwamba mionganoni mwa changamoto ni uwezo wa wakandarasi wanaopewa zabuni za ujenzi katika miradi inayofuatiliwa kutokuwa na uwezo wa kutekeleza miradi hiyo kwa wakati uliopangwa kwenye mikataba. Sasa ni jambo la kusikitisha sana kwamba Serikali yenye ndiyo inachagua hao wakandarasi, Serikali ndiyo inayofuata taratibu za manunuzi na tukachangua wanunuzi ambao hawa wakandarasi ambao ni *best* kutokana na Sheria ya Manunuzi lakini mwisho wa siku inafuatiliwa, inaonekana kwamba wale wasimamizi au wale watekelezaji au wale waliopewa zabuni hawana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze jambo moja hapa, mwaka jana wakati Mheshimiwa Rais amekuja Mtwara kuja kuzindua pale ujenzi wa bandari lakini pia kuweka jiwe la msingi la barabara kutoka Mtwara Mjini mpaka Mnivata kilometra 50, alizungumza wasiwasi wake huu kwamba kuna mkandarasi yule amepewa ujenzi wa barabara ile kutoka Mtwara Mjini mpaka Mnivata kilometra 50 barabara ya uchumi, yule mkandarasi alisema kwamba hana uwezo wa kutosha. Sasa tunashangaa kwamba mtu hana uwezo wa kutosha na anajulikana na Serikali lakini bado anapewa ule

mradi kutekeleza, mpaka leo ule muda ambao alipangiwa kumaliza ule mradi, mradi unasuasua mopaka leo ile barabara kilometra 50 tu sasa ni jambo la ajabu sana.

Mimi niishauri Serikali kwamba yale ambayo tumeyaona kwamba ni mapungufu na wale ambao hawafai, wazabuni ambao tumewapa *tender* hawawezi kusimamia na kutekeleza sawa sawa kwa wakati basi wasipewe hizi kazi ndiyo lengo la Serikali kuliko kuchelewesha kazi tunawapa wale wale ambao tumeona wana makosa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilikuwa napitia kitabu cha Mheshimiwa Mpango hapa kana kunavyopanga hii mipango tunatakiwa tuangalie usawa wa nchi yetu kwa sababu lengo la nchi hii ni kuondoa umaskini. Sasa tulikuwa kwenye bajeti tunazungumza suala la ujenzi kwa mfano wa viwanja vya ndege na humu kwenye mpango nimeona pia kwamba Serikali imejipanga kukarabati na kuendeleza viwanja vya ndege, sasa naangalia hapa kwenye ukurasa huu wa 30 sioni kiwanja cha ndege cha Kanda ya Kusini ambacho ndiyo chanzo kikuu cha uchumi kwa ndege zetu za Kanda ya Kusini, uwanja wa ndege wa Mtwara hapa haupo wa Kanda ya Kusini sasa ni jambo la ajabu sana tunazungumza maeneo mengine na Kanda zingine zinaachwa kwa makusudi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tulizungumza wakati wa bajeti hapa kwamba kiwanja kile kilitengewa shilingi bilioni 54 kwa ajili ya ujenzi lakini humu kwenye mpango hakipo na miradi ambayo inatekelezwa ambayo imepangiwa bajeti tumeiona humu yote ipo imetajwa na Mheshimiwa Waziri wa Mpango. Sasa tunaomba utuambie Mheshimiwa Waziri wa Mpango kwamba tunavyopanga na maeneo mengine tunasahau ama tunayaacha? Badala ya kwenda mbele tunarudisha nyuma, lengo ni nini Mheshimiwa Waziri Mpango?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine pia ni suala hili la reli ya Ukanda ule wa Kusini wenzangu wamezungumza na ukanda huu wa Kusini Mheshimiwa Akbar kasema

kwamba ndiyo ufunguzi wa uchumi na tunapotaka kuondoa umaskini lazima hii nchi tu-*decentralise* uchumi wetu, tufungue milango yote; reli ya katikati *standard gauge* ni jambo jema sana, lakini reli ile ya Kusini ambayo iling'olewa miaka ya 1963 na kupelekwa maeneo mengine basi irudishwe sasa ianzie pale Mtwara Mjini, Bandari ya Mtwara ielekee kule isiwe kila mwaka tunaandika kwenye mipango, utekelezaji unakuwa ni mdogo. (*Makof*)

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana kwamba ule tunaoita upembusi yakinifu ule ambao unataka kuanza kutoka Mtwara Mjini mpaka kule Mbambabay, kule Mchuchuma na Liganga basi uweze kupelekewa fedha siyo kila mwaka tunaandika kwenye mipango fedha hazi pelekwi na utekelezaji unakuwa ni mdogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine kuna suala la uendelkezaji wa viwanda ili viweze kuleta ajira kubwa sana kwa Watanzania na kuondoa umaskini, lakini jambo la kusikitisha chuma kinapatikana Mchuchuma na Liganga ndipo kwenye chuma pale na chuma ndicho kitatoa *material*...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tupunguze sauti, ongeeni taratibu jamani tumsikilize huyu.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:**...chuma kinapatikana Mchuchuma na Liganga lakini kiwanda cha kutengeneza chuma kinakwenda kuwekwa Moshi, ni jambo la ajabu sana. Serikali hii inatakiwa iangalie kwa sababu tunavyowekeza katika uchumi wetu tunahakikisha ya kwamba tunawekeza kwa gharama nafuu sana sasa unavyotoa chuma kutoka Mchuchuma na Liganga kama huo mradi ukikamilika *then* ukakipoeleka Moshi kwenye Kiwanda cha Chuma gharama inakuwa ni kubwa sna na inakuwa badala ya kwenda mbele bado utatumia rasilimali kubwa snaa katika kusafirisha *material*. (*Makof*)

Mimi nashauri kwamba kiwanda cha chuma kijengwe kule kule Songea, kule kule Mchuchuma na Liganga ambako

ndiko *material*/yale yanatoka kule na tusiende kuweka umbali mrefu kama ilivyokwenye taarifa mbalimbali ambazo tumekuwa tunazisoma za Kamati. Hii itapunguza ile hali ya kuweza kutumia gharama kubwa kwenye kusafirisha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilitaka kuzungumza kwenye mpango hili limezungumzwa suala la afya kwamba Serikali imejipanga na inamkakati wa kurekebisha suala hili la afya nalo pia kama ilivyo kwenye maeneo ya viwanja vya ndege kwamba Mikoa ile ya Kusini ukisoma kwenye taarifa hapa ya Mheshimiwa Mpango kwamba amepanga kuboresha hospitali za rufaa kwenye ukurasa wa 24. Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini haipo, nikiangalia humu hakuna kabisa, haijatengewa hata kuwekwa tu kwenye mpango kwa sababu tunaanza kuweka kwenye mpango halafu tunaingia kwenye bajeti. Sasa Hospitali ya Kanda ya Kusini haipo humu ndani na tumezungumza wakati wa bajeti, tumezungumza miaka yote, kwenye mipango yote iliyopita sasa kama unaondoa kwenye kitabu cha mpango vipi kwenye bajeti inayokuja? Kwahiyio mimi nishauri sana kwenye...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:**...ukurasa wa 24 ihakikishwe ya kwamba hospitali hizi za Kanda basi ziangaliwe Kanda zote ili Watanzania waweze kuwa na afya bora.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maftaha. Tunaendelea na Mheshimiwa Catherine Ruge na baadae Mheshimiwa Mendrad Kigola ajiandae.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata fursa na mimi niweze kuchangia

Mpango wa Serikali wa mwaka 2019. Mchango wangu umejikita kwa eneo moja kutokana na umuhimu wa eneo hilo na eneo hilo ni kilimo. Lakini kabla sijajikita kwenye mpango ningependa nitoe takwimu za umuhimu wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kinachangia asilimia 70 ya ajira katika nchi yetu, kinachangia fedha za kigeni takribani *1.2 billion USD* ambazo ni sawa na asilimia 35 ya pesa zote za kigeni zinazoingia katika nchi yetu. Lakini pia kilimo kinalisha malighafi kwenye viwanda kwa asilimia 65, kilimo kinatuwezesha kupata chakula kwa asilimia 100 katika nchi yetu, lakini pia kilimo kinachangia asilimia 29 ya pato la Taifa. Pamoja na *contribution* ya kilimo kwenye Taifa hili lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi bado haijaipa sekta ya kilimo kipaumbele, kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwcaa jana ilikuwa shilingi bilioni 170 pungufu ya shilingi bilioni 44 kutoka kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018. Kwa mwaka mmoja tu bajeti ya kilimo ilipunguzwa kwa asilimia 20.8 wakati wenzetu wa Kenya wanaongeza bajeti ya kilimo kutoka asilimia 2.3 kwenda asilimia tisa ya bajeti ya Taifa sisi tunapunguza bajeti ya kilimo kutoka asilimia 0.8 kwenda asilimia 5.2, *are we serious* kweli tunataka kutengeneza Tanzania ya viwanda? Na tunasema Tanzania ya wanyonge, Serikali ya wanyonge, hivi kuna wanyonge zaidi ya wakulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye ukurasa wa tano wa mpango inaonyesha wka mara ya kwanza kwenye historia ya nchi yetu kilimo kilikua kwa asilimia 1.1 mwaka 2016 baada ya Serikali hii kuingia madarakani, mwaka 2015 kilikua kwa asilimia 3.4 lakini bado bajeti ilipunguzwa. Hii inaonesha Serikali hii ni adui wa wakulima kwa maana wame-focus zaidi na kipaumbele imepewa asilimia tano ya watu ambao wanaweza kupanda ndege na kutokomeza, kuwaweka asilimia 70 ya wananchi wa Tanzania wanaotegemea kilimo kwenye wimbi la umasikini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye mpango. Niliamua nisome vitabu vitatu vyaa mpango

ili niweze kuona *trend analysis* kwenye sekta tu ya kilimo, lakini pia nlitaka nijue ni kwa nini mipango ya hii Serikali haitekelezeki na badaa ya kusoma nilipata majibu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina kitabu hapa cha mpango 2016/2017, 2017/2018 na hiki cha taarifa ya utekelezaji wa mwaka huu na nili-focus kwenye kilimo tu kwa sababu najua tukiwekeza kwenye kilimo tunakwenda kuwatoa asilimia 70 ya Watanznaia kwenye wimbi la umaskini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yaani mambo niliyoyaona ni maajabu. Baada ya kusoma ni kwamba Serikali inatekeleza vitu ambavyo haikupanga, *ina-report* vitu ambavyo haviko kwenye mpango, *inaondoa* vitu ambavyo vilikuwa kwenye mpango lakini kubwa zaidi hata pesa za kutekeleza hiyo mipango pia hazipo. Ukiangalia *implementation* ya bajeti ya maendeleo ya mwaka jana imekuwa *implemented* kwa asilimia 55 tu na asilimia 45 pesa hazikwenda kwenye bajeti ya maendeleo lakini nawashangaa Waheshimiwa Wabunge, tumeacha jukumu letu tulilopewa Kikatiba la kusimamia Serikali lakini jukumu la *stewardship lord* tulilopewa na wananchi la kuja kuwakilisha wananchi Bungeni, tumebadilisha majukumu yetu badala ya kuksimamia Serikali tunapongeza na kushukuru, kumpongeza Rais, inasikitisha kwa kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuoneshe vituko viliyo kwenye mpango kwenye sekta ya kilimo. Mwaka 2016/2017 unaambiwa ukurasa wa 70 mpaka 71 zilitengwa shilingi bilioni 4.35 fedha za ndani kuweza kuzalisha mpunga kwa tani 290,000 na sukari tani 150,000 lakini pia kupatikana kwa hati kwa mashamba makubwa kwenye Mkoa wa Katavi, Rukwa, Tabora, Lindi, Kigoma, Ruvuma, kuandaa kanzidata kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi kwenye eneo la Ludewa na Rufiji hiyo ilikuwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa njoo 2017/2018, hatua iliyofikiwa, kuandaliwa programu ya muda mrefu na mfupi ya upimaji wa ardhi kwa matumizi ya kilimo. Serikali imetoa

shamba la ukubwa wa hekta 10,000 lililoko Mkurunge, Bagamoyo kwa Kampuni ya Bakhresa kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo cha miwa na sukari. Ukiangalia hivi vitu hata havikuzungumzwa kwenye mpango, hiyo ndiyo hatua. Kwa hiyo, mna-*implement what you didn't plan*. Haya njoo sasa kwenye taarifa ya utekelezaji ni vichekesho, unaambiwa hivi; kwanza hakuna kabisa hata habari ya hilo shamba ya Bakhresa, hakuna *implementation status* ya hiyo tani 150,000 ya sukari pamoja na tani 290,000 na mashamba ya miwa hayajazungumziwa kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja eneo la pili, tafiti za kilimo mwaka 2016/2017 milioni 854 za fedha za ndani na milioni 53 zilitengwa kwa ajili ya kuleta tani 10 za mbegu za mpunga, kukarabati na kuimarisha vituo 12 vya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda sasa mwaka 2017/2018, hatua iliyofikiwa ni kuzalisha mbegu 35 mpya za mahindi haikuwepo kabisa kwenye mpango kule wanasema vitu vingine na huku wanasema vitu vingine. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya utafiti havijazungumziwa kabisa. Kati ya tani 10 ambazo miliahidi kutekeleza ni tani 2.9. Njoo sasa kwenye taarifa ya utekelezaji ni vituko, hakuna vituo vyovoyote vilivyo fanyiwa utafiti, habari mpya za mbegu hazijazungumziwa kabisa. Hiyo ndiyo Serikali ya CCM ambayo inajua kupanga na kutekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nishauri kwa haraka haraka, Serikali ijenge uchumi shirikishi ambao unaweza kuhakikisha ukuaji wa kilimo unakuwa sambamba na ukuaji wa pato la Taifa. Ukiangalia kilimo kinakuwakwa asilimia 2.1 wakati pato la Taifa linakua kwa asilimia 7.1 yaani mbingu na ardhi. Ukiangalia viwanda vinakua kwa asilimia 6.8, kilimo asilimia 2.1... (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ruge.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** ...sasa sera yetu.

**MWENYEKITI:** Kabla ya Mheshimiwa...muda wako umemalizika Mheshimiwa.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika kumi hazijakwisha.

**MWENYEKITI:** Hiyo kengele ya pili hiyo Mheshimiwa. Tunaendelea, kabla ya Mheshimiwa Mendrad tunaenda na Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Naomba dakika moja tu nimalizie.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruth Mollel baadae atafuata Mheshimiwa Mendrad Kigola.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mezani na moja kwa moja ninaunga mkono maoni ya Kambi ya Upinzani ambayo yametolewa vizuri sana na Mheshimiwa Halima Mdee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana katika ule mpango ulioletwa nilizungumzia sana suala la rasilimali watu na katika ule mpango wa mwaka jana iliahidiwa kwamba shughuli zilizopangwa ni kusomesha wataalam katika fani adimu za mafuta na gesi, madaktari bingwa katika nyanja za moyo, figo, ubongo nje ya nchi na katika vyuo vyua ndani vya Muhimbili na Benjamin Mkapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika taarifa ya utekelezaji hakuna mahali popote katika taarifa ya utekelezaji ambayo imetupa takwimu ya hao wataalam ambaao tumewapeleka au nje ya nchi au katika vyuo tulivyovitaja na takwimu ni muhimu kwa sababu hiyo ndio itawenza kutuwezesha kupima kama tumefanikiwa au hatujafanikiwa na nikiangalia pia katika taarifa ya utekelezaji taaluma tu ambayo wapelekwa nje ya nchi ilikuwa ni wana hewa 17 ambaao nafikiri ni *civil avitation* na injinia mmoja ndio ambayo imeoneshwa katika vitabu hiki cha utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa yako hii ya mwaka huu kuhusu suala la rasilimali watu umesema kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, umesema maeneo watakayopewa kipaumbele ni elimu na ujuzi hususani kusomesha kwa wingi wataalam kwenye fani na ujuzi adimu, afya na ustawi wa jamii, maji na usafi wa mazingira, vijana, ajira na wenye ulemavu, habari, utamaduni na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *suiting statement* ambayo ningetegemea kwamba katika ule mpango ambao kile kitabu cha mpango mwaka huu tungenyambua *to unbundle* na kusema katika hizi nyanja za mkakati tutakuwa na wataalam wangapi kwa kila eneo, kwa mfano tuna mkakati huo wa ndege za Serikali, tuna hizi bombardier, tuna *Dream linear* ambazo zinakuja zingine, lakini sijaona popote Mheshimiwa Mpango ambapo umeainisha kwa sababu marubani wengi ni wa nje hata Mheshimiwa Ndassa pia amelizungumzia hili ni lazima tuone kinagaubaga wataalam wangapi tutawa-*train*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye suala la *ma-technician* kwa *Air Tanzania* hatuna *ma-technician* kwa hizi ndege mpya wengi ni kutoka nje, je, Serikali ina mpango gani kuhakiksha kwamba tunakuwa na hawa *ma-technician* ambao watakuja kusimamia hizi ndege ili tupunguze gharama za kuwa na hawa *ma-technician* kutoka nje. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo muhimu sana tuna reli hii ya *SGR* tutakuwa na *locomotives* za za kisasa, kwenye katika taarifa iliyotolewa taarifa ni kwamba *technical education* tunajaribu kuongeza *enrolment* tunajaribu kukarabati, lakini hatujasema kwamba kweli tuna *business plans* ya *SGR* tutahitaji wataalam wangapi na tunaweka mkakati gani wa kuweza kipeleka watu hawa kuwasomesha na tupate namba, tujue ni wangapi kufuatana *business plan* kusudi hata hiyo reli inapokwisha tunakuwa tayari tuna wataalam kwa ajili ya hiyo reli, tuna wataalam

kwa ajili ya kuendesha hizo *locomotives* ambazo tunategemea zitakuwa za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpaka sasa hivi katika suala la rasilimali watu suaona mkakati wowote wa Serikali ambaao umewekwa kushughulikia rasilimali watu, kwenye bajeti ya mwaka jana hakuna bajeti ambayo nimeona kinagaubaga ya kuonesha kwamba imetolewa bajeti kiasi gani kwa ajili ya mafunzo ya hawa wataalam wa mkakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye suala la viwanda, viwanda *primary source* ni kama walivyozungumza wengi ni kilimo, lakini tukiangalia bajeti ya kilimo mwaka juzi ilikuwa ni 2%, mwaka juzi ile ilikuwa 11% bado hatujaona ni jinsi gani Serikali kwa kweli iko na ari (*commitment*) ya kuhakikisha kwamba *agriculture* inahimarishwa ili iweze kutoa *input* kwenye viwanda ambavyo tunataka kuvitayarisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ningetegemea kuona katika mpango *numbers* za Maafisa Ugani ambaao watahitajika kwa ajili ya viwanda, nilitegemea kuona katika mpango tuweke *ratio* kwa mfano kama tunavyofanya kwa madaktari, daktari mmoja wagonjwa 8000 au 10000, tuseme *ratio* Afisa Ugani mmoja anategemewa ahudumie wakulima wangapi na waweze kupimwa na waweze kufuatiliwa. Kwenye hili eneo bado kazi inahitaji kufanyika kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja pia kwenye suala la sekta binafsi, inasikitisha mimi nilikuwepo kwenye *reforms* tulipoanzisha mambo ya *PPP*, lakini Serikali ya Awamu ya Tano imerudi kabisa kwenye suala la ushirikishwaji wa sekta binafsi tumeona miradi mikubwa yote badala ya kufanya sekta binafsi inafanya Serikali yenewe, tumeona miradi kwenye Halmashauri zetu inafanya Serikali yenewe, matokeo yake sekta binafsi imedorola, sekta binafsi ndio mwajiri mkubwa kwa hiyo watoto wetu na vijana wetu wanakosa ajira kwa sababu sekta binafsi imedorola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye uwekezaji mazingira ya uwekezaji hata kufuatana na takwimu za dunia Tanzania ni nchi ya 163 kwenye mazingira mazuri ya uwekezaji Botswana wametushinda 86, Kenya 61. Ukija kwenye urahisi wa kufanya biashara Tanzania tuko 137, Kenya wako 80, Rwanda wako 41, tukija kwenye ada za usajili za wawekezaji kuanzisha biashara Tanzania ni dola za Marekani 250, Kenya 40, Rwanda ni 35; kwa takwimu hizi sekta binafsi haitaweza kufanikiwa kwa sababu watu watashindwa kuja kuwekeza na watakwenda kwenye nchi nyingine. Kwa hiyo, nashauri Mheshimiwa Mpango na wataalam wake waendelee kuona ni jinsi gani mazingira ya uwekezaji yataborehswa ili ku-*attract* wawekezaji wa ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nizungumzie sasa kidogo mimi kama Waziri kivuli wa utawala bora. Utawala bora ni kichocheo kikubwa sana cha kuleta wawekezaji na unapokuwa na viongozi ambaao wanatoa kauli ambazo zinakimbiza wawekezaji, viongozi wanaotoa kauli ambazo zinakinzana hata na sera na matamko ya Serikali na bila kuchukuliwa hatua zozote hii yenye we inatosha kuwakimbiza wawekezaji wasiweze kuja kuwekeza ndani ya nchi. Kiongozi ye yote hana maoni binafsi, kiongozi anapozungumza anazungumza kwa niaba ya Serikali ni lazima matamko yake yasikinzane na matamshi ya Serikali, matamko ya Serikali na sera...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ruth Mollel muda wako umemalizika.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mendrad Kigola baadae Mheshimiwa Yahaya Massare na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka wajiandae.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia mapendekezo ya mpango wa mwaka 2019/2020.

Kwanza na mimi nianze kwa kutoa pongezi kwa Rais wetu mpendwa John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya, hakuna mtu ambaye hakubaliani kwa utekelezaji wake, ndani ya miaka mitatu amefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nichukue nafasi kupongeza Mheshimiwa Waziri wa Mipango pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri mliyoifanya bahati nzuri sana mimi niko kwenye Kamati ya Bajeti na ukisoma hivi vitabu ni vitabu ambavyo vinaeleweka vizuri kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile hapa tunafanya ni mapendekezo ya mpango naona kuna watu wengi labda hapa hatujaelewa vizuri haya ni mapendekezo ya mpango ni mpango ambao tunaupendekeza sio mpango tunaoukosoa, sasa mimi naomba nipendekeza kwa sababu katika mpango inaonyesha kwamba malengo makubwa ni kupunguza umasikini na bahati nzuri sana ameonesha *data* kwamba kutoka 2012 mpaka 2020 kiwango cha umaskini kitapungua mpaka kitafika asilimia 16.7 hii nimeona ni nzuri sana. Sasa ili tufikie asilimia 16.7 ambayo tumepunguza kiwango cha umaskini nini kifanyike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi sasa hivi walio wengi tunaomba sana tuimarishe sana na tuboreshe kwenye sekta ya maji. Sekta ya maji ni muhimu sana, bahati nzuri na kwenye mapendekezo umeeleza lakini nafuu niseme kwamba mpango unatuelekeza baadae tuweze kupangia bajeti sasa mimi napenda nipendekeze kwamba pamoja kwamba umeweka kwenye vipaumbele kuimarisha miundombinu ya maji kuhakikisha kwamba kila mwananchi anapata maji, kwenye eneo hili niombe Serikali tuwe makini sana lazima tuhakikishe kwamba tuliposema kwamba mwananchi kutafuta maji hatembe i mita 400 ziwe mita 400 na kufikia mwaka 2019/2020 asilimia kubwa ya Watanzania wapate maji hilo litakuwa limetusaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti , jambo la pili ameonesha kwamba ataimarisha vituo vya afya, imeoneshwa hapa na

mimi nakubaliana na wewe, lakini lazima tuweke mikakati, kuna vituo vya afya ambavyo havijaisha kwa hiyo tuhakikishe kwamba 2019/2020 vile vituo vya afya ambavyo hatujakamilisha vyote tuwe tumeshakamilisha, bahati nzuri sana Serikali imeanza kujenga hata maeneo kuna maeneo kuna Wilaya nyingine zinajengewa hospitali bahati nzuri hata Jimbo la Mufindi Kusini kule tunajenga hospitali/katika Wilaya Mufindi tunajenga hospitali na Serikali imeshatoa shilingi milioni 500 nimefurahi, lakini tuhakikishe kwamba tunaweka mikakati zile fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya kuboresha hospitali mpya zinasimamiwa vizuri, zinatumika vizuri kwa sababu ile ni kodi ya wananchi na kuhakikisha kwamba zile hospitali zinazojengwa zinakuwa nzuri na zinakuwa *standard.*(*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa sana la watumishi katika hospitali sasa hilli lazima liende sambamba, tukimaliza hospitali basi na ajira mpya kwa watumishi hasa wa upande wa afya waweze kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo lingine la msingi sana kwa sababu tumesema tunapunguza umaskini sasa nataka niongeee kwenye upande wa *REA*. *REA* vijiji niombe Serikali tumeanza vizuri tumalize vizuri tunategemea kufikia mwaka 2020 vile vijiji vyote ambavyo havijapata umeme vimepata umeme vijiji vyote na bahati nzuri Waziri wa Nishati huwa anaongea vizuri sana kwamba kila kitongoji hiyo ni mikakati ya Serikali kwamba kila kijiji kila kitongoji na kila kaya ziweze kupata umeme hiyo ni mipango mizuri na tumeonautekelezaji unafanya na makandarasi wako *site* hiyo naipongeza sana Serikali, ila mimi nisisitize tuzidi kuongeza juhudhi saa hivi makandarasi hawaendi na *speed* ile ya mara ya kwanza, wakishaongeza juhudhi ya makandarasi kufikia mwaka 2020 vitongoji vyote na vijiji vyote vikiwa vimepta umeme basi umasikini moja kwa moja *automatically* utakuwa umepungua.(*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo moja kwa moja ita-connect hata uboreshaji wa uzalishaji wa bidhaa katika

viwanda vyetu. Tukitaka kuboresha viwanda lazima tuwe na umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi sana kuona Serikali ina mpango mkubwa na ule umeme wa maji Rufiji wameonesha kwenye mipango tukiwa na umeme wa maji kutoka Rufiji nadhani tutakuwa tumetimiza lengo la kupeleka umeme vijijini kwa sababu tutakuwa tuna miundombinu mingi sana ambayo inaweza ku-connect kila kijiji na kila kitongoji kupewa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilitaka niliongele kwenye elimu, elimu ameongea vizuri Waziri wa Mipango, ameeleza vizuri sana, lakini naomba tuongeze kipengele kingine Serikali iongeze juhudhi kwa kujenga hosteli kila shule ya sekondari. Tuna tatizo kubwa ya hosteli kwenye mashule yetu watoto bado wanatembea kilometra mpaka 10 mtoto wa sekondari binti anatembea kilometra 10 na hii inasababishia wanafunzi wengi sana kupata mimba mashulenii. Sasa kwenye mipango yetu niombe Serikali tuhakikishe kila sekondari tunaweza kujengea hosteli ili watoto wakae bweni, hili litasaidia sana kupunguza matatizo na kuongeza kiwango cha ufaulu kama watoto wetu watakuwa wanakaa hosteli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu tena bado kuna upungufu wa walimu wa sayansi, tuiwekee mikakati kabisa, niliwhali kuongea siku moja nilisema wanafunzi wanaosoma vyuo vikuu wanachukua elimu ya sayansi wapewe mkopo asilimia 100 na hii itasaidia ku-motivate wanafunzi wengi wajunge na masomo ya sayansi ili tupate walimu wengi tutapata madaktari wengi na hiyo itasaidia na zile maabara ambazo tumejenga kwa sababu Serikali imehamasisha kuna maabara zimejengwa zimeshaisha lakini hakuna wanafunzi wanajitolea kusoma sekondari kwa sababu akienda Chuo Kikuu hapati mkopo asilimia 100. Sasa niombe Serikali kwenye hilo tuiliwekee kwenye mkakati kwenye mpango ionekane kwamba wale wanafunzi wanaojitolea kusoma sayansi wapewe asilimia 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ambalo nimeliona kuwepo kuna upendeleo katika mikopo hasa watoto wa kike, watoto wa kike bado asilimia ile ya kupeleka hizi masomo ya juu bado kwa sababu mkopo hawapewi katika vyuo vikuu, sasa niishauri Serikali katika mipango utoaji wa mikopo mtoto wa kike apendelewe zaidi kuliko mtoto wa kiume kwa sababu mtoto wa kike kwa mfano hajapata mkopo anaanza kufuatilia bodi ya mikopo Dar es Salaama anakaa mwenzi mzima anafuatilia mkopo Dar es Salaama hii imeleta madhara makubwa sana kwa watoto wa kike matokeo yake wanaweza wakajiingiza kwenye mambo mengine ambayo hawakutegemea kwa sababu ya kufuatilia mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali ikitoa mikopo kwa watoto wa kike wote hii itakuwa inapunguza hata ile madhara ya kupata mimba mashulenii hii itakuwa imesaldia sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kigola.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono asilimia 100 mpango huu ambaao ni mzuri ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana uko sahihi huu Mpango unahitaji maboresho ndio maana Mheshimiwa Mpango hapo amekaa anaandika mashauri yanayotoka kwa Wabunge, kwa hiyo, ambaao hawajaelewa ndio hivyo. Tunaendelea na Mheshimiwa Yahaya Massare na baadae Mheshimiwa Rashid Chuachua ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie mapendelekezo haya ya Mpango ya mwaka 2019/2020.

Mimi nataka nianze na suala la umaskini ambalo limeoneshwa katika ukurasa wa nane. Jambo hili lina dhamira njema nimeona dhamira ya Serikali katika mapendelekezo haya. Lakini kuna taatizo kubwa hapa riba

ya mikopo hasa kwa taasisi ambazo hizi mabenki yetu imekuwa si rafiki kwa watu wetu wengi. Ni namna ngumu sana wananchilli waweze kujwezesha hususani wajasiliamali wadogo wadogo, taasisi hizi za fedha lazima ziwe rafiki na ili uchumi wa nchi hii uweze kwenda mbele, wananchi hawa wakiweza kukopeshwa lakini tuweze ku-*increase export* katika mazao yetu ikiwemo mazao ya misitu, asali na mazao mengine ya kilimo ambayo yamekuwa na matatizo makubwa tumeshuhudia kuona leo mazao kama ya mbaazi yamekuwa hayauziki katika mikoa ambayo inalima mazao haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza Serikali tuishauri ione namna bora ya kuwezesha wananchi wakulima hasa wadogo wadogo wa vijiji ili waweze nao kushiriki katika kujenga uchumi wa nchi hii. katika suala la kilimo limeonyeshwa ukurasa wa 17 lakini ni namna gani tunawezesha wakulima tumeshuhudia kuona matrekta yako pale Kibaha yanaunganishwa, ni kwa nini basi sasa tusijikite namna bora kama iliyofanya ile kilimo kwanza ambayo imepelekea nchi hii leo tunajitegemeakwa kiasi kikubwa sana katika uchumi hasa kilimo tumekuwa ukanda huu wa Afrika tumekuwa tunauza mazao kwa nchi za ambazo tumepatakanana nazo kwa sababu mpango wa kilimo kwanza ulikuwa na tija matrekta yalikuwa vijiji na wananchi walikuwa wanalima.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mikopo ambayo ilikuwa ni rafiki japo wengine changamoto zilijitokeza wengine hawakuweza kulipa lakini sio iwe ndoo tatizo tu-*deal/na issue* ya mtu ya mmoja mmoja, mpango ule wa kilimo kwanza ulifaulu sana na matrekta yanapokaa pale Kibaha sioni kama itakuwa ni faida kwa Serikali hata huyu muwekezaji tunamvunja moyo kuona matrekta badala ya kwenda kwa wakulima kule vijiji ili yaendelee kuleta mengine basi anakuwa hawezikufanya.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza katika kuboresha uchumi suala zima la gesi nalo tulione gesi iko Dar es Salaam leo makazi ya watu wa Dar es Salaam

nimeona majaribio yanataka kufanyika kwa maeneo machache tu yakiwemo kwenye maeneo makazi ya watu wanene kule Masaki na maeneo mengine. Lakini maeneo ya makazi ya watu wadogo kama sisi tunaokaa pembezoni basi isaidie gesi hii iwe sehemu kubwa ya kupikia kuondokana na ukataji wa miti ambao si rafiki kwa maendeleo ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifugo tumelina ukurasa wa 18, lakini hakuna mikakati kabisa inayoonesha kwa makusudi mazima kuona sasa mifugo hii yetu inatoka katika utaratibu ule wa kuchunga na sasa waweze kufuga. Ni vizuri tumeona kwamba mna mpango wa madume bora, lakini naona ni machache ambayo yako kwenye taasisi tu kubwa kubwa, wafugaji wadogo wadogo bado hatujawaweka wala hatujawa-*accommodate* kama nao wawe sehemu ya kunufaika na mapendekezo haya ambayo yanaletwa mbele ya Bunge hili tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika ukurasa wa 27 na 28 barabara nyingi zinaonekana zinataka kujengwa, lakini bado barabara zinazounganisha mikoa hazijamalizika. Mikoa ya Singida kuunganisha na Mkoa wa Mbeya ambako na mimi jimbo langu limo humo, barabara yake haionekani humu katika mapendekezo ya mpango huu. Ni mpango gani upo na Serikali kwamba tunauunga Mkoa wa Mbeya kuitia Itigi? Lini sasa wataanza kuonesha katika mapendekezo yajayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri uje na mapendekezo yanayoonesha utakapokuja kwenye mpango tuone ni nini dhamira ya Serikali ya kuunganisha wananchi wa mkoa mmoja na mkoa mwengine, ukiwemo Mkoa wa Singida na Mkoa wa Simiyu. Daraja la Sibiti tumeliona kwa hili nipongeze sana na juhudzi za Serikali ziko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 30 wa mapendekezo haya, nimeona nishati vijijini (*REA*). Bado wakandarasi wengi hawajaanza kufanya kazi, hatujui tatizo

ni nini. Sasa kwenye mapendekezo haya hatuoni dhamira gani ya Serikali Mkoa wetu wa Singida mojawapo ni miongoni mwa mkoa ambao *REA* wamefika, lakini hawajaanza kazi, basi tunataka tuone maboresho katika sula hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona suala la afya umelionesha katika ukurasa wa 38, lakini bado Hospitali za Rufaa ni changamoto, tumeona hospitali moja tu mmeitaja, Hospitali ya Benjamin Mkapa, lakini mikoa mingine hospitali zao za rufaa hazijaoneshwa kwamba hamjazizingatia katika mapendekezo ya mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengi ambayo tunatakiwa kuona, lakini Wabunge wanataka kuona mchakato huu wa reli unafika basi Kigoma, unakwenda hadi Mwanza, umeoneshwa tu kwa kifupi. Nichukue nafasi hii kumshauri Mheshimiwa Waziri azingatie hilo nalo na kwenda makutupora basi na kule mbele tuone basi juhudhi hizi ambazo zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na haya machache tu ya kuchangia mpango huu wa mapendekezo ambayo nimeona kwa kweli, dhamira njema ya Serikali ya kufanya maendeleo katika nchi hii. Ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahaya Massare. Tunaendelea na Mheshimiwa Chuachua baadae atifuatia Mheshimiwa Hamidu Bobali ajiandae.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi nashukuru kupata fursa ya kuchangia kidogo katika maeneo ambayo nilipata nafasi ya kuyamakinikia wakati ninapitia vitabu viliviyotolewa na Serikali kwa ajili ya mjadala wetu wa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze na kutoa pongezi kwa Serikali kwa kazi kubwa waliyofanya ya kutekeleza miradi katika kipindi ambacho wameikiainisha,

lakini niseme tu wakati najaribu kumakinika zaidi kwenye taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika kipindi cha mwaka 2016/2019 sikuona kazi zilizofanywa na Wizara ya Maji kwenye kitabu hiki. Kama itampendeza Waziri Mpango basi atupatie miradi hiyo tuione maana tuna wajibu wa kujua Wizara yetu ya Maji imefanya kazi kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine nilitaka kufahamu utekelezaji wa suala la maji kwa Serikali kwa upande wa Mradi wa Maji wa Mbini ambapo tulitengewa shilingi bilioni mbili katika kipindi kilichopita kwa hiyo, tungepeta fursa ya kuona utekelezaji huo tungeweza kujua kama fedha hizo zimetoka au zimefikia katika hatua gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapopitia mapendekezo ya mpango pamoja na utekelezaji wa miradi bado naona kuna kazi kubwa na Serikali inapaswa kuona umuhimu sasa wa kutenga fedha za kutosha kwenye miradi ambayo inatoa huduma za jamii, huo ndio mtazamo wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi ya umeme, tuna miradi ya maji, lakini pia tuna suala la elimu, hayo ndio maeneo matatu nitakayoyazungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na umeme, suala la usambazaji wa umeme wa *REA* kwa kweli, haliendi sambamba na matarajio ambayo sisi kama Wabunge tunayo. Kwa hiyo, kwa mfano ukisoma kitabu cha utekelezaji ukurasa wa 55 inaonesha kwamba takribani vijiji kama 5,000 ndivyo ambavyo vimefikiwa katika mpango huo. Tukumbuke tunao mpango wa utekelezaji wa *REA* kwa awamu ya tatu sasa na zaidi ya vijiji 7,000 mpaka sasa bado havijafikiwa. Ukienda kwenye mapendekezo ya mpango, katika mapendekezo ya mpango ukurasa wa 30 inaonesha kwamba mwaka kwa 2019/2020 matarajio ni kufikia vijiji 557.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Mkoa wa Mtwara peke yake, Wilaya ya Nanyumbu, Wilaya ya Masasi, Wilaya

ya Tandahimba, Wilaya ya Newala na Wilaya ya *Mtwara DC* utaona kwamba wastani wa utekelezaji wa mpango huu wa *REA* kwa jumla ukitafuta wastani ni kama vile ni 23.6% jumlisha na bajeti ya 2018/2019. Katika mkoaa huu peke yake vijiji 497 vimeachwa mpaka sasa bado havijafikiwa, lakini 2019/2020 tuna mpango wa kufikia vijiji 557, vijiji vingine hivi tunavifiki lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda unakwenda na hapa mimi napendekeza sasa kama tatizo linaloonekana katika utekelezaji wa miradi ya *REA* ni fedha, basi napendekeza Serikali ione umuhimu sasa wa kupunguza fedha katika baadhi ya miradi mikubwa ambayo tunataka kuitekeleza ili tupeleke fedha hizo kwenye miradi inayowagusa wananchi, hususan miradi ya umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la maji, tatizo liko palepale, fedha katika utekelezaji wa miradi. Ukitabu ya Waziri ukurasa wa 31, inaonesha kwamba tumeshawafikia Watanzania milioni 31 kuwawekea maji ya bomba. Hii ni kama 50% tu ya Watanzania wote, bado kuna kazi kubwa ya kufanya katika hili na bado nashauri, ili kuweza kufikia miradi mingi kwa pamoja na kuwafikia wananchi wengi ni muhimu Serikali ikaona umuhimu wa kupeleka fedha za kutosha kwenye miradi hii na ikibidi kupunguza fedha kwenye baadhi ya miradi mikubwa, ili kufika katika miradi ambayo inawagusa wananchi moja kwa moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la elimu, kila nilipokuwa nachangia mpango nimekuwa nikisema kwamba mipango inayoletwa na Serikali pamoja na mambo mazuri mengi yanayofanywa, lakini haigusi elimu nje ya mfumo rasmi na leo nitarudia kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, tangu tumeanzisha kutoa elimu bila malipo, kwa mfano katika shule ya msingi wanafunzi wengi sasahivi wanaandikishwa na wengi wanamaliza, lakini bado naijuliza wanafunzi hawa ambaao kimsingi shule za msingi ni nyingi sana kuliko shule za sekondari, wanapomaliza, ni wazi kabisa watoto hawa

kwanza wengi wao ni watoto wa wanyonge na hawawezi kwenda shule za sekondari za kulipia au shule za binafsi, lakini katika shule za sekondari za Serikali wanachukuliwa wachache, wengi wanabaki, wanakwenda wapi? Hili ni swali ambalo najiuliza kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa tu mfano, ukisoma Ripoti ya UNICEF ya mwaka 2018 inaonesha kwamba walifanya utafiti kwenye watoto milioni 3.7 wakabaini kwamba katika watoto wale milioni 3.7 wenyе umri wa miaka 14 mpaka miaka 17 ni watoto 59.1% ndio ambao walikuwa shulenii, takribani 40.9% hawakuwa madarasani, hawakuwa shulenii, walikuwa mitaani na wapo katika umri wa kupata elimu. Na watoto hawa walikuwa wamegawanyika katika makundi mawili tu, kulikuwa kuna watoto ambao hawakwenda kabisa shulenii na kulikuwa kuna watoto ambao wameacha shule. Hivi kweli Serikali inajua kwamba inalo jukumu la kutoa elimu hata kwa watoto ambao wako nje ya mfumo wa elimu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba ni muhimu Serikali itambue kuwa pamoja na juhudii inazozifanya za kuhakikisha kwamba Watanzania waasoma bila ya kulipa, lakini hata tufanye nini hatuwezi kuwa-accommodate Watanzania wote kwenda *form one* kwa sababu shule hatuna za kutosha. Kwa hiyo, kwa namna yoyote lazima tuwe na *alternative means* ya kuhakikisha kwamba, hawa watoto wanapata elimu kwa sababu wapo wanaoacha shule kwa sababu ya mimba, utoro, migogoro ya kifamilia na wapo wanaoacha kwa sababu ya uyatima. Baada ya kuacha shule ambazo ni shule rasmi za Serikali sisi kama Wabunge tunao wajibu wa kuiambia sasa Serikali ichukue majukumu haya ya kuhakikisha kwamba, watoto hawa wanapata elimu kwa sababu, nao ni watoto ambao wanahitaji kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nizungumze kitu kimoja, tunayo Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ambapo inaonesha takwimu zake kutoka mwaka 2004 mpaka mwaka 2017 imepitisha takribani watoto 159 kumaliza kidato

cha nne, 159,000 yaani 150,000 kumaliza kidato cha nne. Hawa watoto ni wachache, maana yake Serikali katika watoto karibu milioni ambao tunawaacha kila mwaka wasioweza kuingia shulenii au wanaoacha shule tunawaacha wakiwa mtaani. Hii ina maana kwamba kila tunavyozidi kwenda mbele ndivyo kiwango cha watu wasiojua kusoma na kuandika kinaongezeka. Ndivyo kiwango cha watu ambao hawamalizi kidato cha nne kinaongezeka, ndivyo kiwango cha watu ambao hawamalizi hata darasa la saba kinaongezeka. Jukumu letu ni nini Serikali katika jambo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawataja bado vijana ambao hawapo katika umri wa shule ya msingi, wapo katika umri wa shule ya sekondari, wako mtaani. Wana ari ya kutaka kusoma, hawawezi kwa sababu ya umaskini, tunafanyaje kama Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu tunayoitoa kwa wanyonge kwa walio ndani ya shule inapaswa pia, tuitoe kwa wanyonge kwa walio nje ya shule kwa kupitia mfumo wa elimu ya watu wazima pamoja na kwa kutumia nje ya mfomo rasmi. Naomba Serikali iangalie maeneo haya, lakini pamoja na mambo mengi niliyozungumza kama sehemu ya kupata marekebisho katika mpango wetu, naunga mkono hoja ya Serikali. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chuachua. Tuanendela na Mheshimiwa Hamidu Bobali atafuatiwa na Mheshimiwa Desderus Mipata na Mheshimiwa Edward Mwalongo ajiandae.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia na kunijalia mimi jioni ya leo kupata fursa ya kuweza kushauri machache ambayo yanaweza, kama mtaamua kuyasikiliza na kuyafanya kazi yanaweza kutusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo swali moja kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango. Naomba tu kwanza Mheshimiwa Mpango anijibu atakapokuja kwenye kufanya majumuisho,

ama atujibu Watanzania, kilio kikubwa cha Watanzania ni kwamba watu hawana fedha mifukoni, yaani mifukoni fedha hakuna, kwenye mabenki fedha hakuna, kwanza tunataka tujue fedha ziko wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, kinachoshangaza zaidi, mie sio mchumi mtatusaiia nyie wachumi, kinachoshangaza zaidi kwamba fedha mfukoni hakuna, benki hakuna fedha, halafu kuna mfumuko wa bei, sasa kiuchumi hii inakuwaje? Yaani fedha, *purchasing power* ya watu imepungua mifukoni, lakini pia kwenye benki watu hawana pesa, halafu kunakuwa na *price fluctuation*, hii inakuwaje kwenye uchumi? Kwa kawaida watu wanapokuwa na fedha nyingi mifukoni ndio panapotokea na hiyo *boom*, sasa inakuwaje kwamba watu hawana fedha, halafu kumekuwa na mfumuko wa bei?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tusaidie na watu hawana fedha kweli kweli, hawana fedha kabisa na sio watu tu hata makampuni tunashuhudia sasa *TTCL* juzi wametangaza kupunguza wafanyakazi 500, *TBL* huko ndio watu wako hoi kabisa na makampuni mengine tunajua namna hali ilivyo, sasa hilo ni swali langu la kwanza Mheshimiwa Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili wakati nachangia ninaomba niishauri Serikali, tumelisahau sana sekta ya gesi na tumeisahau bila kujua kwa nini tunafanya hivi, wakati Serikali hii hii ndio iliyowaahidi Watanzania kwamba, itaibadili Mikoa ya Lindi na Mtwara kuwa Qatar ya Afrika, lakini pia Serikali hii hii illuaminisha Watanzania kwamba kwa kupitia uchumi wa gesi tutakuwa na umeme wa uhakika, tutakuwa na viwanda vingi vya mbolea, tutakuwa na viwanda vya *menthol*, kutakuwa na viwanda vya *Liquified Natural Gas* pale Lindi, tutakuwa na vitu vingi, tuliahidiwa na Serikali hii hii, leo tumeifikia wapi kwenye gesi? Tunaomba maelezo Mheshimiwa Mpango. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi nilikuwa nasoma taarifa kwenye mtandao mmoja, *Hydro-carbons Technology*

*Limited* ambao ndio wanatoa sana taarifa za gesi. Russia ambao ndio *leading* na *super powerwa* gesi duniani ambao wana *cubic litre* karibu milioni 47,000 wao ndio wanaouza umeme karibu 60% ya umeme wa Ulaya unatoka Russia na hili mnalifahamu, lakini sisi umeme wa gesi Watanzania hatuutaki tunaona sijui kwamba una gharama, tunaachana na umeme wa gesi tunaenda kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajabu ambalo ni jambo la hatari sana, nilikuwa nafuatilia taarifa kwenye mtandao, sisi mpaka sasa ni nchi ya 22 kwa kuwa na *reserve* nyngi ya gesi, kwa taarifa zilizopo mpaka Januari, 2017 ni nchi ya 22 duniani. Msumbiji ni nchi ya 15 na mkumbuke gesi ya Tanzania iko kwenye eneo moja na gesi ya Msumbiji, ni pale *Ruvuma Basin* ambayo wenzetu tayari sasahivi wameshagundua na wanaitumia karibu milioni mbili *cubic litres* hizo kwenye *trillion* huko, hata mahesabu yake sijui, 2,100,086 sisi tuko kwenye milioni 1,068,000 wakati sisi tunagundua gesi, Msumbiji walikuwa bado hawajaanza matumizi ya gesi. Kwa hiyo, wana-*extract* gesi nyngi ambayo gesi ni kitu kinachohama, *probably* watakuwa wanaichukua gesi hata hii ambayo sisi ingekuwa tungeweza kui-*extract* kwenye eneo la Tanzania. Mwisho wa siku tutakuja kujikuta kwamba, gesi yote ya *Ruvuma Basin* imetumika Msumbiji, sisi hatuna gesi ya kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mpango hili liangalie sana, gesi ile pale Msimbati pale, *Mnazi Bay*, iko mpakani kabisa kati ya Tanzania na Msumbiji na wenzetu mpaka sasa wana *plantza LNG* tatu ambazo wana-*export gas* sasa hivi, sisi hatuna hata moja. Kulikuwa na mpango wa kujenga mitambo ya *LNG* pale Lindi, pale Likong'o na mpakani kabisa kwenye eneo la jimbo langu na watu mmekwenda, mmeefanya tathmini kwamba mnataka kulipa fedha bilioni tano mkatumbia kwenye mpango wa mwaka juzi, wa mwaka jana kwamba mmetenga, mpaka leo hata mtu mmoja hamjamlipa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuambieni mtakapokuja kujibu kwamba, mnaachana kabisa na

mipango ya gesi, mnaachana kabisa na mipango ya *LNG* ili tuweze kujua kwa sababu kule Lindi na Mtwara tunaishi kwa matumaini tukijua *LNG* itakuja kumbe kitu chenyewe hakipo kabisa. Kwa hiyo, naomba hili tuliweke wazi na kila mtu alifahamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013 wakati watu wa Lindi na Mtwara walipofanya *riot* kuikumbusha Serikali juu ya majukumu ya wao kunufaika na gesi na mnakumbuka tarehe 16 Mei, *TPDC* walifanya *press conference* kuwajulisha umma namna gani wananchi wa Lindi na Mtwara watanufaika na ugunduzi wa gesi kule Lindi na Mtwara. Ndugu zangu, Mheshimiwa Mpango, ninachotaka nikueleze yale waliyoyasema *TPDC* jambo moja la uhakika ambalo sasa lipo ni moja tu kwamba umeme wa uhakika upo, lakini mengine yote mmetudanganya hayapo kabisa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpango hili tunapolisema naomba uli-*take very serious* na ninaona lazima tuseme kwamba tukiidharau gesi, si tukiidharau, gesi ni kimiminika kinachohama, Msumbiji wataitumia na mwisho wa siku sisi tutakuja kuvuna mabua kama alivyosema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanasema sana mbishi Mheshimiwa Mpango, haambiliki, lakini ndio tunasema hivyo. Tuliongea humu kwenye korosho na wengine tulisema kabisa kwamba ikifika mwezi wa 10 majibu yatapatikana hapa na mwezi wa 10 majibu yamepatikana ni kwa sababu hii hii ya kueleza mkatudharau. Sasa ukichukua ule msemo wa Kiswahili kwamba kama husikii la muadhini hautasikia la mchoteamaji, basi sawa tutaendelea hivyo hivyo, lakini naamini madhara yake yanatugusa sisi Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, mimi nilitaka kujua sera ya uwekezaji ya Tanzania sasa hivi wapi tumekwama? Juzi nimeona taarifa imetolewa kwamba usalama wa biashara Tanzania tumeshuka kutoka 137, aliyoisema hata mama yangu hapa Mheshimiwa Ruth Mollel, sasa hivi tuko 144. Hali ya ufanyaji wa biashara, usalama wa

biashara Tanzania tuko nafasi ya 144 duniani, tunaendelea kuporomoka, tatizo ni nini? Kwamba kadri siku zinavyokwenda sisi kibashara tunashuka, tumekwama wapi Mheshimiwa Mpango?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kengele imepigwa, jambo la mwisho Mheshimiwa Mpango ni suala la korosho. Korosho ni moja ya *giant cash crop in this country* na inatuingizia fedha kubwa. Mwaka jana imeingiza *1.3 trillion* katika nchi hii, sio kitu kidogo cha kukidharau ni jambo kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mpango tunakata kujua, tumesikia Mheshimiwa Rais amesema kwamba zingeweza kununuliwa, hebu tuge *assurance* watu wa Lindi na Mtwara; na nimemsikia Waziri anasema eti minada hii ni ya awali, sijui ile sheria haijasomwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, minada ya korosho Lindi inaanza tarehe 1 Oktoba, leo tuko tarehe 7 Novemba, ukituambia ni minada ya awali unatudanganya. Miaka yote korosho tunaanza kuuza tarehe 1 Oktoba, leo hili jambo sio la kawaida, lazima tuseme ukweli ndugu zangu, tuseme kwamba, kuna tatizo lipo na tuwaambie Watanzania kuna tatizo moja, mbili, tatu na *solution* ni hii. Mkituambia *solution* kwamba, jeshi litabangua hata kwa meno *it is not a solution*, tunaona kama mnatutania. Mtuambie *what is a way forward, solution* ya korosho iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda kule Lindi watu wananyanyaswa, korosho zinabaguliwa, korosho ambazo mwaka jana zilikuwa zinaonekana ni *super* leo watu hawazitaki na zina *content* za kutosha kwa sababu wanajua hatuna soko la uhakika mtu anakwenda anasema *content* ya korosho hii ndogo. Mheshimiwa Mpango tunaomba majibu ya uhakika korosho yetu lini tutauza na soko likoje. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimwa Bobali, tunaendelea na Mheshimiwa Desderius Mipata na baadae Mheshimiwa Edward Mwalongo na Mheshimiwa Selemani Kakoso ajandae.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi, na nimshukuru vilevile Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima, kama nitapata nafasi nitaweza kuchangia maeneo matatu, eneo la kilimo, afya na elimu na kama nafasi itaruhusu na mambo yanayohusu barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu wanaotoa pongezi nyingi sana kwa hotuba nzuri ya Mheshimiwa Mpango na utendaji mzuri sana wa Serikali ya Awamu ya Tano na hapana mashaka juu ya utendaji huu, umejidhihirisha juu ya mambo mengi ambayo ushahidi wake nitaelezea baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye kilimo. Nakubaliana sana na taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti juu ya mapendekezo anayotoa juu ya kuboresha kililimo katika kitabu chake ukurasa wa 18. Kwamba ili tuweze kwenda lazima Serikali itenye fedha za kutosha katika kuhudumia kilimo na hasa ukiona mwelekeo wetu ni mwelekeo wa viwanda, sasa huwezi kukwepa na historia inatuambia nchi zote duniani zilizofanya vizuri kwenye viwanda zilianza kuboresha kilimo, kwa hiyo hatukwepi hapo. Na kwa mtazamo wangu naona ni kama tunaenda hatujazingatia sana suala la kuimarisha kilimo. Katika kuimarisha kilimo ni lazima upatikanaji wa pembejeo uwe wa uhakika na kwa wakati na kwa bei nafuu zinazokuwa *affordable* kwa wakulima, zinazowezekana kununulika na uchumi ulipo sasa kwa wakulima.

Lakini pia kuendeleza vituo vya utafiti ili viweze kuleta matokeo bora kwa mbegu na mazao tunayofanya. Lakini vile vile kuhakikisha kwamba upatikanaji wa nyenzo za uvuvi zinapatikana bora na kwa bei nafuu na kuimarisha masoko ya kilimo na ufugaji. Mambo haya kama yatazingatiwa,

kilimo kitakwenda. Lakini ninavyoona ni kama kilimo kwetu hapa Tanzania tunaacha sekta binafsi ikiongoze, ukiwaachia sekta binafsi kwa mawazo yangu mimi, nashauri Serikali si sawa ni hatari kwa usalama wa chakula lakini pia kwa usalama wan chi yetu kwa sababu kilimo kinaajiri Watanzania wengi, na ukiachwa kiendeshwe kwa matumaini ya kusema sekta binafsi ndio itakuwa inawawezesha pembejeo na masoko unafanya makosa makubwa. Tuje na mkakati utakaowezesha kubuni mbinu za kuwawezesha upatikanaji wa haya niliyoyasema kwa wakulima, kwa uhakika na kwa wakati, lakini vilevile masoko yao. Na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ni chombo ambacho kikitumiwa vizuri na kikiwezesha, kinaweza kikaleta neema ya wakulima. Kikatafuta masoko ya ndani ya nchi nan je ya nchi nab ado mambo yakaenda vizuri kwenye kilimo. Kwa hiyo ndugu zangu naomba Mheshimiwa Waziri, uhakikishe kwamba suala la kilimo inakuwa kipaumbele cha kwanza. (*Makof*)

La pili, katika kilimo kuna uvuvi. Suala la uvuvi linavyoendeshwa na wavuvi wanaonekana kama ni balaa sasa hivi, Ziwa Tanganyika sasa hivi kuna tataruki kubwa na wananchi hawavui wamekaa na maisha ya kule *nature* yao wanategemea ziwa. Ukishaweka utaratibu ambao huwawezeshi kuingia Ziwanu maana yake wanakufa kabisa. Naomba kwa kutumia hotuba hii, Waziri anaehusika ajaribu kuangalia vijana wake aliovatuma kule, wanachokifanya sio hicho. Kwa sababu mtu anapokiuka utaratibu lazima watu wapige kelele wanajua haki zao, kwa hiyo nawaomba Serikali itupie macho kule. (*Makof*)

Sasa hivi wavuvi wanahamia ng'ambo ya DRC na kwa maana hiyo Halmashauri yetu ya Wilaya ya Nkasi leo hazina mapato sasa kwa mwezi huu wa Oktoba na wananchi wana tataruki kubwa na wananchi wa maeneo hayo hawapati hata kitoweo cha samaki. Kwa hiyo, itakuwa shida kubwa, naomba Serikali iliangularie hili na ifuatilie kwa haraka sana hali ni mbaya sasa hivi. (*Makof*)

Suala lingine ni suala la Afya, ndugu zangu suala la afya nchi nzima tumeona juhudhi kubwa sana itanayofanywa

na Serikali yetu hasa kwenye vituo vya afya na mimi kwenye Jimbo langu nimeweza kupata Kituo cha Pembe na sehemu zote. Lakini niseme tu juhudii hii ni upendo wa Serikali kuonesha kwamba ikiwa kipaumble ni afya maana yake watu watakuwa na afya na wataweza kuendeleza shughuli zingine. Niombe haya maboma yote ambayo yapo kupitia mpango huu ukajibu ukaweza kuyaezeka na kukamilisha, nchi nzima kuna zahanati nyangi sana zimejengwa, kuna vituo vya afya vingi tu, sasa kupitia mpango huu tuone kama vinaendelezwa na kujengwa. Kwenye Jimbo langu tu peke yake kuna zahanati zaidi ya 12 zilizojengwa na wananchi ziko katika hatua mbalimbali, wananchi hawaja anza kupata huduma. Kwa hiyo na tumewahamasisha na wakahamasika, sasa itakuwa tunapoenda kwenye uchaguzi kipindi kijacho itakuwa kazi kubwa sana kuelezea haya. Lakini vilevile vituo vya afya viko.

**MBUNGE FULANI:** Vingapi?

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Vingi tu nchi nzima kwenye Jimbo langu tu viko zaidi ya vinne Kasu, Kate, Namansi kule, Mbende, Wampembe, Kala bado vinatakiwa visaidiwe na wananchi wa Kala wana shida kubwa zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mipata, tunaendelea na Mheshimiwa Edward Mwalongo baadae Mheshimiwa Profesa Maghembe ajiandae.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa rehema zake na neema zake, mimi na wenzangu humu ndani hatujambo na tunaendelea na wajibu wa kuwakilisha Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Makamu wake kwa maana ya Naibu

Waziri kwa kadri wanavyofanya kazi na wanavyosimamia masuala ya uchumi wa nchi yetu. Niseme awali kabisa napongeza mpango huu naunga mkono pia hoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze na suala la kilimo. Ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa saba, kuna mahali anaonyesha kwamba mfumuko wa bei uko chini ya *numeral* asilimia tano. Sasa mfumuko huu wa bei wote tunajua kwamba kinachosababisha mfumuko wa bei uwe katika hali hiyo katika nchi yetu ni upatikanaji wa uhakika wa chakula kwa maana ya mahindi na mchele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama kweli tunataka wananchi wa nchi hii pamoja na mfumuko wa bei hii, kuwa chini namna hii waishi maisha yenyе furaha basi tuwasaidie wakulima hawa. Wakulima hawa wanaishi maisha ya dhiki sana, mahindi yao hayana soko, pamoja na kwamba mahindi haya ndio yamewezesha nchi hii sasa mfumuko wa bei kuwa chini, lakini hali ya mbolea ni mbaya sana na hali ya pembejeo ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia mahali pengine nimeona kwenye mpango anaeleza kwamba kutakuwa na uunganishaji wa matrekata ya kutosha, lakini ukifanya utafiti mdogo tu makampuni yote ya matrekta yaliyopo Tanzania unayoyafahamu, hakuna kampuni inayouza trekta zaidi ya 200 kwa mwaka mzima. Na leo hii pale Kibaha, kuna yale matrekta mekundu yale wanalamika kwamba hawajui watayauzaje kwa jinsi yalivyo mengi. Hebu tujaribu kuona tunalinganishaje mahitaji wa wakulima ya matrekta na uweseshaji kutoka kwenye taasisi za kibenki. Lakini mikopo yetu mingi mikopo rafiki kwa wakulima, mabenki mengi yamekuwa na riba ya juu sana, lakini ukienda kwenye mabenki wanasema sisi kama benki hatuna riba ya juu, riba hii imewekwa na Serikali. Sasa Serikali mnataka nini, mnataka wakulima waneemeke, mnataka kupata hela nyngi kutoka kwenye riba. Hili ni jambo ambalo mnatakiwa mliangalie kama mkulima hawezi kukukopa benki na kulipa mkopo huo, maana yake hayo matrekta hayawesi kununulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana wakulima wa mahindi wapate uangalizi maalum ufanywe utaratibu maalum wa masoko, ni kweli tunahitaji mahindi kwa chakula katika nchi, lakini vile vile tunahitaji wakulima hawa waneemeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la mnafahamu kabisa sisi kama nchi tunahitaji fedha ya kigeni. Katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini sasa hivi liko zao la parachichi. Zao hili limekosa watalaan, hebu niombe sana Serikali muangalie namna gani sasa mtazidisha wataalam kwenye hili zao kwa sababu hili zao ndio linaleta fedha za kigeni sasa. Matokeo yake sasa ni kwamba kila mteja anayekuja anakuja na *standard* zake, anakwenda kwa mkulima mwagine anasema ananunua parachichi kubwa, mwagine anasema ananuna parachichi ndogo, kwa hiyo kila mtu sasa amekuwa anaamua anachokitaka.

Lakini sio hiyo tu, hatuna nyumba maalum za kuhifadhi maparachichi kwa maana ya *park house*, lakini vilevile kuna tatizo la vifungashio vya mazao kama parachichi. Vifungashio vinakuwa *imported* lakini vina kodi kubwa na kadhalika. Kama kweli parachichi linaleta fedha ya kigeni basi naomba sana msaidie kama Serikali kuona kwamba zao hili sasa linapata mstakabali mzuri ili kusudi, wakulima wengi waneemeke, lakini vilevile hata nchi iweze kupata fedha za kigeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la miradi ya maji. Tunafahamu kwamba hatuwezi kufanya maendeleo kama hatuna maji. Lakini tunalo tatizo kubwa sana kwenye miradi ya maji, tuna fedha ambazo miaka yote tumesema ziko *ring-fenced* kwa ajili ya miradi ya maji. Lakini ukiangalia Waziri wa Maji au Wizara ya Maji hailipni wakandarasi *on time*, inachelewa sana kuwalipa wakandarasi. Hakuna mkandarasi tajiri Tanzania anafanya kazi ya maji, Makandarasi wanaofanya kazi ya maji ni makandarasi wenzetu tu malofa malofa tu, ananunua mabomba, analaza mabomba, akimaliza kulaza mabomba na yeze mwenyewe

ameishiwa, aki-*raise certificate* Wizarani *certificate* ni miezi mtatu mpaka miezi minne, haiwezekani. Miradi hii haiwezi kukamilika hata kama tunasema tunataka kumtua mama ndoo haiwezekani, utamtuaje ndoo mkandarasi halipwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba sana Serikali iangalie kwamba tunapopanga hii mipango tunaposema kwamba tunawapa wakandarasi kazi halafu wakandarasi wakishafanya kazi wa-*raise certificate* walipwe basi walipwe kwa wakati. Mkandarasi anatoa *certificate* miezi mitatu halipwi, tuliangalie sana hilo ili tuweze kusaidia.

Jambo lingine kwenye miradi, tunayo miradi ambayo ni miradi ya kuendeleza miji. Miradi hii ina mikopo kutoka *World Bank*, lakini miradi utekelezaji wake umekuwa ni wa mateso makubwa sana kwa Halmashauri zetu. Wanajenga *stand*, wanajenga masoko, wanajenga barabara, lakini wakandarasi kwenye mikataba wameandikiwa kwamba kutakuwa na msamaha wa kodi. Lakini unapopeleka msamaha wa kodi Wizarani, msamaha hautoki. TAMISEMI imefanya semina, imewaita watalaam wa Wizara ya Fedha, imeita wataalam sijui wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wamewapa semina, wamewaelimisha wanaanza kutekeleza yale waliyowaelimisha ukifika Wizara ya Fedha hakuna msamaha wa kodi.

Naomba sana kama tunapanga mipango yetu, tunawapa watu semina tujue kabisa zile semina ni gharama ya Serikali, na ni fedha ile tunaipoteza. Kwa hiyo, tunapoanza utekelezaji miradi hii basi mara moja msamaha wa kodi uweze kutoka na miradi iweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije suala la biashara. Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, biashara nyingine ambayo wanafanya ni biashara ya mazao ya misitu. Lakini sisi kama Watanzania kama kweli tunataka maendeleo kwenye hizi biashara, hebu tuangalie *style* yetu ya kufanya biashara. Mazao ya misitu ya Nyanda za Juu Kusini ni mazao ambayo yanatokana na misitu ya kupandwa ambayo ni mbao, nguzo, magogo mbalimbali, fito na mijengo mbalimbali. Lakini iko

sheria ya maliasili ambayo inakataza mazao ya misitu yasitembee usiku. Sasa unajiliza sheria hiyo ni nzuri sawa, lakini mfanyabishara anabebe mzigo kutoka Nyanda za Juu Kusini kwa maana ya Njombe, amebebe mbao, halafu akifika karibu anakaribia Dodoma kama mitaa ya huko Mpunguzi, saa 12 jioni ikifika lazima asimamishe gari alale pale. Lori la mzigo lililobebe mbao, lililobebe nguzo, lililobebe fito, linasimamishwa lilale hata kabla hata kuku hawajaingia kulala. Hivi kweli sisi tunataka kufanya maendeleo tunataka kufanya nini. Kama gari la mizigo limekaguliwa njia nzima toka alikotoka na mzigo amekaguliwa lakini anafika Mpunguzi ambako hazizalishwi mbao, haizalishwi nguzo, hakuna miti ya kupandwa lakini anapaswa kulala hapo mpaka asubuhi saa 12 jioni, aendelee na safari.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama unataka watu wawe na fedha na watu wafanye biashara, vikwazo vidogo vidogo kama hivi muwe mnavifuta mara moja ili kusudi watu wafanye biashara. Mimi sioni kama kuna sababu yoyote ya kuzuia watu wanaosafirisha mazao ya msitu hayakupandwa baada ya saa 12 jioni. Kwanza ameambiwa gari unayotumia kusafirishia liwe la wazi, amefanya gari limekuwa la wazi, usifunike na turubai, hajafunika na turubai, lakini bado anaambiwa saa 12 jioni mwisho. Ukikutwa na gari imebeba mbao saa 12:05 unapigwa faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la elimu. Tunaiendea sana Tanzania ya viwanda...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia hiyo sentensi yako ya mwisho muda wako umeisha.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Tunaiendea sana Tanzania ya viwanda, naomba sana Serikali iangalie uwezekano wa kuwa na vyuo vya uwalimu wa ufundi ili kusudi sasa waweze kutoka Walimu wengi waweze kufundisha katika shule zetu ili tuweze kupata mafundi wengi vinginevyo viwanda hivi tutawafanya vijana wetu wawe watwana, wawe watu wa kupakia maboksi, kufagia viwanja

na kuchimba mashimo ya takataka. Lakini kama tunataka vijana hawa wafanye kazi za kitaalam viwandani ni kazi za ufundi. Kwa hiyo kazi ya kwanza ni tupate walimu wa kutosha wa Ufundu na waweze kutoa elimu kwa wanafunzi ili waweze kufanya hizo kazi za ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa walimu wa sayansi hali ni mbaya sana wewe shule ni ya sekondari miaka 10 lakini haina mwalimu hata mmoja wa *physics* naomba sana hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Hiyo sio sentensi moja tena. Haya tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Maghembe, baadae Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Almas Maige ujiandae.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika mdahalo huu wa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Mwongozo wa Bajeti kwa ajili ya mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze kwanza Serikali kwa kutuletea mpango mzuri, na ningependa sana niweke msisitizo hapa na kuweza kumu-*encourage* Dkt. Mpango kwa kazi nzuri anayoifanya kule Wizara ya Fedha. (*Makof*)

Mimi nitachangia kitu kimoja tu katika sekta moja ya elimu, na nitachangia juu ya kuboresha utaratibu wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Ndugu zangu wote mnajua kwamba tunatoa karibu shilingi bilioni 500 kila mwaka, lakini kwenye vyuo vikuu bado wanabaki wanafunzi wengi hawapewi mikopo, wanafunzi wanalamika, vijana wanalamika, wazazi wanalamika na watu wale ambao wanalea watoto na kuwapitisha katika elimu wanalamika sana.

Sasa kwa mtaji huu wa shilingi bilioni 500 tukiweka marekebisho kidogo tunaweza kuwapa mikopo wanafunzi wote ambao wanapata elimu ya juu na hapa ndio ninapotaka kutoa mapendekezo.

Pendekezo la kwanza, ni kwamba badala ya mikopo kutolewa na Serikali, Serikali ishirikiane na sekta binafsi ili kuhakikisha kwamba sekta binafsi ndio inatoa mikopo, kwa hiyo mikopo itoke kwenye benki za biashara.

Pili, mikopo itolewe kwa wanafunzi wote ambao wamejunga na wana sifa za kupata elimu ya juu. Na mikopo hiyo itolewe bila riba kwa watoto wanaokopeshwa na kwa sababu watoto watakopeshwa wote, kiasi cha mikopo kitapanda kitafika mpaka shilingi bilioni 800/bilioni 900 hata trillioni moja. Lakini kwa sababu inatoka kwenye sekta binafsi haiwezi kuwa na *pressure* kubwa katika bajeti ya Taifa.

Kwa hiyo katika utaratibu huu Serikali itakuwa na wajibu wa kuzilipa benki riba ya mikopo hiyo. Kwa hiyo, kwa *estimates* ambazo nimeweka hapa kwenye karatasi hapa juu ya bahasha, kama mikopo inakuwa bilioni 500 kama ambayo inatolewa sasa benki *ziki-charge* riba ya asilimia 10 Serikali italipa shilingi bilioni 50 kila mwaka. Lakini kama benki *zita- charge* asilimia 20 basi Serikali italipa shilingi bilioni 100 na hii ni badala ya kulipa mikopo shilingi bilioni 500. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, benki zinatoa mkopo kwa wanafunzi ambao watalipa *principal* wakati wameshapata *degree* zao, Serikali itakuwa inalipa riba ya mikopo hiyo mpaka mwanafunzi amalize na mwanafunzi anatakiwa apewe *time frame* ya kulipa na kumaliza na *time frame* ipo katika mikopo ambayo inatolewa sasa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza kwenye kipindi cha sasa mpaka kwenye bajeti itakapotangazwa hapa mwaka kesho Serikali ije na mpango ambao itashirikiana na benki kuhakikisha kwamba watoto wote ambao wanakwenda chuo kikuu kila mmoja anapata

mkopo na kila mmoja analipiwa riba na Serikali, watoto watafurahi, wazazi watafurahi, wapiga kura watafurahi na Serikali itapunguziwa kiasi ambacho inatoa na kulipa kama mchango wake kwa mikopo kwa wanafunzi wanaokwenda chuo kikuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa niliseme sasa kwa sababu nina muda kidogo katika kuboresha elimu ya sekondari nchini kwetu majya ya matatizo tuliyonayo shule hazina maabara kwa miaka sita mpaka saba sasa Serikali inawahimiza wananchi wajenge maabara katika shule zile za kata, kwenye Wilaya yangu mimi nina shule 25 na ni shule mbili tu ambazo zimeweza kujenga maabara tatu zinazotakiwa, sasa mwaka huu. Serikali ije na bajeti ya kusaidia wazazi wanaojenga maabara za shule za sekondari hili shule zote ziweze kuwa na maabara kwa sababu tumenunua vifaa, lakini vifaa vyote vimewekwa stoo kwa sababu hakuna hakuna maabara kwenye shule zetu za sekondari na haiwezekani tuwe na wana sayansi ambao wanafundishwa bila maabara, hakuna wanasyansi wanaopatikana bila kupatikana maabara ya kufundishia msingi wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, mwaka huu wala tusipeleke huko mbele na hizo pesa ambazo tunaweza kusave kutokana na kupungua kwa mikopo inayotolewa na serikali tunaweza kuzitumia kujenga maabara zote zikakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho katika Mkoa wa Kilimanjaro na hasa Wilaya za Mwanga na Same kwa miaka 15 hatujapata walimu hata siku moja, walimu wanagawanywa lakini mikoa ile haipati sababu mwanzoni walikuwa wanasema wana walimu wengi kupita maeneo mengine ya Tanzania.

Kwa hiyo, walimu wanastaafu wanaondoka, wanafariki wanazikwa, wanahamishwa wanakwenda mikoa mingine lakini nafasi zao hazijazwi. Kwa miaka 15 katika Wilaya ya Mwanga tunahitaji walimu 1,005. Sasa hivi tuna

walimu 601 na upungufu mkubwa kabisa wa walimu 384 sasa kwenye shule zetu za msingi kuwa na walimu wawili, watatu, wanne, ndiyo *maximum*, watoto wanakaa shule hawafundishwi, nafasi za walimu zipo na nafasi hizo zina mishahara yake maana wale watu waliostaifu wameacha nafasi zile zina mshahara, mtu aliyefariki ameacha nafasi ile ina mshahara, mtu aliyehama amehama amechukua nafasi nyingine Wilaya nyingine pale Mwanga nafasi yake ipo. Nimeombala Serikali kwenye bajeti iliyopita, nimewapelekea Mawaziri wahusika barua kwa ajili ya kuwakumbusha nataka nikumbushe tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wa elimu ya msingi wa Wilaya ya Mwanga hawana walimu hata kidogo tunaiomba Serikali kwenye mpango huu Serikali ituletee walimu 384 ili watoto waendele kufundishwa, na kufurahia elimu ya bure illyoazishwa na Rais wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii nina unga mkono hoja iliyopo mezani kwetu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, baadae Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga wajijandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru sana kunipa nafasi hii niweze kuchangia kwenye Mpango wa Bajeti ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala afya. Tunashida kubwa sana sana ya huduma ya afya watumishi wa afya *almost* ni Tanzania nzima, kiukweli baadhi ya huduma zimeporeshwa na hata dawa zimeongezeka hospitalini lakini watu wanafika hospitalini hawapati kuudumiwa kutokana kwamba hatuna watumishi wa afya. Kwa hiyo, naomba kwenye Mpango wa Maendeleo ujao lazima Serikali iyakikishe tumepata Watumishi wa afya wa kutosha maeneo yote ya Taifa hili kwenye zahanati, zahanati moja inakuwa na wahudumu wawili au mmoja, tunasema

tunapunguza vifo vya akinamama na watoto, tume poresha zahanati, lakini mama anafika pale anajifungulia nje kwa sababu mhudumu ni moja akaangaike na wagonjwa wa kawaida, akaangaike na mama anayejifungua, ahaangaike na mama mwenye mimba ni shida, tunaomba Serikali ije na mpango namna gani kuwakikisha nchi nzima maeneo yote tunakuwa na wahudumu wa kutosha wa afya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye mpango ujao uoneshe kabisa namna kuwakikisha kwamba hospitali zote za rufaa na hospitali mikoa zinakuwa na vifaa tiba muhimu vyote kila hospitali iwe na *CT Scan* ya hali ya juu, *x-ray* ya kisasa, iwe na *ultrasound* ya kisasa na iwe na *MRI* ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Muhimbili saiv inafanya vizuri kwa sababu ina vipimo hivyo, lakini watu ni wengi na siyo wote wanaweza kuja Muhimbili, wengine wanapata shida huko mikoani walipo.

Kwa hiyo, ili kuwakikisha kwamba Watanzania wanapata vipimo watibiwe vizuri kwa kutokana vipimo vyao na uchunguzi wa kutosha kwenye mikoa yote wahakikishe kwamba kuna vifaa tiba vya kutosha na tuhakikishe hili kwamba tunalinda afya ya Watanzania na watatibiwa siyo kwa kubahatisha bali kuhakikisha wamepata vipimo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la utafiti, kiukweli katika miaka yote tunashauri hapa Bungeni hata kuingia mikataba na mataifa mengine kuweza kutenga fedha asilimia kumi ya pato la Taifa kwenda kwenye utafifi bado hatujaweza kufanya kama Taifa, huwezi kuwa na maendeleo endelevu bila kuwekeza kwenye utafiti. Ili uende kwenye kilimo vizuri lazima utafiti, ufugaji utafiti, uvuvi utafiti, huwezi leo suala la kilimo limezungumziwa sana siwezi kulizungumzia, lakini leo ukliangalia wakulima wengi wanalima kwa kubahatisha tunahitaji utafiti kwenye kilimo, utafiti kwenye pembejeo, utafiti kwenye mbolea, kwenye udongo, kwenye masoko kila kitu ni utafiti, kwa nini Serikali

aitengi fedha asilimia moja kwenda kwenye utafiti? Kwa hiyo, mpango ujao uoneshe namna gani tunatenga fedha *one percent* la pato la Taifa kwenda kwenye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine tunaomba kwenye mpango ujao uoneshe namna gani ya kuunganisha mikoa yote kwa barabara za lami, mikoa yote kwa barabara za lami mpaka sasa hivi kuna baadhi ya mikoa ambazo hakuna barabara za lami hazijaunganishwa mkoaa kwa mkoaa barabara za lami kwa sababu nchi yetu ni nchi ya kilimo wakulima wanapata shida sana kusafirisha mazao kutoka kwenye mkoaa mmoja kwenda kwenye mkoaa mwininge hakuna barabara za lami, leo kule Kaliua unakuta kuna mahindi ya kutosha, lakini mkoaa mwininge kuna shida ya mahindi, kuyapeleka inakuwa ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhakikishe kwenye mpango ujao namna gani ya kuhakikisha mikoa yote ya Tanzania na kwa barabara za lami, kwa mfano, Kaliua kuna barabara inayoanzia Katavi inakuja Kaliua inakuja Kahama inakwenda mpaka Rwanda, leo tuna mahindi ya kutosha Katavi, mahindi ya kutosha Kaliua lakini Rwanda wanahitaji mahindi barabara ingekuwepo ya kutosha imeunganishwa ingeweza kusafirisha masoko huko kuliko kutegemea pale pale au pale ndani ya mkoaa kwa hiyo lazima mpango ujao uoneshe hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine tunakwenda kwenye uchumi wa katilakini uchumi wa viwanda, hatuwezi kuwa na uchumi wa viwanda kama hakuna umeme wa uhakika na kutosha tena umeme wenye nguvu. Ni ukweli REA inajitahidi kuweza kusambaza umeme lakini ule umeme una nguvu ndogo, transforma zilizowekwa ni ndogo, mvua ikinyesha *ime-shake* hakuna, unakuta hata viwanda vidogo ambavyo viko size ya *welding*, kusukasuka na kunyoa bado wale vijana hawafanyi kazi kwa uhakika kutohana umeme hauna uhakika. Kwa hiyo, kwenye mpango ujao wa bajeti lazima tuhakikishe namna gani tunakuwa na umeme wa uhakika, tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda huwezi kuzungumzia viwanda kama umeme ni wa aina hii ambao tunao sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ije na mpango namna gani ya kuhakikisha kwamba tunajenga *substation* zote za kupokelea umeme na kusambaza umeme, kwa mfano pale Kaliua na Urambo kuna sehemu ya kujenga *substation*, ilikuwa kwenye mpango wa bajeti uliopita tunaomba itekelezeke ili tuweze kupata umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala mazingira pamoja na mabadiliko ya tabianchi. Nimeangalia kitabu cha Mheshimiwa Waziri kina sentensi moja tu inayoonesha suala la mazingira na mabadiliko ya tabia nchi, hili suala la mazingira, hili suala la mazingira ni suala gumu na ni suala ambalo ni *very serious*, lakini kiukweli Serikali haijawekeza kwenye mabadiliko ya tabianchi na kupambana na mazingira kabisa na hata ukiangalia kwenye bajeti zilizotangulia mwaka juzi/mwaka jana fedha inayotoka kwenye bajeti ya Wizara ya Mazingira ni kidogo sana asilimla kubwa inakwenda Muungano lakini bajeti ya mazingira ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeshakuwa *bare* maeneo mengi, misitu inazidi kuteketea, mbao zinaondoka, lakini hakuna mkakati lakini tuna *desasters*, tuna matetemeko ya ardhi, tuna baadhi ya visiwa vinazama, yapo matukio mengi kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi, lakini hatuoni fedha inatengwa na ukiangalia fedha inayotengwa kwenye bajeti za nyuma ni fedha ya nje kwa maana fedha ya ndani haitengwi ya kutosha na wakati mwingine haitengwi kabisa, lazima mpango ujao uoneshe namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nategemea sana mojawapo ya kitu kinachopoteza sana misitu ya Tanzania ni suala la uchomaji wa mkaa na Mawaziri wanaona wakipita kutoka Dodoma kwenda Morogoro, kwenda Dar es Salaam tunategemea makaa ya mawe itakuwa ni *solution* kutoa nishati kupunguza kukata mikaa kwenye miti, kuharibu misitu, lakini ukiangalia huku Mheshimiwa Waziri anasema makaa ya mawe, basi Serikali inaangalia kama mwekezaji huyo atakuwa na manufaa kwa Taifa. Miaka 20 kweli Serikali

inaangaliaga tu? Miaka 20 makaa tunayo hapa hapa tuweze kuyatoa ni kuya-*export* na kuyatumia, lakini tunakuwa jagwa huku tunasubiria tunasubiria tunachukua muda mrefu sana kutekeleza mradi wa kimkakati ambayo ni muhimu kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili suala la mazingira liangaliwe na huu mradi wa makaa ya mawe upewe kipaumbele cha kutosha ili tuweze kutumia nishati mbadala ili tuokoe misitu inayoteketea na tuweze kulitoa Taifa hili kwenye jangwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine tumekuwa tunaomba sana Serikali tuwe na vikosi makini vyenye uwezo wa kuweza kuokoa kwenye vyombo vyamaji. Tumeona kipindi hiki jinsi tumpata shida, watu wameteketea kwa sababu hatuna kikosi makini cha kuokoa, tumeomba miaka mingi kwamba lazima kama Taifa kwenye vyombo vyamaji, kwenye ukanda wa maziwa yote na ukanda wa bahari tuwe na vikosi makini vyamaji kuokoa, lakini leo watu wamezama kwenye maji, tunaenda kutumia wavuvi siku mbili/tatu mpaka wengine wamepoteza maisha kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba kwenye mpango ujao Serikali iweke mkakati na mpango namna ya kuwa na vikosi makini vyenye uwezo na vifaa na weledi wa kutosha kuweza kusaidia kuokoa watu pale inapotokea tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine suala la mifugo tunaiomba bajeti ijayo au mpango ujao uonyeshe vizuri namna gani ya kutumia rasilimali ya mifugo ya Taifa hili kuweza kuongeza uchumi wa Taifa kwa kiasi kinachotosha lakini pia kuweza kusaidia uchumi wa jamii ya wafugaji na Watanzania kwa ujumla. Pamoja na kuwa tuna rasilimali ya mifugo lakini bado hatujawea kuitumia vizuri. Tunaomba bajeti ijayo ioneshe maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo, ioneshe viwanda kwa ajili ya mazao ya mifugo, ioneshe ruzuku ya Serikali kwa ajili ya kusaidia kwa ajili ya kusaidia mifugo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia sentensi yako.

**MHE. MAGDALENA H.SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena. Tunaendelea na MMheshimiwa Almas Maige, baadae Mheshimiwa Boniventura Kiswagana Mheshimiwa Vedastus Mathayo.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kuniruhusu na mimi nichangie hotuba hii ya ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango kuhusu Mapendekezo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuanza kutoa maoni yangu kabla ya kusema ukweli wa utendaji wa Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais Magufuli, mimi naamini sasa masia nyumbani haaminiki, upande wa pili kule wanasema maneno mabaya ambayo hatuelewi kuhusu utendaji mzuri wa Serikali ya Awamu ya Tano. Sisi huku tunapongeza mambo mazuri yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano lakini sio sisi tu, hata nchi za nje wanapa taabu kujua lugha gani watumie neno gani watumie wamesema *magufulification* na sisi tunasema kazi tu maana yake kazi nzuri imefanyika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nitaje mafanikio yaliyotajwa hapa kweye kitabu cha Mheshimiwa Mpango pamoja na kukusifia wewe na taaluma yako wewe na dada yangu Kijiji, Naibu Waziri lakini pia watendaji wa kazi ya Wizara yako ambao wameleta mpango mzuri sana katika mapendekezo yenu ya maendeleo ya huu mwaka moja na mpango wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na ukuwaji wa uchumi. Uchumi wa Tanzania hakuwi wenyewe unakuzwa ina maana kuna watu wanafanya kazi ili uchumi

wetu ukuwe, lakini mapato ya kodi za pamoja na mapato yasiyokuwa ya kodi yamekuwa sana kulinganisha miaka mitatu iliyopita, lakini vilevile ulipaji wa madeni na mimi naomba niseme hapa ni *declare interest*, Wizara hii imenilipa madeni kama mkandarasi, wakandarasi walipolipwa na mimi naipongeza Wizara hiyo kwa sababu nilikuwa mtu ambaye niliyolipwa madeni hayo ya wakandarasi, lakini pia barabara pia mimi ni moja watu walio *benefit* na barabara inayojengwa kutoka hapa kwenda Tabora imebakia karibu kilometra 65 tu ili barabara yote iliyojengwa pale ikamilike tuwe tunatoka hapa kwenda tabora kwa muda masaa mawili/matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna reli ya *standard gauge* sitaki kuisema sana imetajwa mpaka imekuwa tunu ya Tanzania, lakini pia kuboresha shirika la ndege, mimi niseme nini. Kila mtu mwenye macho ahambiwi tanzama ndege zote zile tangu lini sisi tungeweza kupanda *dream line* ndani hapa hapa ndani lakini kila mtu ana panda *dream line* kwa faida kubwa tunaipata, lakini viwanja vya ndege pamoja na kiwanja cha Tabora kimekarabatiwa vizuri, lakini bandari imejengwa vizuri, imefungwa mitambo ya kuona vitu vya kuona mitambo ya kuona vitu vinavyopita kwenye makontena yale na kazi kubwa imefanyika ya kukamata watu wanaajaribu kuiba nyara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo mimi sisemi, kazi kubwa ya kilimo imefanyika lakini hapa nitakuwa na mapendekezo yangu baadae, lakini huduma ya afya katika Jimbo langu pamoja na zile vituo vya afya 295 vimetolewa mimi nimepata kituo kimoja ambacho kimejengwa na kila kitu sasa kipo ndani kazi ndogo iliyobakia tunaomba gari la wagonjwa ili tuweze kuwakimbiza wale wangonjwa wanaozidiwa kwenda Hospitali ya Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nishati tumesikia miradi mipya ya Kinyerezi, miradi mpya ya umeme na umeme wa REA ambao sasa utaleta maendeleo vijijini. Lakini huduma ya maji sisi upande wa Tabora tumepata mpaka maji kutoka

Ziwa Victoria mradi mkubwa na mabomba yamekaribia kabisa jimboni kwangu na kwenda Tabora Mjini, lakini pia kuamasisha makao makuu kutoka Dar es Salaam kuja hapa lilikuwa jambo lisilowezekana mbona hamshangili? Mbona hamuoneni ukweli huo kwamba tupo hapa Dodoma pamoja na kila mtu isipokuwa Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais yupo hapa, Waziri Mkuu yupo hapa, Mawaziri wote wako hapa. Jambo limekaa miaka 43 karibu hawashangai upande wa pili na hili pia hamlioni wakati mnajua tupo hapa? Lakini pia mambo ya madini mwaka huu tumepata bilioni 301 faida au mapato kutokana na madini, ilikuwaje miaka iliyopita hayakupatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maoni yangu kuhusu elimu lakini tunasoma elimu ya msingi bure jambo hili haliwezekani na halikuwezekana miaka iliyopita tunatumia zaldi ya bilioni 20 kwa mwezi kulipia watoto wetu waende shule, lakini pia usafiri wa majini, meli zimejengwa pamoja na ajali iliyotokea tunaomba Mungu awarehemu marehemu waliofariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo sasa ni change mimi mambo gani ingefaa Wizara yako Mheshimiwa Mpango ifikirie mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafute mahusiano kati ya sekta binafsi na Serikali; kuiwezesha sekta binafsi Mheshimiwa Dkt. Mpango itazalisha na kuuza uchumi wa nchi hii, duniani kote Tanzania tu ndio tunasema kwamba labda Serikali peke yake itafanya, lakini sekta binafsi ina mchango mkubwa sana katika kuuza uchumi.

Kwa hiyo, mimi napendekeza Serikali itafute jinsi ya *ku-engage private sector* tuweze kuitumia ikuze uchumi na kuongeza ajira. Lakini pia Serikali itoe kipaumbele kwa katika kurasimisha baadhi ya kazi, shughuli nydingi hapa Tanzania za wananchi hajijawa rasmi na hiyo sekta na hiyo isiyo rasmi hailipi kodi, lakini inapata mgao mkubwa wa maendeleo wa fedha za maendeleo lakini kama ingerasimishwa basi tungeweza kupata mapato makubwa kuongeza kwenye

kapu la mapato ya Serikali pamoja na kuwatengea vijana na akinamama katika Halmashauri zetu lakini hela hizo haziendi, kwa mfano katika Halmashauri ya Uyui hela zote zaidi ya milioni 400; milioni 500 zilizogaiwa hazifiki milioni 46 kwa mwaka mzima. Hili ni tatizo. Kwa hiyo, Serikali itafute njia ya kuweza kurasimisha upatikanaji wa hela za wale akina mama na vijana huko vijiji ili waweze kuleta maendeleo na kujibudu huko.

Mheshimiwa Mwenyeikiti, lakini pia Serikali ifanye kazi ya kurejesha elimu ya ufundi hapa nchini na hili ni jambo la muhimu kabisa, viwanda haviwezi kwenda bila mafundi sadifu na mafundi mchundo, ninamaanisha *artisans* na *full technician certificate people*, bila hiyo viwanda haviwezi kwenda hali hii ilikuwepo miaka iliyopita ikatokea bahati mbaya sana elimu ya ufundi imedhalilishwa, imeteremshwa mimi nafikiri ni muhimu sasa kila shule za kata ipewe somo moja la ufundi labda umeme, labda ujenzi wa mabomba na kadhalika ili tuwe na mafundi kule vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyetiki, mwisho jambo muhimu sana ni kuweza kutumia kukuza uchumi wetu ni kutumia taasisi za majeshi, katika nchi zingine kwa mfano Vietnam na sio Vietnam peke yake kwa sehemu kubwa ya maendeleo katika nchi imetumika majeshini aidha katika kufanya *research* au kuzalisha mali ambao ilikuza uchumi, sisi tuna mashirika matatu hapa makubwa sana. Shirika la Mzinga pale Morogoro lingeweza kufanya kazi kubwa sana ya kukuza uchumi wakiwezesha, lakini pale Kibaha kuna Shirika la Nyumbu ambapo wanayo *Research and Development Unit (R&D)* wangeweza kufanya kazi kubwa sana za kiuchumi na kuwa chanzo cha kukuza uchumi na kuongeza ajira. Lakini mashirika yale mawili yanetelekezwa na yanahangaika peke yake na yanatumia bajeti ya Ngome ambayo hakuna hela, Serikali ichukue jukumu muhimu la kuwezesha maeneo haya mawili tunaweza kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mpango lakini lipo Shirika la SUMA JKT ambayo pia unaweza kuwa uzalishaji mkubwa sana na juu chakula kina-*stabilize* mfumo

wa bei, Magereza wakiwezeshwa wanaweza kulima chakula cha kutosha kula watu wote lakini pia wanaweza kuleta chakula cha kutosha kuziba nafasi ya mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri nilitaka kusema hayo, lakini la mwisho kabisa niongelee kuhusu lugha ya kufindishia. Elimu ni ufunguo wa kila kitu, hakuna maendeleo bila elimu, lakini elimu yetu inawapa watoto mzigo kweli kweli. Watoto wanasona darasa la kwanza mpaka la saba kwa kiswahili na mwaka huu watoto wamefeli sana kiingereza halafu wakifika darasa la saba wakienda *form one* wana *switch frequency*, wanasona kiingereza kwanza wanapata tabu yakuelewa kiingeraza, lakini wanapata tabu ya kuelewa masoma kuna tatizo gani hapa la watu wasisome kiswahili, kwanini watoto wetu wasome kiswahili zipo nchi nydingi wanasona lugha za kwao na hata nikizitaja Ufaransa, Uingereza, Marekani, Ujeruman Urusi, China kote wanasona lugha zao na watoto wanaelewa, mimi nilikuwa kwenye mahafali mbili kwenye shule za sekondari jimboni kwangu...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kuunga hoja mkono hii asante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na baadae tutaendelea na Mheshimiwa Vedastus Mathayo.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi na kwanza naomba niunge hoja mkono mapendekezo ya mpango ulioletwa kwetu pamoja na mapendekezo na ushauri wa Kamati ya Bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mpango tufanikiwe kiuchumi, tunahitaji mali ghafi inayozalishwa nchini. Kwenye kilimo ni vizuri tukatoa kipaumbele kwenye kilimo cha umwagiliaji, tunayo mabonde mengi wengine wapo

kandokando na maziwa ni muhimu tukawekeza kipaumbele ili watu walime wakati wote, tunayo mifano ya wale ambao wanatumia *irrigation scheme* kwa mfano kule Magu tunaye Ngongoseke analima *green house*, ni *green house* nzuri ambayo imeajiri watu wengi, lakini ana uhakika na soko la biashara ya kwake. Lakini tunaye mwингine anitwa *Vick Fish* amewekeza vizuri, tunaye Mtemi Chenge hapa amewekeza vizuri kilimo cha umwagiliaji cha mpunga cha mfano. Kwa hiyo niombe sana Serikali tutoe kipaumbele kwenye uwekezaji wa kilimo cha umwagiliaji ili tuweze kuzalisha malighafi ambayo kimsingi itatumika viwandani ili kuhakikisha viwanda tulivyonavyo *material* yapo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhitaji viwanda lakini wawekezaji wetu bado wanakumbwa na changamoto nyingi kwamfano *exemption* ya viwanda kwa maana ya mitambo pamoja na *godowns* wanapata shida sana hebu tuangalie tuweze kutoa *exemption* ili wananchi wetu waweze kujenga viwanda baadae kodi tu watalipa. Kwa mfano wawekezaji wa wazawa ndani hatuwapi *tax holiday*, tukiwapa *tax holiday* wanapata namna ya kujenga uwezo ili baadae waweze kuimarika na kuweza kutoa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri sana Serikali yetu ambayo inahitaji kwa kweli uchumi wa viwanda, lakini ili tufikie kwenye uchumi mzuri na kuboresha mpango huu suala la *Stiegler's Gorge* ni jambo muhimu sana kupewa fedha za kutosha ili tuweze kupata umeme tuweze kuendesha hii hivi viwanda pamoja na mambo mengine ambayo wananchi wanahitaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya barabara kwa sababu tunapozungumza uwekezaji wa viwanda lazima tusafirishe malighafi, lazima tusafirishe bidhaa, ni vizuri ikawekwa kipaumbele kama ambavyo kwenye hotuba yako umesema umeliwekea kipaumbele, cha muhimu ni fedha zipatikane ili utekelezaji uwepo haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi ambayo wananchi wameianzisha, miradi ya afya, miradi ya elimu.

Kuna maboma mengi llani ya Chama cha Mapinduzi inasema zahanati kila kijiji sisi tumejitahidi kuhamasisha wananchi pamoja na wadau mbalimbali wamejenga maboma ya kutosha. Kwenye mpango huu tuone namna ya kuweza kukamilisha tunapokuja kwenye bajeti tuweke fedha za kukamisha maboma haya ili wananchi wawewe kupata huduma wanayoihitaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe wataalam, wachumi wabobezi watueleze sisi Wabunge na watueleze wananchi hivi umaskini mnaupima kwa namna gani? Kwa sababu hapa asubuhi kila mmoja anazungumza uchumi, wabobevu wa uchumi mtueleze uchumi mnaupima kwa namna gani, kwa sababu unaweza leo wewe watu wasema wananchi hawana fedha mfukoni, unaweza ukawana na fedha mfukoni lakini huwezi kusafiri kwa sababu miundombinu haipo, huo ni uchumi; unaweza ukawa na fedha mfukoni lakini huduma ya afya ukakosa huo ni uchumi? Unaweza ukawa na fedha mfukoni ukakosa elimu nzuri huo ni uchumi? Leo vyuo viro umaskini wa elimu watu hawana, mtueleze kwamba uchumi manaupima kwa namna gani kwa sababu nchi hii imepiga hatua sasa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona wananchi wake leo kule vijiji wanashindana kujenga nyumba nzuri huo sio uchumi? Wanashinda kusomesha huo sio uchumi? Wanashindana kuishi maisha bora huo sio uchumi? Tunaupima uchumi kwa namna gani, uchumi wa kukosa hela mfukoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wachumi wabobevu mueleze jambo hili mnaupimaje, kwa sababu tumeweza kuwa tunapata taabu, halafu mimi nashangaa sana ndio maana Mwenyenzi Mungu wakati anataka kuumba nchi, mbingu na dunia hakuumba kwanza mwanadamu, aliona akiumba mwanadamu atampa taabu kuumba mambo yote ambayo aliyafikiria kuyaumba. (*Makofii*)

Sasa mimi niwaombe na wale wote manao hangaikia Katiba, Katiba yetu haiwezi kuwa inajadiliwa na

watu 600 na kama mtaamua Serikali kuleta Katiba wakae  
watu wachache wabobevu, wachache waweke mpango  
mzuri wa namna Katiba yetu sio watu 600 ndio maana  
nasema hivi Mungu alipotumba wanadamu hapa Tanzania  
kwa awamu hii ni kama aliumba mapacha wanne.  
Akamuumba John Magufuli, akamuumba Samia,  
akamuumba Majaliwa, akamuumba na Dkt. Mpango. Yale  
mnayoyafanya ninyi watu wanne fanyeni hivyo hivyo, kwa  
sababu tukitaka watu wote tutoe mawazo yetu tutapotosha  
Taifa. Kwa hiyo niwaombe sana, tunapoleta mapendekezo  
ya mpango kazi yetu sisi Wabunge ni kushauri ili tuweze  
kuboresha mpango wenyewe. (*Makof*)

Kwa hiyo, Serikali imefanya kazi kubwa na naendelea  
kuipongeza Serikali. Leo ukienda Dar es Salaam barabara  
zinajengwa kila mahali, ukienda Arusha barabara zinajengwa  
kila mahali, ukienda Mwanza barabara zinajengwa kila  
mahali, ukienda Mbeya barabara zinajengwa kila mahali,  
tunataka uchumi wa namna gani? Tunataka viongozi wa  
namna gani fanyeni kazi wala msikatishwe tamaa wananchi  
wapo bega kwa bega na ninyi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji nchi iliyotulia,  
tunahitaji vyombo vyaya ulinzi na usalama vilinde raia wake,  
unajua watu tunasema watu wanakufa, duniani kote watu  
wanakufa na hili jambo la kawaida, unajua tusifanye iwe  
hoja, kutekwa kwa ma-billionaires tusifanye iwe hoja, duniani  
kote watu watekwa. Ndio maana vyombo vyetu vyaya ulinzi  
wa Kangi Lugola linda raia wako. Hakuna mahali popote  
nchi hailindi raia wake, ndio maana hata Mwenyezi Mungu  
kule mbinguni analindwa na jeshi kubwa la malaika, kwa  
hiyo, lazima watu wote walindwe, tuimalishe lakini tuwape  
angalau namna ya majeshi yetu kadri ambavyo wanaulinda  
tuwaongezee uwezo wa kuweza kukabiliana na matatizo  
hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono  
hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiswaga. Tunaendelea na Mheshimiwa Vedastus Mathayo.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika haya maandalizi ya mpango wa bajeti 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nianze kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango pamoja Naibu wake kwa maandalizi ya mpango mzuri na niseme tu kwamba katika mpango huu yapo yale mambo ambayo yamepewa kipaumbele kama kuendelea kufanya kazi ya ununuzi wa ndege, lakini vilevile mradi wa *Stiegler's Gorge* pamoja na wa reli ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia leo katika nchi yetu Tanzania ni nchi ambayo tuna vivutio vingi vya watalii, lakini ni kwamba wenzetu Wakenya wanatushinda watalii kwa wingi na mapato ya utalii ni kwa sababu hatuna *direct flight* za kuja Tanzania. Kwa hiyo, leo nilipoona humu tunataraji kwa na *direct flight* za kutoka China kuja Tanzania, kutoka India kuja Tanzania huo ni mwanzo mkubwa na mwanzo mzuri unaonyesha tunatarji na sisi kupata mapato ya fedha za kigeni kutokana na watalii kwa hiyo nasema *big up* katika hilo. Lakini ukiangalia mradi wa *Stiegler's Gorge* ambaao baadhi yetu tunaubeza tunatambua kwamba ili nchi yetu iweze kuendelea inahitaji muwekezaji na mwekezaji yoyote akitaka kuwekeza moja wapo ya *factor* kubwa anayoingalia ni gharama ya uendeshai ambayo anakwenda kwenye umeme.

Kwa hiyo, wote tunafahamu gharama za umeme wa maji kwa namna zilivyo chini, kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba tuna nafasi kumbe ya kuvutia watu wengi wawekezaji wengi kuleta viwanda vyao nchini. Kwa sababu ya gharama za umeme tunatarja kuwa chini, kwa hiyo, tunaendelea kuishukuru Serikali kwa mpango huo. Lakini Mheshimwa Dkt. Mpango nikuombe tu ufanye jambo ambalo

ni la haraka na litaonesha matokeo ya haraka. Kwenye huu mpango wa reli ya kisasa leo Watanzania wengi tukiwemo Mikoa ya Mara, Mwanza, Kagera pamoja na wote ambao usafiri wa Dar es Salaam kuja kwenye mikoa yetu tunatumia zaidi ya siku moja maana yake abiria lazima walale njiani.

Sasa kwa sababu tumeona kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro ni kilometra 300 na mpaka sasa umeshatengeneza 24% ni mategemeo yangu by mwaka kesho au mwaka kesho kutwa mwanzoni kile kipande kitakuwa kimekamilika. Sasa nini kifanyike wakati huu ujenzi unaendelea hebu tuanze kabisa kununua vichwa vyta tayari tayari kwa ajili ya treni, kwa ajili ya kuleta abiria hapo, pamoja na mabehewa lakini pamoja na *stand* kwa ajili ya mabasi, matokeo yake yatakuaje kutoka Dar es Salaam treni iwe inaondoka saa 11 naamini saa 12 itakuwa Morogoro, abiria wote wa mikoani wakipanda pale saa 12 tafsiri yake kwamba hakuna abiria hata mmoja atakayelala njiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaamini huo mpango peke yake utaanza kuonesha matokeo ya haraka wakati huo ujenzi wa reli kadri unapofika kwenye kituo kimoja mfano ukifika Dodoma utaratibu mwingine unaendelea yaani huduma zote zinaendelea kupatikana kuliko tutakaposema tusubiri tujenge kwa muda mrefu au kipande kirefu halafu ndipo hizo huduma zianze kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya kuwa nimesema hayo sasa katika mpango huu wa 2019/2020 wote tunafahamu kwamba kilimo ndio uti wa mgongo, kilimo kinachukua 70% ya Watanzania, nini kifanyike kwenye upande huo hebu kama tunahitaji kuajiri watu wengi na maisha yetu yawe mazuri lazima tujikite kwenye kilimo cha umwagiliaji na tutakapojikita kwenye kilimo cha umwagiliaji na tutakapojikita kwenye kilimo cha umwagiliaji tutambue mabonde yaliyopo katika nchi hii na mabonde hayo leo tunaweza kuamua mfano tusema tunalima mpunga, katika mabonde yote tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya kuwa nimesema hayo sasa katika mpango huu wa 2019/2020 wote tunafahamu kwamba kilimo ndio uti wa mgongo, kilimo kinachukua 70% ya Watanzania, nini kifanyike kwenye upande huo hebu kama tunahitaji kuajiri watu wengi na maisha yetu yawe mazuri lazima tujikite kwenye kilimo cha umwagiliaji na tutakapojikita kwenye kilimo cha umwagiliaji na tutakapojikita kwenye kilimo cha umwagiliaji tutambue mabonde yaliyopo katika nchi hii na mabonde hayo leo tunaweza kuamua mfano tusema tunalima mpunga, katika mabonde yote tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuzungumza zao la mpunga kwanza ni zao la biashara, lakini vilevile ni zao la chakula, lakini vilevile nchi zote zinazotuzunguka ni nchi ambazo zinahitaji mchele wa Tanzania. Ukienda Kenya, Uganda, Rwanda, Kongo na Zambia, mchele wa Tanzania ukiruhusiwa tu kuuzwa unao kila nchi unaupenda. Sasa nini kifanyike tukishaanisha hayo mabonde wakati mwingine tunaweza kutangaza wakandarasi kama tunavyotangaza kazi za bararaba. Tukasema tunahitaji mkandarasi hekta 2000 hizi zipo hapa, basi tunachohitaji wewe mkandarasi weka miundombinu ya *irrigation* watu watalima mfano zao moja kama niilivyo sema la mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia zao la mpunga, mpunga ni zao hakuna kinachotupwa yale mabaki yake kwa maana ya majani mifugo inakula, zile pumba hata wale wachoma matofali sasa hawataharibu mazingira kwa kukata mita watatumia kuchomea matofali. Lakini sisi wote ni mashaidi zile wanaita *rice polish* kwa maana zile chenga zake ndio tunakula vitumbua, lakini na mchele wake tunauza.

Kwa hiyo, kumbe ni imani yangu kwamba kwa kulima mpunga ni zao ambalo linaweza likamsaidia Mtanzania ye yote yule na likapandisha kipato chetu na hela yenye we haina kwamba soko limeanguka kwa sababu mahitaji ya soko yapo ndani na nje ya nchi. Kwa hiyo ni imani yangu

tukikipa kilimo kipaumbele cha kwanza hasa kilimo cha umwagiliaji itatusaidia sana katika kuukomboa na kunyanya kipato cha Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipaumbele cha pili tufanye nini1 Kwangu mimi kipaumbele cha pili tukipeleke kwenye suala la uvuvi. Kwa bahati mbaya watanzania wengi kila fursa tunayoipata inabadilika tena inakuwa hatari kwa watu wetu. Leo wale watu waliopo baharini, waliopo Ziwa Tanganyika, waliopo Ziwa Victoria ni kilio kitupu. Ni kilio kitupu kwa sababu badala ya yetu sisi tuone namna kuwasaidia, kazi yetu ni kwamba mtu amekosea anapigwa faini ambayo haiwezi. Kwa hiyo, wale watu wetu wengine wanafungwa, kwa hiyo hali ya maisha inakuwa ngumu, lakini nini kifanyike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ili watu wetu tuweze kuendeleza uvuvi, ili wale watu wetu waweze kuthamini maana ya uvuvi, kinachopaswa kufanyika hebu Serikali itenye fedha, tuwe na uvuvi ule ufugaji wa kufugia ziwani, ufugaji wa kufugia baharini kwa maana ya kutengeneza zile *cage*, ukishalianzia lile kwa vyovyote vile uvuvi haramu hautakuwepo kwa sababu wale wananchi wenyewe amba ni wafugaji wa samaki wao wenyewe ndio watakaokuwa walinzi wa ziwa letu na walinzi wa bahari zetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwa kufanya hivyo kwanza watakuwa wanapata kipato lakini vileyile watakuwa walinzi wazuri katika maziwa yetu na bahari zetu kwa kuhakikisha kwamba uvuvi haramu haufanyiki. Lakini hata zile fedha ambazo watu wa *patrol* huwa wanawatoza wakienda kuwakamata wakati mwingine huwa wanawatoza shilingi milioni mbili mpaka shilingi milioni tano zile fedha zinapaswa ziwarudie, zirudi kwa kutengeneza miundombinu kama hiyo ili watu wetu waendelee kuona umuhimu wa uvuvi na imani yangu kwamba mambo yatakuwa mazuri na wale watu wetu watafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo katika ushauri wangu tunapaswa tujikite, katika kuwasaidia wananchi wetu na Watanzania wetu, ni ukweli usiopingika kwamba leo yupo mtoto anasoma mpaka chuo kikuu, anatoka na *bachelor* yake ya *sociology*, lakini huyo mtoto ukimchukua na yule mtoto ambaye amesoma *VETA* akamaliza, huyu wa *VETA* bado yupo *better of* kuliko yule ambaye ana *degree* yake ya *sociology*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta kwamba mpaka leo kipaumbele kikubwa tunakitoa zaidi kuhakisha kijana asome mpaka *degree* yake, kumbe kati ya eneo ambalo tunahitaji kuliendeleza tunapaswa kuendeleza maeneo ya vyuo kwa maana hivi vyuo vya *certificate* na *diploma* ambavyo watu wetu wataendelea kupata ujuzi na itawasaidi zaidi katika kujajiri kuliko huu utaratibu ambao tunathamini zaidi wale watu ambao wana *bachelor* kumbe wakati mwingine *bachelor* yake anazidiwa na mtu mwenye *certificate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja na kupongeza sana, ahsanteni sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mathayo. Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa kazi ya leo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 8 Novemba, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*